# MFUMO WA
# UCHUMI WA SOKO JAMII
# KWA TANZANIA

KUELEKEA MAENDELEO YA UCHUMI
JUMUISHI NA ENDELEVU

ISBN: 978-9987-716-14-2

**Machi, 2019**

© Konrad-Adenauer-Stiftung e. V. (KAS)

Sehemu yoyote ya kitabu hiki inaweza kunakiliwa na kubadilishwa kukidhi mahitaji yanayotakiwa bila kuomba idhini ili mradi mwenye haki miliki ajulishwe na machapisho yote yatolewe bure. Machapisho yoyote ambayo ni kwa ajili ya biashara yatahitaji kibali kutoka Konrad-Adenauer-Stiftung e. V.

Konrad-Adenauer-Stiftung e. V. itashukuru kupatiwa nakala ya chapisho lolote ambalo sehemu ya maandishi au vielelezo vyake vimenukuliwa kutoka kwenye kitabu hiki.

Utayarishaji na uchapaji wa chapisho hili umefadhiliwa na Konrad-Adenauer-Stiftung e.V.

Angalizo: Maoni yaliyotolewa na waandishi wa kitabu hiki ni ya kwao wenyewe, wala si msimamo wa KAS.

KONRAD
ADENAUER
STIFTUNG

S.L.P 6992
Mtaa wa Ismani, Upanga
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2153174
www.kas.de/tanzania

# Yaliyomo


**Orodha ya Vifupisho** .................................................................. **v**

**Orodha ya Vielelezo na Majedwali** .......................................... **vii**

**Orodha ya Viambatisho** ............................................................ **viii**

**Dibaji** ........................................................................................... **ix**

**1. Utangulizi** ................................................................................ **1**

**2. Historia ya Kinadharia ya Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii** ........................................................................................... **3**

2.1. Kanuni na Taratibu za Kiuchumi ...................................... 3
*2.1.1. Mfumo wa Uchumi wa Kijamaa* .............................. 3
*2.1.2. Uchumi wa Soko Huria/Ubepari* .............................. 4
*2.1.3. Uchumi wa Soko Jamii* ............................................ 4

2.2. Sifa za Uchumi wa Soko Jamii .......................................... 4
*2.2.1. Utangulizi* ................................................................ 5
*2.2.2. Uchumi wa Soko Jamii – Wadau na Majukumu yao* 7
*2.2.3. Kanuni, Nguzo na Malengo ya Uchumi wa Soko Jamii* 9

2.3. Manufaa ya Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii ............ 13

**3. Uchambuzi wa Hali ilivyo Nchini Tanzania** ........................ **16**

3.1. Historia ya Maendeleo ya Kiuchumi Nchini Tanzania ... 16

3.2. Maendeleo ya Uchumi Mkubwa na Uchumi wa Kati/Mdogo ........................................................................ 18
*3.2.1. Vigezo Muhimu vya Uchumi Mkubwa* ..................... 18
*3.2.2. Mambo Muhimu katika Uzalishaji* .......................... 25
*3.2.3. Sekta Muhimu* ......................................................... 28

3.3. Maendeleo ya Jamii ........................................................... 33
*3.3.1. Hifadhi ya Jamii* ...................................................... 33
*3.3.2. Afya, Uzazi na Vifo* .................................................. 35
*3.3.3. Makundi Yaishiyo kwenye Mazingira Magumu* ....... 39

3.4. Maendeleo ya Kisiasa ....................................................... 42

*3.4.1. Sera ya Elimu* ........................................................ 44
*3.4.2. Nguvu Kazi na Sera ya Ajira* ................................... 46
*3.4.3. Sera ya Ushirikiano wa Kimataifa* ........................... 47

3.5. Maendeleo ya Kiteknolojia (Sayansi, Teknolojia na Ubunifu) ........................................................................ 48

3.6. Maendeleo ya Mazingira ................................................ 49

3.7. Uchambuzi Yakinifu wa Kutambua Uwezo - Nguvu - Udhaifu - Fursa na Changamoto za Tanzania ............... 53

**4. Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii kwa Tanzania** .......... **56**

4.1 Dira na Dhima ................................................................ 56

4.2 Nguzo za Kimaadili ......................................................... 57

4.3 Mikakati .......................................................................... 60
*4.3.1 Mipango na Uratibu* ............................................ 62
*4.3.2 Mali Binafsi* .......................................................... 67
*4.3.3 Utaratibu wa Fedha* ............................................. 69
*4.3.4 Utaratibu wa Biashara* ......................................... 73
*4.3.5 Utaratibu wa Ushindani* ....................................... 79
*4.3.6 Utaratibu wa Kimataifa* ........................................ 84
*4.3.7 Utaratibu wa Matumizi ya Fedha* .......................... 85
*4.3.8 Utaratibu wa Kijamii* ............................................ 90
*4.3.9 Eneo la Kuzingatia: Sekta ya Kilimo* ....................... 100

4.4 Hatua za Utekelezaji ...................................................... 104
*4.4.1 Utekelezaji wa SMET Kupitia Jumuiya za Dini* ........ 104
*4.4.2 Utekelezaji wa SMET Kupitia Wawakilishi wa Kisiasa* ........................................................................ 105
*4.4.3 Utekelezaji wa SMET kupitia Sekta Binafsi na ya Umma* ........................................................................ 105
*4.4.4 Utekelezaji wa SMET kupitia Asasi za Kiraia* .......... 106

**5. Hitimisho** ........................................................................ **107**

**Viambatisho** ...................................................................... **108**

**Rejea** ................................................................................ **112**

# Orodha ya Vifupisho

| | |
|---|---|
| AfDB | Benki ya Maendeleo Africa |
| ATE | Chama cha Waajiri Tanzania |
| BAKWATA | Baraza Kuu la Waislamu Tanzania |
| CBT | Bodi ya Korosho Tanzania |
| CCT | Jumuiya ya Kikristo Tanzania |
| CETA | Chama cha Walimu wa Somo la Uraia Tanzania |
| CTI | Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania |
| CWT | Chama cha Walimu Tanzania |
| EAC | Jumuiya ya Afrika Mashariki |
| FCA | Sheria ya Ushindani |
| FCC | Tume ya Ushindani |
| FDCs | Vyuo Vikuu vya Maendeleo |
| GATT | Mkataba wa Kimataifa juu ya Forodha na Biashara |
| GEPF | Mfuko wa Pensheni wa Mafao ya Kustaafu |
| IMF | Shirika la Fedha la Kimataifa |
| NACTE | Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi |
| NHIF | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya |
| NPF | Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi |
| NSSF | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii |
| PPF | Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma |
| PSPF | Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma |
| PSRC | Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma |
| SDGs | Malengo ya Maendeleo Endelevu |
| SMEs | Biashara Ndogo na za Kati |
| SMET | Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii kwa Tanzania |
| SSRA | Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii |
| TaESA | Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania |
| TANESCO | Shirika la Umeme Tanzania |

| | |
|---|---|
| TCCIA | Taasisi ya Biashara, Viwanda na Kilimo |
| TCU | Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania |
| TEC | Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania |
| TNBC | Baraza la Taifa la Biashara |
| TPSF | Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| TRC | Shirika la Reli Tanzania |
| TRL | Kampuni ya Reli Tanzania |
| TTCL | Kampuni ya Simu Tanzania |
| TUCTA | Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania |
| UN | Umoja wa Kimataifa |
| VAT | Kodi ya ongezeko la thamani |
| VECs | Vituo vya Elimu ya Ufundi |
| VETA | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi |
| WTO | Shirika la Biashara Duniani |
| ZATUC | Shirikisho la Vyama vya Wanyakazi Zanzibar |
| ZECO | Shirika la Umeme la Zanzibar |
| ZRB | Bodi ya Mapato Zanzibar |
| ZSSF | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar |

# Orodha ya Vielelezo na Majedwali

**Vielelezo**


Kielelezo 1: Changamoto za Sekta ya Uzalishaji Mali Tanzania 24

Kielelezo 2. Ajira Nchini Tanzania – Muundo na Takwimu ....... 27


**Majedwali**


Jedwali 1: Viashiria Vinavyoonesha Ufanisi wa Sekta ya Uzalishaji mali za Viwandani ..................................... 24

Jedwali 2: Nyenzo za Uzalishaji Mali ......................................... 25

Jedwali 3: Viwango vya Urahisi wa kufanya Biashara na Viashiria vyake (2015-2017) – Tanzania .................... 32

Jedwali 4. Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto .................. 54

## Orodha ya Viambatisho

Kiambatisho Na. 1: Orodha ya Mashirika ya Umma Tanzania..108

Kiambatisho Na. 2: Taasisi na Mashirika ya Umoja wa Mataifa nchini Tanzania ............................................ 111

## Dibaji

Tanzania imepitia kwenye maboresho mbalimbali ya kiuchumi tangu ipate uhuru ikiwemo Azimio la Arusha mwaka 1967 na soko huria mwaka 1986. Azimio la Arusha lililenga kuleta matumaini ya usawa, umma kumiliki na kuendesha njia za uzalishaji huku lengo kuu likiwa ni kufikisha mahitaji na huduma za jamii katika maeneo ya vijijini kwa urahisi zaidi. Lengo la Soko huria lilikuwa kuleta bei halisia ya soko na kurahisisha upatikanaji wa bidhaa. Mabadiliko hayo yalikuwa ya lazima kwa mazingira ya wakati huo. Aidha jitihada nyingi zimekuwa zikifanyika ili kuinua hali ya maisha ya Watanzania.

Hata hivyo, mpaka sasa watu wengi bado ni masikini na rasilimali za nchi zinaendelea kupungua. Bado watu wanatembea umbali mrefu kutafuta chakula, maji, elimu na huduma za afya. Kiuchumi, uzalishaji katika sekta binafsi haumilikiwi na wazawa baadala yake nchi inategemea makampuni kutoka nje. Aidha ukuaji wa uchumi hauakisi maendeleo ya uchumi wa taifa. Baadhi ya Watanzania hawawezi kumudu hata mlo mmoja kwa siku na wengine wanakufa kwa kukosa huduma za afya. Kiwango cha ujinga kinaonekana kuongezeka, miundombinu yetu ya elimu haikidhi ongezeko kubwa la watoto wanaoandikishwa katika elimu ya msingi huku mfumo wetu wa elimu ukiwa haukidhi mahitaji na vigezo vya ajira. Sekta ya kilimo ambayo tunasema ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi, bado haitoi matokeo ya uhakika. Hali hii inapelekea kutafuta mbinu mpya, mawazo mapya na mwelekeo mpya kwa manufaa ya kizazi cha leo na kijacho. Kitabu hiki ni mahususi kwa ajili ya kutoa mchango katika juhudi zilizokwishachukuliwa ili kukwamua uchumi wa nchi na kuleta maisha bora ya watu wake.

Hali ilivyo sasa inaashiria kuwa ni lazima nchi iwe na mfumo mpya wa uchumi ili iweze kufikia malengo ya kuwa nchi ya uchumi wa kati. Somo tunalojifunza kutoka baadhi ya nchi za Ulaya hasa Ujerumani, nchi mbalimbali duniani pamoja na uzoefu wetu kutokana na mabadiliko ya uchumi yaliyopita hapa nchini tangu taifa lipate uhuru vinatusukuma kuuendea mfumo wa Uchumi

Jamii, ambao umeonesha mafanikio makubwa katika maendeleo ya uchumi jumuishi. Ikiwa Tanzania itaridhia kuutumia mfumo huu wa uchumi itapiga hatua ya juu sana kiuchumi na kuwa taifa lenye nguvu kiuchumi na ushindani wa soko kikanda na kimataifa kutokana na mazingira yake yalivyo. Uzoefu mkubwa wa waandishi wa kitabu hiki ndio unaowasukuma kuutambulisha muundo wa Uchumi Jamii ambao unaendana na mazingira ya nchi. Kitabu hiki kinawasaidia wasomaji kufahamu maana ya Uchumi Jamii, tathmini ya hali ya kiuchumi na kijamii nchini Tanzania kwa sasa (ikijumuisha uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto), muundo huu mpya wa Uchumi wa Soko Jamii kwa Tanzania unajumuisha tunu zake, mikakati ya namna ya kufikia malengo na jinsi utakavyotekelezwa.

Kwa msaada wa shirika la Konrad-Adenauer-Stiftung e. V., kitabu hiki kimeandaliwa na timu ya wataalamu, ikiwajumuisha Profesa Honest Prosper Ngowi, Padre Dk. Charles Kitima, Dk. Winnie Nguni, Ndg. Ntui Ponsian Prot, Bi. Chrispina Kiemi, Dk. Stefanie Brinkel na Ndg. Erasto Ndeuka.

***Profesa Honest Prosper Ngowi*** ni Profesa wa Uchumi, Mtafiti na Mshauri wa Uchumi na Biashara katika Chuo Kikuu Mzumbe. Ni Mkuu wa Idara ya Mafunzo ya Muda Mfupi, Utafiti na Ushauri. Ni mwandishi wa hali ya juu ambaye ametafiti, ameshauri, amefundisha na kuchapisha kwa ujumla (zaidi ya machapisho 70 ya kitaaluma, zaidi ya ripoti 80 za utafiti na ushauri, pia mada zaidi ya 500 zinazohusu masuala ya uchumi na biashara zilizochapishwa katika magazeti na majarida mbalimbali). Profesa Ngowi amekuwa msimamizi wa nje wa mitihani katika vyuo vikuu kadhaa vikiwemo; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda na Chuo Kikuu cha North West cha Afrika ya Kusini. Amekuwa mmojawapo wa Wakurugenzi wa Bodi kadhaa ikiwemo Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Mfuko wa Utafiti wa Uchumi na Jamii (ESRF), Mfuko wa Asasi za Kiraia (Mwenyekiti wa Bodi kwa miaka miwili hadi mwaka 2017), SWISS Aid, Restless Development, Envirocare, Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Stellenbosch kilichopo Afrika ya Kusini pamoja na SAGCOT. Profesa Ngowi ni

rafiki wa heshima katika Kituo cha Masomo ya Teknolojia Afrika na ni mwanachama wa Jopo la Wasomi Waandamizi wa Chuo Kikuu cha Lusaka Zambia. Pia ametumikia nafasi ya Mtafiti Mwandamizi kutoka nje katika Chuo Kikuu cha Bergen nchini Norway. Akiwa msomi katika jamii, anaandika mada mbalimbali hasa zile zinazohusu uchumi na biashara katika kurasa za magazeti mabalimbali kama vile Mwananchi ('Tujadili Uchumi' kila Alhamisi), "The Citizen", (*'Economics Made Simple'* kila Jumamosi kwa miezi 6 sasa bila kusimama) pia ni mtoa mada katika vituo kadhaa vya redio na runinga (akiwa na kipindi chake katika runinga ya ITV kiitwacho Uchumi na Biashara kila siku ya Ijumaa kuanzia saa 1.00 jioni, akijadili masuala mbalimbali yahusuyo hali ya sasa katika uchumi na biashara. Aidha, ameanzisha runinga katika mtandao iitwayo "Ngowi TV" (www.ngowitv.co.tz) inayoangazia masuala ya Uchumi, Biashara na Maendeleo. Profesa Ngowi ni mzungumzaji wa lugha zaidi ya mbili kwani anazungumza Kiingereza, Kinorwey na Kiswahili kwa ufasaha, pia anaweza kutumia Kidanishi na Kiswedishi kwa kiasi katika mazingira maalumu ya kazi.

***Padre Dk. Charles Kitima*** ni Makamu Mkuu wa Chuo mstaafu katika Chuo cha SAUT, ambapo hivi sasa ni Mhadhiri Mwandamizi katika chuo hicho. Amehusika kufanya tathmini ya vyuo vikuu vya umma katika eneo la Afrika Mashariki husasani Tanzania na Kenya tangu mwaka 2006. Ni miongoni mwa makamishina waanzilishi wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) akiwa ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uidhinishaji ya TCU (2007 hadi 2010). Pia ni Mshauri Mwandamizi katika elimu ya juu akishughulikia uhakiki wa ubora na muundo wa vigezo. Amewahi kuwa miongoni mwa timu ya wataalamu watatu katika baraza la vyuo vikuu vya Afrika Mashariki (IUCEA) ambayo ilitengeneza Muundo wa Vigezo kwa ukanda wa Afrika. Ana uzoefu mkubwa katika miundo ya ubora kwa nchi za Afrika Mashariki. Alihusika kuandaa Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Ujuzi; mradi huo unafadhililwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia. Ana uzoefu kimataifa katika uhakiki wa miundo ya ubora wa taaluma.

***Dk. Winnie Nguni*** ana Shahada ya awali ya Masoko kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Shahada ya uzamili katika Uratibu wa Ugavi na Usafirishaji wa Watu na Vitu (Lojistiki) kutoka Chuo Kikuu cha Molde (Norway). Ni mkufunzi anayejituma, mshauri na mtafiti mwenye rekodi nzuri inayothibitishwa na machapisho yake. Pamoja na kuwa mbobezi katika taaluma ya Lojistiki anao ujuzi mkubwa wa kilimo biashara, usimamizi wa mnyororo wa thamani na usambazaji. Dk. Winnie Nguni ana Shahada ya Uzamifu katika usimamizi wa mnyororo wa thamani ya kilimo-utalii kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Copenhagen (Denmark). Ana uzoefu wa kutosha katika kuandaa na kuwezesha programu mbalimbali zinazohusiana na ujasiriamali, upangaji wa biashara na ushindani, usimamizi wa mnyoyoro wa thamani pamoja na mtandao. Hata hivyo Dk. Winnie Ngumi amefanya kazi na taasisi mbalimbali kama vile DANIDA, SIDA na Shirika la Kazi Duniani (ILO) katika kutafiti na kuchapisha masuala yanayohusiana na biashara ndogo na za kati pamoja na masuala ya jinsia katika sekta ya utalii na kilimo. Ametoa ushauri katika uangalizi wa miradi na uthamini, utafiti wa masoko, upangaji wa biashara pamoja na uchambuzi wa mnyororo wa thamani na usambazaji. Hivi sasa ni mwezeshaji wa mafunzo mbalimbali yanayohusiana na masoko na Lojistiki katika Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDBS).

***Ntui Ponsian Prot*** ni Mhadhiri Msaidizi katika chuo cha SAUT. Ni mwezeshaji wa mafunzo ya biashara yanayojumuisha: Uhasibu wa Fedha, Utoaji Taarifa ya Fedha, Usimamizi wa Fedha, Usimamizi wa Fedha Kimataifa, Uhasibu kwa Wanasheria pamoja na Mbinu za Utafiti. Amekuwa Mkuu wa Idara ya Uhasibu na Fedha kwa miaka mitatu wakati huo huo akifundisha na kufanya tafiti. Anapenda kufanya tafiti katika Uhasibu wa Fedha, Biashara na Wajibu kwa Jamii, Usimamizi wa Fedha, Sera za Uhasibu, Uhasibu wa Mazingira, Fedha za Kimataifa pamoja na uongozi wa biashara ambapo ameandika machapisho mengi yanayohusu maeneo hayo ya utafiti. Aidha amehusika katika uandishi wa mapendekezo ya miradi, mipango mkakati na mipango ya biashara kwa taasisi za dini na nyinginezo ambayo imetekelezwa kwa mafaniko

makubwa. Hivi sasa Ntui Ponsian Prot ni mwanafunzi wa shahada ya uzamifu (PhD) katika Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDBS) akisomea Uongozi wa Biashara huku akijikita katika eneo la Uhasibu.

***Chrispina Kiemi*** ni Mhadhiri Msaidizi katika Chuo cha SAUT. Ni msomi mwenye Shahada ya Uzamifu katika Fedha na Mhasibu wa Umma aliyethibitishwa (CPA (T)). Ni mzoefu wa kufundisha masomo yanayohusiana na biashara, kama vile Usimamizi wa Fedha, Fedha Kimataifa, Usimamizi wa Miradi, Kodi, Ukaguzi, Uhasibu wa Fedha na Utafiti wa Biashara. Amewezesha na kuendesha warsha na makongamano mbalimbali yakiwemo Uongozi Kimkakati na Mipango ya Biashara pamoja na Ujasiriamali wenye Matokeo na Urahisi wa kupata Pesa. Aidha ameendesha warsha na kongamano kuhusu “Hali ya Uchumi nchini Tanzania - Fursa na Changamoto za muundo wa Uchumi wa Soko Jamii kwa Tanzania”. Pia Chrispina ametoa machapisho kadhaa pamoja na kufanya shughuli za ushauri kwenye miradi ya kijamii.

***Dk. Stefanie Brinkel*** ana Shahada ya Uzamifu katika Uongozi wa Biashara kutoka Chuo cha Martin-Luther-University Halle-Wittenberg (Ujerumani). Amefanya kazi kama Ofisa wa Programu katika ofisi za Konrad-Adenauer-Stiftung e. V. (Dar es Salaam - Tanzania) tangu mwaka 2015.

***Erasto Ndeuka*** ni Afisa Miradi na Mhasibu Mkuu wa shirika la Konrad-Adenauer-Stiftung e. V. (KAS), ofisi ya Tanzania. Amehusika katika kuwaleta pamoja wataalamu walioandaa chapisho hili, kutoa mawazo juu ya dhana ya Uchumi wa Soko Jamii na kusimamia tafsri ya chapisho hili kutoka lugha ya Kiingereza.

***Konrad-Adenauer-Stiftung e. V. (KAS)*** ni Shirika la Hiari la Ujerumani lililopewa jina la Kansela wa kwanza wa Ujerumani, Konrad Adenauer baada ya Vita ya Pili ya Dunia (1949-1963). Majukumu makuu ya shirika hili ni kukuza demokrasia, maendeleo endelevu, utawala bora, uhusiano wa kimataifa, masikilizano ya kikanda na uchumi jamii. Ofisi za KAS zinasimamia zaidi ya miradi 200 katika nchi zaidi ya 120 ulimwenguni kote. Shirika la KAS limekuwa

likiendesha shughuli zake nchini Tanzania tangu mwaka 1964 baada ya kualikwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ili kutoa msaada wa mafunzo ya uongozi katika Chuo cha Kivukoni, Dar es Salaam.

# 1. Utangulizi

Katika nchi zilizoendelea kadhalika na zile zinazoendelea, juhudi na mbinu mbalimbali zimechukuliwa katika kutafuta maendeleo ya kiuchumi. Baadhi ya nchi zilifanikiwa mapema, nyingine zilihitaji muda zaidi lakini zilifikia malengo yao. Nchi nyingi bado zinashughulikia mipango yao ya maendeleo ya uchumi ingawa matokeo yake yanaweza kuwa si ya kuridhisha sana. Nchi nyingine zilibadili mbinu na mifumo yake lakini bado maendeleo yaliyopatikana ni ya chini na hali ya umasikini bado imebaki kuwa juu. Tanzania haina tofauti sana na nchi za aina hii. Tanzania imeshuhudia kiwango kizuri cha ukuaji wa uchumi, lakini bado maendeleo yake ya kiuchumi (kwa mtu mmoja mmoja) ni ya kukatisha tamaa sana. Wananchi wake wengi bado wanaishi kwenye umasikini uliokithiri. Sababu za mafanikio na kushindwa kwake zinaweza kuwa ni matokeo ya mambo mengi lakini sababu kubwa zinaweza kuwa ni mbinu, falsafa, utaalamu na tekinolojia zilizotumika na zinazoendelea kutumika mpaka leo hii.

Haya yote yanaweza kuelezwa kwa aina ya mfumo wa kiuchumi uliotumika au unaoendelea kutumika. Nchi zilizofanikiwa zinaweza kutumika kama mifano ya kujifunzia kwa nchi nyingine, ingawa mazingira na hali zao zinaweza kutofautiana.

Mfumo wa uchumi unaotambuliwa kwa kuleta mafanikio na uimara wa maendeleo katika nchi kadhaa ikiwemo Ujerumani na nchi za kiNordiki unajulikana kama **Uchumi wa Soko Jamii**. Chapisho hili kwa sasa linajaribu kuutambulisha na kuufanya mfumo huu wa uchumi utumike nchini Tanzania kwa kuzingatia hali ilivyo ili kutengeneza njia inayostahili kufuatwa kwa ajili ya kupata maendeleo ya uchumi endelevu na jumuishi kwa nchi yetu. Maelezo kamili ya namna uchumi wa soko jamii ulivyo yametolewa katika sura ya pili (2). Uchambuzi wa hali ya kiuchumi na kijamii ilivyo nchini Tanzania kwa sasa umeelezwa katika

sura ya tatu (3). Msingi wa maendeleo ya uchumi wa soko jamii umeelezwa kwenye sura ya nne (4) na mwisho kabisa sura ya tano (5) imetoa hitimisho na wito kwa watunga sera na wananchi kwa ujumla kuukubali mfumo huu na kuufanya utumike ili uweze kuleta mapinduzi ya kiuchumi nchini Tanzania.

# 2. Historia ya Kinadharia ya Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii

Kitaaluma usimamizi wa uchumi tangu zamani na mpaka sasa unahitaji na kutegemea mpangilio wa mambo kikanuni na taratibu madhubuti (Leipold, 2008, uk 144). Inaaminika kuwa bila kanuni na taratibu hizo kufuatwa inakuwa ni vigumu sana kwa Tanzania kupata ukuaji wa uchumi unaojumuisha watu wote. Vile vile inaaminika kuwa uchumi wa soko jamii ni muhimu kwa ufanisi wa uchumi ulio imara. Hata hivyo uchumi wa soko huria una hatari ya kusababisha ongezeko la umasikini kwani si jumuishi kwa watu wote, na hivyo husababisha watu wachache au makampuni machache kuwanyonya wengine kupitia namna wanavyoendesha biashara zao. Kwahiyo, Serikali inao wajibu wa kuchukua hatua ya kuhakikisha hali hiyo haitokei, lakini udhibiti huo usiwe tishio kwa ushindani wa kibiashara na kuzuia ubunifu na juhudi binafsi.

## 2.1. Kanuni na Taratibu za Kiuchumi

Wakati tatizo la msingi kabisa katika usimamizi wa uchumi mara zote limekuwa ni uhaba wa bidhaa na huduma mbinu mbalimbali zimebuniwa ili kukabiliana na hali hiyo (Leipold, 2008, uk 144). Ipo mifumo mikuu miwili inayotofautiana ambayo ni uchumi wa soko huria na uchumi unaopangwa na serikali kuu. Upo mfumo wa tatu uliojitokeza katika hiyo unaoitwa mfumo wa uchumi mseto ambao umechukua baadhi ya tabia za uchumi wa soko huria (ubepari) na baadhi ya tabia za uchumi unaomilikiwa na kusimamiwa na serikali (ujamaa).

### *2.1.1. Mfumo wa Uchumi wa Kijamaa*

Katika mfumo huu wa uchumi mambo yote yanapangwa na serikali kuu na kuratibiwa kupitia mpango wa kitaifa wa uchumi na hakuna uhuru wa kufanya shughuli za kiuchumi kwa watu binafsi au vikundi (Leipold, 2008, uk 144). Katika mfumo huu uzalishaji na umiliki wa mali ni lazima uwe mikononi mwa vikundi halali au chini ya umma (Schuller/Welsch, 2008, uk 429). Katika mfumo wa

namna hii, sekta binafsi na ubunifu vinakuwa dhaifu na ufanisi huwa wa kiwango cha chini.

### *2.1.2. Uchumi wa Soko Huria/Ubepari*

Katika mfumo huu, mambo huwa tofauti na mfumo wa kiserikali ambapo shughuli nyingi za kiuchumi huwa mikononi mwa watu binafsi au vikundi binafsi na huratibiwa tu na bei za bidhaa na huduma sokoni (Leipold, 2008, uk 144). Katika mfumo huu, ugatuaji wa madaraka wa kupanga na kuratibu huachwa mikononi mwa soko ambapo upatikanaji ama upungufu wa bidhaa na huduma unatokana na bei za bidhaa au huduma. Hii ina maana kwamba, upungufu wa bidhaa au huduma husababisha ongezeko la bei na upatikanaji wa bidhaa na huduma kwa wingi husababisha bei kushuka.

**Hapa tunajiuliza** 'Je kuna uhusiano gani wa kisera na kitaasisi kati ya madaraka ya serikali na matendo ya watu binafsi na uhuru wao wa kiuchumi na ustawi wa jamii?' Hapo ndipo linajitokeza wazo la uchumi wa soko jamii (Leipold, 2008, uk 145).

### *2.1.3. Uchumi wa Soko Jamii*

Mfumo huu unaunganisha uchumi wa soko huria pamoja na jukumu la serikali katika kudhibiti hali ili haki itendeke kwa wote na kuleta ushindani unaofaa, kudhibiti hali ya ukuaji wa uchumi, kupunguza mfumuko wa bei, kupunguza upungufu wa ajira, kuboresha hali ya mazingira ya kazi na kuleta ustawi wa jamii kwa ujumla. Lengo la mfumo huu ni kutengeneza uwiano kati ya uchumi wa soko huria na usimamizi wa serikali kwa kiasi kinachofaa ili kuleta maendeleo (Leipold, 2008, uk 145). Tofauti na mifumo mingine ya uchumi, mfumo huu wa uchumi wa soko jamii ni mfumo jumuishi kwa watu wote na unaruhusu watu wote kushiriki na kuchangia katika ujenzi wa uchumi wa nchi yao.

## 2.2. Sifa za Uchumi wa Soko Jamii

Sehemu hii ya chapisho inaeleza kwa undani nadharia ya mfumo huu ikijumuisha wadau wote pamoja na wajibu wao katika kuhakikisha utekelezaji wa mfumo huu pamoja na kanuni zake.

### *2.2.1. Utangulizi*

Kwa mujibu wa Chama cha Watu wa Ulaya (European Peoples Party), 'Uchumi wa Soko Jamii' ni matamanio ya kifalsafa yaliyojikita katika jamii ya watu yanayozingatia utu wa mtu, maendeleo yake, juhudi zake, kumtia moyo, kumpa uhuru na kutoa wajibu kwa kila mtu. Waasisi wa mfumo huu wa uchumi (Alfred Muller Armack, Walter Eucken, Leonhard Miksch, Franz Bohm, Wilhelm Ropke, Alexander Rustow, Konrad Adenauer na Ludwig Erhard) walikuwa na maono ya utekelezaji kama ifuatavyo:

a) Mahali ambapo ukuaji wa uchumi ulikuwa hauhitilafiani tena na maendeleo ya kijamii isipokuwa sasa vinafanya kazi kwa kushirikiana na kujengana pamoja na kuhakikisha kuwa kunakuwa na ustawi endelevu wa jamii na kuleta matokeo chanya katika jamii kwa ujumla na,

b) Kwamba dhamira kuu ilikuwa kuimarisha uhuru wa watu binafsi, mshikamano na uwajibikaji wa mwananchi mmoja mmoja pamoja na serikali (EPP 2009, uk. 2-3).

Taasisi ya Konrad-Adenaur ya Ujerumani inaeleza kuwa mfumo huu wa uchumi unamweka mtu na utu wake katikati ya mambo yote. Shughuli zote za kiuchumi zinafanyika kwa kuzingatia utu, uwezo, mahitaji na hamasa za kibinadamu. Mfumo huu ni tofauti na ile mifumo ya kijamaa ambayo hujali zaidi mashirikiano ya uzalishaji ambayo huingiliwa mno na serikali badala ya kujali zaidi utawala wa kiuchumi ambao hujali, huthamini na kuheshimu juhudi binafsi na ubunifu (KAS 2008 uk. 9).

Kwa mujibu wa Benecke (2008, uk.11-15), kuna mahitaji makuu manne ili kuwa na mfumo wa uchumi wa soko jamii wenye ufanisi. Mambo hayo yameelezwa kwa ufupi kama ifuatavyo:-

a) Muundo wa misingi madhubuti: Ni lazima pawepo na sera, sheria na kanuni imara za kutosha, mfumo wa mahakama ulio huru, uwezekano wa kushiriki katika kufanya maamuzi kwa haki na uhuru wa kujieleza kwa jamii.

   Bila ya kuwa na kanuni za wazi zinazokubalika na jamii ambazo ndizo zinazotumika katika kufanya maamuzi na jamii yenye

kujituma na yenye moyo wa kushiriki katika ujenzi wa taifa, isitegemewe kuwa kutakuwa na uwekezaji wa maana nchini. Hata hivyo ni muhimu kuwa na uwezekano wa kufanyika kwa mabadiliko pindi inapotokea uhitaji kulingana na wadau au hali ya mabadiliko yoyote muhimu.

b) Utayari wa serikali kuunga mkono: Ni lazima serikali ioneshe kuunga mkono mfumo huu wa kiuchumi. Serikali yenyewe lazima ihakikishe kuwa huduma zinazowezesha mfumo huu wa uchumi kufanikiwa, kama vile elimu, afya, miundombinu ya mawasiliano na uchukuzi zinapatikana. Hali kadhalika serikali lazima itambue na kukubali mipaka yake katika kuratibu na kudhibiti shughuli mbalimbali katika mfumo huu na kuachia madaraka kwa vyombo vinavyojitegemea. Hii inahusisha kwa mfano majukumu ya benki kuu.

c) Vyombo huru vya habari vyenye kuwajibika: Katika kuwataarifu wadau juu ya hali ya uchumi wa nchi ilivyo, vyombo vya habari vina jukumu la kutoa taarifa zenye uhakika kama vile maelezo ya bidhaa, kanuni na taratibu, maslahi yaliyopo, fursa na mapungufu yaliyopo kwenye mfumo wa nchi. Wadau wanaweza kuwa ni wazalishaji wa bidhaa, wanunuzi, washauri, wakusanya kodi, waingizaji wa bidhaa, watoa fedha za mitaji na wananchi wote kwa ujumla.

d) Uhuru na utayari wa washiriki katika kuhakikisha malengo ya mfumo huu yanafikiwa: Kimsingi mfumo huu unaruhusu wadau wote kuwa huru katika kufanya maamuzi yao. Wakati huohuo wote hutegemeana kwani hakuna anayeweza kufikia malengo yake peke yake bila kuathiri maslahi ya mwingine. Kwahiyo ni muhimu kwamba washiriki au wadau wote wakatambuana, si kama maadui, ila wawe tayari kushirikiana kwa maslahi ya wote. Washiriki hawa wanaweza kuwa serikali, wajasiriamali, umoja wa wafanyabiashara, taasisi za umma zinazojitegemea, asasi za kiraia, taasisi za biashara na viwanda, mawakala wa mazingira, taasisi za fedha, mifuko ya hifadhi ya jamii na taasisi za elimu ya juu.

### *2.2.2. Uchumi wa Soko Jamii – Wadau na Majukumu yao*

Ili mfumo wa uchumi wa soko jamii uweze kufanikiwa wadau wake lazima watimize majukumu maalumu. Yafuatayo ni maelezo ya wadau hawa pamoja na majukumu yao:

a) **Serikali Kuu na Serikali za Mitaa:** Kuna haja ya kuainisha shughuli mbalimbali za umma katika ngazi tofauti za kiutawala kama vile mapato na matumizi (Diller 2008, uk.232). Mgawanyo wa aina za kazi vile vile ni muhimu ukaeleweka na kwa kawaida huwekwa kwenye njia kuu mbili,

- Usimamizi na utatuzi kwenye ngazi ya juu ya kitaifa – kwa mfano ulinzi na usalama wa taifa na ustawi wa jamii hushughulikiwa na serikali kuu na,
- Ugatuaji wa madaraka kwa ngazi ya chini kama vile halmashauri za miji na wilaya ambako huduma kama vile maji safi na salama na kazi za kujitolea hushughulikiwa.

Kulingana na maelezo ya mtaalamu aiitwaye Diller, mgawanyo wa majukumu lazima uendane na mgawanyo wa fedha za matumizi unaokidhi mahitaji (Diller 2008, uk. 232-233).

b) **Mashirika ya Umma** (Dickertmann/Piel 2008, uk. 329-331): Pamoja na kuonekana kuwa ni majukumu ya serikali, lakini kazi nyingi zenye maslahi ya umma hufanywa na taasisi zinazojitegemea kibajeti. Mashirika haya hufanya kazi bega kwa bega na serikali za mitaa na ndiyo sababu ya kuitwa mashirika ya umma- ni taasisi za kiserikali zinazoshughulikia kazi za kijamii. Hivyo yanaweza kufikiriwa kuwa ni mamlaka ya tatu kutoka serikali kuu na zile za mitaa zinazoshughulikia masuala ya kitaifa na ya kijamii na vile vile kuratibu mfumo wa masoko kwa maslahi ya uchumi wa sekta binafsi. Mashirika haya huwa yanajitegemea kifedha na mifumo ya kiutawala na wa kiutendaji. Fedha za matumizi ya huduma zitolewazo na mashirika haya hutokana na uhakika wa mapato yatokanayo na njia mbalimbali stahiki kama vile michango ya lazima ya wanachama wao, nyongeza ya kodi za makusanyo n.k. Mifano halisi ya mashirika haya ni:-

- Skimu za ajira, afya, uuguzi, mifuko ya hifadhi ya jamii na bima mbalimbali.
- Wawakilishi wa wafanyabiashara, viwanda na kilimo, lakini pia kuna nyongeza ya taasisi ambazo zinaweza kujumuishwa kama mashirika, kama vile:-
  - Taasisi za kimataifa kama vile benki za maendeleo
  - Taasisi za kidini
  - Taasisi shirikishi kama vile mifuko ya kiserikali (utafiti na utamaduni)
  - Makundi ya mashirika ya kutoa misaada, makundi yasiyo ya kibiashara, mashirika ya kimuungano wa kiserikali yanayotoa huduma kama vile elimu na afya na makundi yanayotoa huduma za pamoja (mfano vyama vya siasa na hisani mbalimbali, ushirika wa vyama vya wafanyakazi na vyama vya waajiri).

c) **Soko:** Hapa ndipo mahali pa makutano ya upatikanaji wa bidhaa na mahitaji utokeapo (Seitel 2008a, uk.312). Ubadilishanaji wa bidhaa na fedha kwa maelewano kati ya wanunuzi na wauzaji hutokea hapa. Wahusika hapa ni watu wa aina zote, binafsi na umma pia, ikiwajumuisha wafanyakazi na mameneja wao, na jamii yote kwa ujumla. Kwa maelezo ya Mayer, (2013), sekta binafsi ina nafasi ya kipekee sana katika maendeleo ya uchumi wa nchi. Maendeleo hayo ya uchumi yanajumuisha ukuaji wa uchumi, mikakati ya kupunguza umasikini na kuleta mabadiliko chanya ya kiuchumi nchini.

d) **Bodi za usimamizi:** Hivi ni vyombo vyenye jukumu la kudhibiti, kusahihisha na kutoa maamuzi ya mambo kwenye maeneo mbalimbali. Maeneo yenye kuhitaji usimamizi wa aina hii ni kama vile madawa, mabenki, nishati na usafiri wa ndege (Fritz-Abmus 2008, uk.444). Katika mfumo wa uchumi wa soko jamii, kazi maalumu ya benki kuu ni kuwa chombo chenye mamlaka ya juu kabisa katika shughuli za kibenki na ni jukumu lake kuhakikisha kuwa kiasi cha mzunguko wa fedha nchini kiko sahihi kulingana na hali ya uchumi ilivyo (König 2008, uk.172).

Hali kadhalika shirikisho la wazalishaji na wasambazaji wa bidhaa wana mamlaka huru inayosimamia ushindani wa kibiashara kama vile kuunganisha matawi mbalimbali, kuhodhi au kushughulikia matumizi mabaya ya soko (Stockmann 2008, uk. 227) na vile vile pawepo na wakala wa ajira ambaye kazi yake ni kuwa na mamlaka kamili ya kutoa ushauri wa moja kwa moja serikalini kuhusiana na suala la ajira (Kleinhenz 2008, uk. 229). Hata hivyo kuna vyombo vingine vya kitaaluma vinavyojitegemea katika maamuzi ambavyo pia husaidia katika mfumo wa uchumi. Wanataalamu hawa huunda vikundi kwenye mfumo wa chemba kulingana na taaluma zao. Kwa mfano **chemba** ya biashara na viwanda inahusika na maamuzi ya kibiashara, wakati **chemba** za matabibu zinahusika na maamuzi ya matibabu tu na bodi ya wataalamu wa ujenzi nao wanashughulika na mambo yahusuyo ujenzi na shughuli za kijamii zinaongozwa na mifumo ya hifadhi za jamii (Hinz 2008, uk. 103).

Kwa nyongeza kuna washirika wa kijamii ambao wanaweza kuwa kwenye ngazi mbalimbali kulingana na kazi zao. Hizi ni kama vile **mabaraza** ya kazi na usimamizi katika ngazi ya kibiashara, vyama vya wafanyakazi na vyama vya waajiri, wakala wa ajira na usimamizi wake na shughuli za kijamii kwenye ngazi ya taifa na shirika la kazi duniani la umoja wa mataifa kwenye ngazi ya kimataifa (Rosner 2008, uk. 418-419).

Ili kurahisisha kupima ufanisi wa uchumi, kamati maalumu huajiriwa kwa mkataba. Kamati hii huwa huru (bila ya kuingiliwa na serikali kwa namna yoyote ile) katika utendaji wake. Kwa mfano nchini Ujerumani, kamati hii huundwa na watu watano wajulikanao kama "watu watano wenye hekima na busara" (Wolburg 2008, uk. 128-129).

### *2.2.3. Kanuni, nguzo na malengo ya jumla ya uchumi wa soko jamii.*

Mfumo huu wa soko unaongozwa na kanuni kadhaa. Kanuni hizi ni pamoja na uwezo wa kujitegemea/kujiendesha na mshikamano.

- **Uwezo wa kujitegemea/kujiendesha:** Huu ni msingi unaoelezea uwezo wa kila mwananchi katika kutekeleza na kufanikisha majukumu katika jamii. Inaaminika kuwa kila mtu akiwa peke yake au katika vikundi vidogo vidogo kama familia n.k anakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya mambo yake. Hata hivyo endapo jambo limeshindwa kuamuliwa na ngazi ya chini basi jambo hilo litapelekwa ngazi ya juu inayofuata kwa ajili ya uamuzi kwa mfano kutoka ngazi ya familia hadi ngazi ya serikali ya mtaa, kata, wilaya n.k. (Haase/Schneider/Weigelt 2008, uk. 492). Ni muhimu kutoa nafasi kwa ngazi zote kufanya kazi badala ya kukimbilia tu kwenye ngazi ya serikali kuu. (Dickertmann/Piel 2008, uk. 412).

  Ni muhimu kuelewa kwamba, dhana hii ya uwezo wa kujitegemea na kujiendesha inahitaji serikali kuendelea kutoa huduma za jamii hata kama mtu anajitosheleza kwa mahitaji.

- **Mshikamano:** Hii inamaanisha kuwa na ushirika wa pamoja, kusaidiana katika mambo mbalimbali kwenye jamii (Haase/Schneider/Weigelt 2008, uk 491). Hitaji kuu hapa ni utu wa mtu na sio tofauti zao zingine kama vile dini, hali ya kiuchumi, rangi, kabila n.k (Baumgartner 2012, uk. 64). Mshikamano umejengeka katika wajibu wa kutoa mchango wa kila mmoja katika jukumu la pamoja (Baumgartner 2012, uk. 60). Kwa hiyo mfumo huu wa soko unahitaji kujitoa kwa mtu mmoja mmoja kwa ajili ya mshikamano wa kijamii ili pawepo na ushirikiano pale ambapo vyombo vya serikali havitoi msaada wa kutosha.

Kwa kuongezea kanuni zifuatazo pia ni miongoni mwa misingi ya mfumo huu wa uchumi jamii (KAS 2009, uk. 1-8; EPP 2009, UK. 3-5).

- Katika mfumo huu wa soko mgawanyo wa rasilimali kama vile bidhaa na huduma, na rasilimali kama vile nguvu kazi, mtaji na ardhi vyote kimsingi vinaratibiwa na soko. Shughuli zote za kiuchumi zinaongozwa na ushindani sokoni. Mfumo wa ushindani sokoni unaotegemea bei huria unalenga kuongeza upatikanaji wa bidhaa adimu na hivyo kuongeza ufanisi na maendeleo ingawa kuna haja ya kuangalia mazingira mengine

ya nje yanayohusu uzalishaji mali. Mfumo huu wa uchumi wenye ushindani unajaribu kuzuia nguvu ya soko kuegemea upande mmoja, kwa mfano, kudhibiti watu fulani kuhodhi mwenendo wa soko na matumizi mabaya ya madaraka. Vile vile panahitajika soko huru ili kuruhusu biashara ya kimataifa kufanyika bila upendeleo wa aina yoyote. Hata hivyo msingi wa ushindani katika soko unamaanisha pia uwajibikaji ambapo ushindani unafungamanishwa na mwenendo mwema wa wahusika wote. Matarajio ya kupata faida huleta ushindani wakati wa uwajibikaji, endapo patatokea hasara ushindani unasaidia sana kupunguza tabia ya kutokujali na udanganyifu katika shughuli mbalimbali (KAS 2009, uk. 4). Kwa nyongeza ni kwamba mfumo huu wa uchumi umejengwa katika mfumo wa umiliki binafsi wa mali ambao unatoa uhuru wa matumizi kwa mmiliki wa mali hizi. Mfumo huu unamlazimu mshiriki kujenga ubunifu katika kutafuta mali kwa njia halali ambao ndiyo msingi mkuu wa mjasiriamali. Ni mfumo wa uchumi wa umiliki mali binafsi tu ndio unaohakikisha kuwa ajira inakuwa endelevu (KAS 2009, uk.2).

- Ili shughuli za kiuchumi ziweze kuwa na ufanisi na endelevu ni lazima ziwe na mfumo wa kisheria. Mfumo huo wa kisheria unaweka utaratibu wa kuwa na uchumi imara na serikali rafiki kwa raia inayozingatia kanuni za utawala bora (KAS 2009, uk.1). Kuna haja ya kuona kuwa sheria zinafuatwa na kuweka usimamizi ili wale wote wanaozivunja wanaadhibiwe. Hii pia inasaidia kuhakikisha kuwa mfumo huu unatoa manufaa kwa jamii yote kupitia ugatuaji wa madaraka. Mambo ya msingi kabisa ni kuwa na mfumo wa uchumi ulio imara wenye kutoa mazingira mazuri ya uchumi mdogo mdogo ulio imara na tulivu (kwa mfano bei zinazotabirika kwa kudhibiti mfumuko wa bei) na mpango mzima wa sera ya muda mrefu iliyo imara.

- Wakati huo huo serikali inatakiwa ihakikishe kuwa inatoa huduma za jamii zinazohitajika na umma lakini ambazo soko haliwezi kuzitoa kabisa au haliwezi kuzitoa kwa kiasi kinachohitajika. Huduma hizi ni kama vile elimu, miundombinu ya kutosheleza na huduma za afya za kueleweka na kuridhisha

(KAS 2009, uk5). Kwa nyongeza, ingawa ukuaji wa uchumi unarahisisha kupungua kwa umasikini, uchumi wa soko jamii hauwezi kuondoa tofauti za kipato na kasoro za kifursa zilizopo katika jamii nzima. Kwahiyo mfumo huu wa uchumi wa soko jamii unahitaji mifumo ya hifadhi ya jamii inayojitosheleza, njia bora za usambazaji wake, njia bora za kodi inayolenga utekelezaji bora, ili kuhakikisha kuwa kuna amani na usalama wa kutosha kuwawezesha wananchi kushiriki vya kutosha katika shughuli za kiuchumi na kuiwezesha serikali kutekeleza wajibu wake. Ili kuweza kulipia shughuli hizo za serikali panahitajika mfumo wa kutia moyo wananchi kuwa wanao uwezo na madaraka (KAS 2009, uk.6). Ugatuaji wa madaraka kutoka serikali kuu kwenda serikali za mitaa ni lazima upongezwe na kuendelezwa kwani unawapa wananchi uwezo wa kimaamuzi na kiutekelezaji.

- Mwisho kabisa ili kuleta ufanisi na uwajibikaji katika malengo ya muda mrefu suala la uchumi endelevu lina umuhimu wa kipekee kabisa katika mfumo mzima wa uchumi. Heshima kwa mazingira na utu wa mtu ni lazima viwe sehemu ya mchakato wa utoaji maamuzi ndani ya mfumo wa uchumi kama sehemu ya ufanisi wa muda mrefu na ishara ya utambuzi wa haki kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Kwa nyongeza chama cha watu wa Ulaya (EPP, 2009) kimetoa majumuisho yafuatayo kuhusiana na nguzo muhimu za uchumi jamii:-

a) Uhuru wa mtu binafsi, majukumu yake na ushirikiano na serikali na vile vile maslahi ya vikundi yanayoongozwa na jamii iliyo huru.

b) Masoko huru, ushindani wa kutosha, umiliki binafsi wa njia za uzalishaji mali, uhuru wa bei, mikataba ya hiari, madeni ya binafsi, udhibiti wa kuhodhi soko na matumizi mabaya ya madaraka, biashara huru za kimataifa na utulivu wa thamani ya fedha.

c) Mshikamano na uwezo wa kujitegemea/kujiendesha unaoheshimu utu wa mtu na kulinda amani ya jamii kutokana na sera zinazotabirika na zinazokubalika na mfumo wa soko

wenye kuleta tija na vile vile kuwa na hali ya kusaidiana iliyo endelevu.

d) Kuheshimu uzalishaji na maendeleo yanayojali vizazi vyote vya sasa na vijavyo.

Kwa ujumla mtazamo mzima wa mfumo huu wa uchumi jamii ni kuunganisha kanuni za soko huria na mfumo wa kijamii unaolenga kuhakikisha kuwa kunakuwa na ustawi kwa watu wote (Ludwig Erhard, Dickertmann/Piel 2008, uk. 407).

## 2.3. Manufaa ya Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii.

Chimbuko la mfumo wa uchumi wa soko jamii ni nchi za Ulaya. Hapo mwanzoni jina la mfumo huu lilitokana na wazo la uchumi lililozaa msingi wa sera ya uchumi nchini Ujerumani Magharibi tangu mwaka 1948 (Quaas 2008, uk. 393). Kulingana na maelezo ya mtaalamu wa uchumi Schlecht, ni kwamba; marekebisho ya kifedha na ya kiuchumi yaliyofanyika mnamo tarehe 20 Juni 1948 ndiyo yaliyozaa mfumo huu wa uchumi jamii katika nchi ya Ujerumani Magharibi. Ilikuwa ni mwanzo wa kuanzishwa kwa taasisi ya kimfumo wa kijamii na kiuchumi ambao kwa muda mfupi ilifurahiwa kuwa ni mfumo wa maajabu maeneo mengi duniani (Schlecht 2008, uk. 401).

Wakati mfumo huu wa uchumi wa soko jamii ukitekelezwa kwa mara ya kwanza nchini Ujerumani; pia wachumi katika nchi nyingine za Ulaya na wanasiasa kutoka Ufaransa na Italia, Uswisi, Uingereza, Ubeligiji, Uholanzi, Luxemburg, Austria na nchi nyinginezo walikuwa sehemu ya mtandao ulioanza kuendeleza na kuboresha wazo hili tangu mwanzo wa karne ya 20 (EPP 2009, uk. 2). Kama walivyosema waasisi wa mfumo huu wa uchumi, hali mbaya ya kiuchumi huko Ulaya kati ya miaka ya 1920 na 1930 ambayo ilileta balaa la vita ya pili ya dunia kwa kiasi kikubwa ilisababishwa na kuzorota na mwisho kuanguka kabisa kwa soko huru na lenye ushindani. Wazo la uchumi jamii lilibuniwa kama njia huru ya uchumi badala ya uchumi uliopangwa na serikali na ushirikishwaji wa jamii badala ya soko huria tu, ilichangia kwa kiasi kikubwa utulivu wa kisiasa na maelewano ya kijamii katika nchi ya

Ujerumani. Mfumo huu pia ulichangia kuleta maendeleo ya hali ya juu, ustawi na mshikamano kwa kipindi cha miaka 60 iliyopita huko Ulaya Magharibi na katika nchi nyingine nyingi Duniani (EPP 2009, uk. 2).

Mfumo huu wa uchumi wa soko jamii umeonesha kwamba unao uwezo wa kusaidia shughuli za maendeleo ambazo zinahitajika na nchi nyingi, Tanzania ikiwemo.

Hata hivyo ni muhimu kutambua kuwa kuna tofauti nyingi kati ya hali ya nchi moja na nyingine na hivyo basi ni vyema mfumo huu ukachukuliwa na kuundwa na kuboreshwa kulingana na mazingira na hali ya nchi husika.

Tanzania pia inaweza kujifunza kutoka nchi nyingine nje ya Ujerumani, ambazo zimechukua mifumo ya uchumi yenye sifa nyingi zinazolingana na mfumo wa uchumi wa soko jamii. Kwa mfano nchi za Nordiki (Denmark, Finland, Sweden, Norway na Iceland) ambazo zote zipo kati ya kundi la nchi 23 bora kabisa kuhusiana na maendeleo ya mtu, hii ni kulingana na taarifa ya maendeleo ya binadamu ya mwaka 2016. Nchi hizi zimeendelea sana kijamii na kiuchumi kwa kutumia maboresho yanayotokana na sifa zilizopo kwenye mfumo huu wa uchumi wa soko jamii. Nchi za ki-Nordiki zenyewe zimebuni mfumo wao uitwao mfumo wa kinordiki, ambao unafanana sana na mfumo huu wa uchumi jamii (Anderson 2007; Pontusson 2011). Mfumo huu wa kinordiki unasisitiza zaidi juu ya ushiriki wa nguvu kazi katika jamii, upatikanaji wa huduma za ustawi wa jamii na uendelezaji wa binadamu. Nchi hizi hutumia mapato yake makubwa kwenye kusimamia na kugharamia kuanzia malezi ya utotoni, elimu, utafiti na maendeleo. Nchi hizi pia hushirikiana kwa karibu kudhibiti na kugawana hasara ya mambo yasiyotabirika pamoja na taasisi zenye nguvu kubwa kwenye mambo ya ajira kwa mfano vyama vya wafanyakazi na vyama vya waajiri (Andersson 2007, uk.11-14). Utafiti unaonesha kuwa nchi hizi za kinordiki zimefanikiwa katika ufanisi na ukuaji wa uchumi pamoja na amani inayotokana na soko la ajira, mgawanyo wenye uwiano mzuri wa mapato na mshikamano wa kijamii (Andersson 2007, uk.11).

Kwa kuzingatia kuwa Tanzania ina mtazamo wa kisoko, inaweza pia kujifunza katika mifumo ya baadhi ya nchi za Kiasia kama vile Singapore. Hapo mwaka 1960, Singapore ilikuwa na tatizo kubwa sana la upungufu wa ajira,ukosefu wa mifumo ya maji taka, hali mbaya ya huduma ya afya na maji safi na salama,umasikini uliokithiri na hali ya uhalifu mkubwa. Serikali ya Singapore iliomba msaada wa wataalamu kutoka Umoja wa Mataifa kwenda kutoa ushauri na ilianzisha taasisi kurahisisha uwekezaji wa moja kwa moja kwa wawekezaji wa nchi za kigeni ndani ya kisiwa hicho (Taymaz 2003). Kwa ujumla nchi ilipitisha na kuukubali mfumo wa kibiashara na uwekezaji kutoka nje na kukubali mfumo mzima wa sera ya kuuza bidhaa zake nje ya nchi. Na sasa nchi hiyo inavuma kwa uchumi shirikishi na maendeleo ya kila mtu.

# 3. Uchambuzi wa Hali ilivyo Nchini Tanzania

Kabla ya kujikita kwenye maamuzi iwapo na kwa namna gani mfumo wa uchumi wa soko jamii unaweza kutumika kwa manufaa na kusaidia kujibu haja za jamii ya kitanzania, hali ya kiuchumi, kijamii na kisiasa iliyopo nchini lazima ichambuliwe na kuelezewa kwa ufasaha.

Yafuatayo ni mambo muhimu kwa maendeleo endelevu nchini na utekelezaji wa mfumo huu wa uchumi jamii.

a) Maendeleo ya uchumi wa kitaifa na ule wa binafsi au vikundi (aya ya 3.2),
b) Maendeleo ya kijamii ( aya ya 3.3),
c) Maendeleo ya kisiasa (aya ya 3.4),
d) Maendeleo ya sayansi na teknolojia (aya ya 3.5), pamoja na
e) Maendeleo ya mazingira (aya 3.6).

Mgawanyiko wa aina hii unaungwa mkono na ugunduzi uliofanywa na shirika la Umoja wa Mataifa, Idara ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii (UNDESA) na Dalal –Clayton na Bass (2000) wanaeleza kimawazo na kimtazamo kwamba maendeleo yamegawanyika katika sehemu zifuatazo, nazo ni:- kiuchumi, kisiasa, kijamii na kimazingira. Hali ya kitekinolojia ilivyo pia ndiyo inayoamua mwelekeo wa kimaendeleo (Sirimanne 2017).

Kabla ya kuingia kwa undani, ni muhimu kujua historia kidogo juu ya njia zilizofuatwa na Tanzania katika kujitafutia maendeleo ya kiuchumi tangu kupatikana kwa uhuru hadi sasa na mwishowe matokeo ya hali hiyo yanajumuishwa kwenye mfumo wa mazuri tuliyonayo, mapungufu, fursa na changamoto yaani (SWOT analysis).

## 3.1. Historia ya maendeleo ya kiuchumi Tanzania

Katika miaka ya mwanzoni baada ya uhuru, kutoka 1961-1967 nchi iliendelea na uchumi wa kibepari wa kikoloni uliotawaliwa na soko

huria na uchumi hodhi kwa wachache. Uchumi wa nchi ulikuwa mikononi mwa matajiri wachache wenye ushawishi mkubwa hasa wazungu na wa Asia (sana sana wenye asili ya kihindi). Hawa walihodhi sehemu kubwa ya uchumi wa nchi na hawakuingiliwa na serikali kwa lolote.

Hapo mwaka 1967 lilitangazwa AZIMIO LA ARUSHA lililomaliza mfumo wa uchumi wa kibepari. Hii ilichangiwa sana na imani kubwa ya baba wa taifa Mwalimu Nyerere juu ya uchumi wa nchi kuwa mikononi mwa umma. Matokeo yake ilikuwa ni kutaifishwa kwa njia zote kuu za uchumi zilizokuwa mikononi mwa watu binafsi.

Ujamaa wa kiafrika kama ulivyojulikana ukawa ndio njia mpya ya kiuchumi na kijamii kwa nchi ya Tanzania mpaka katikati ya miaka ya 1980. Kipindi chote cha utekelezaji wa Azimio la Arusha, njia zote kuu za kiuchumi zilitaifishwa na mipango yote ya kiuchumi ilipangwa na serikali kutoka makao makuu ya nchi. Biashara zote za serikali zilisimamiwa na mashirika ya umma yaliyoundwa kwa ajili hiyo.

Kufuatia mabadiliko makubwa yaliyofanyika kuanzia miaka ya katikati mwa 1980 chini ya utawala **wa Rais** Ali Hassan Mwinyi mambo yaligeuka kwa kasi kwa kuanzishwa mfumo wa soko huria, mfumo uliokumbatia sekta binafsi. Mashirika ya umma yalibinafsishwa na uchumi huria kuhamasishwa. Uwekezaji wa ndani na wa nje ulikaribishwa na kupokelewa kwa mikono miwili kutokana na mageuzi ya sera ya kiuchumi. Uchumi ukatawaliwa na nguvu ya soko **huria** inayoongozwa na upatikanaji wa bidhaa na mahitaji yanayopanga bei. Hata hivyo uwekezaji wa wazawa haukupewa nguvu kimkakati kwa kuwezeshwa ili wazawa wawe na ushirika na wawekezaji wa nje/wa kigeni ambao walikuwa na nguvu za kimtaji na kiteknolojia. Sera ya uchangiaji katika huduma za kijamii kama elimu na afya ilianzishwa kutokana na mpango wa marekebisho ya kimkakati ulioanzishwa . Kutokana na marekebisho haya ya kimkakati ya mwaka 1986, nchi ilijitahidi sana kuwapatia wananchi wake hali bora zaidi ya maisha. Kwa mfano nchi ilibuni mipango kadhaa ya utekelezaji katika kuinua

hali ya maisha ya watu wake, kama vile Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA I na MKUKUTA II) na (MKURABITA) ambao ni Mpango wa Kurasimisha Mali na Biashara, KILIMO KWANZA na mpango wa mwelekeo wa maendeleo hadi 2025. Pamoja na juhudi zote hizi uchambuzi wa uhakika unaonesha kuwa hadi sasa matokeo yaliyokusudiwa ya kuwaletea wananchi unafuu wa maisha bado hayajafikiwa kikamilifu.

Tukilinganisha mifumo mbalimbali iliyowahi kutumika kwa maendeleo ya uchumi wa Tanzania, kitakwimu inaonekana kuwa mfumo uliooneshà matokeo bora zaidi ni wa soko huria. Mwandishi Potts anasema kati ya 1961-1967, uchumi ulikua kwa asilimia 6.5, nchi ilipokuwa chini ya mfumo wa ujamaa ukuaji wa uchumi ulishuka hadi asilimia 4.4. Hata hivyo kutoka 1980-1985 ingawa nchi ilikuwa bado ya kijamaa Tanzania iliathirika sana na vita ya Kagera,ukuaji wa uchumi ulishuka zaidi na kufikia asilimia 1.1. Baada ya mageuzi ya kimkakati 1986-1995 ukuaji wa uchumi ulipanda tena na kufikia asilimia 3.2. Ingawa katika kipindi chote hiki nchi haikuwa na muundo maalumu wa kiuchumi, kuna ushahidi wa kimazingira kuwa uchumi ulikuwa wa soko huria, kwani bidhaa ziliingizwa ndani na kutolewa nje ya nchi kwa uhuru na bei za bidhaa na huduma zilipangwa na soko kulingana na upatikanaji na mahitaji.

## 3.2. Maendeleo ya uchumi mkubwa na uchumi wa kati/mdogo

### *3.2.1. Vigezo muhimu vya uchumi mkubwa*

Kwa kiasi kikubwa inaaminika kuwa muundo imara wa uchumi wa taifa lolote ni wa muhimu sana, ingawa hautoshelezi kwa ukuaji endelevu wa uchumi (Fischer 1993, uk.3). Uchumi wa taifa husemekana kuwa imara kama una sifa zifuatazo. Kwanza **mfumuko wa bei** ni mdogo na unaweza kutabirika, pili **riba za kibenki** zinaridhisha ,tatu **sera za kifedha** ni tulivu na endelevu, nne thamani ya **ubadilishaji wa fedha** ni ya kiushindani na inatabirika, tano **uwiano kati ya mauzo nje ya nchi na kuagiza bidhaa kutoka nje** ni mzuri. Pamoja na haya yote msisitizo

mkubwa upo kwenye mfumuko wa bei na ukwasi au nakisi ya bajeti ya matumizi na mapato ya nchi. Kigezo kingine cha kijumla kinachozingatiwa ni pato la taifa, yaani "GDP" (Wolla 2013, uk.1).

GDP inaelezwa vizuri kuwa ni thamani ya jumla ya bidhaa pamoja na huduma zilizotolewa na nchi katika mwaka husika (Wolla 2013, uk.1). Kigezo hiki kinahusisha matumizi yote ya mtu mmoja mmoja pamoja na uwekezaji wao, na manunuzi yote ya serikali pamoja na uuzaji baada ya kutoa thamani ya bidhaa zote zilizoagizwa kutoka nje ya nchi.

Kulingana na takwimu za serikali kwa Tanzania bara uchumi ulikua kwa asilimia 7.0 kwa miaka ya 2015 na 2016 wakati kwa Zanzibar ulikua kwa asilimia 6.6 2015 na asimilia 6.8 kwa mwaka 2016. Ukuaji huu ni kati ya ukuaji wa juu kabisa katika nchi za Afrika Mashariki. Ukuaji wa kiwango cha asilimia 7 wa uchumi ni sawa na dola za kimarekani 3.3 bilioni inayotokana na pato la taifa (GDP) la dola za kimarekani 47.4 bilioni kwa mwaka 2016. Kwa zaidi ya mwongo mmoja uliopita Tanzania imekuwa na ukuaji wa uchumi uliotulia kwa kuwa na kiwango cha juu cha ukuaji wa uchumi wa wastani wa asilimia 6.5 kila mwaka (World Bank Group 2017a). Kama ambavyo kiwango cha ukuaji wa uchumi kilivyozidi kukua kadhalika pato la taifa kwa mtu mmoja mmoja limekuwa likiongezeka tangu miaka ya 1990 na kuendelea. Kutoka kiwango cha dola za kimarekani 155.59 hapo mwaka 1993, pato la taifa kwa mtu mmoja mmoja liliongezeka na kufikia dola za kimarekani 950.81 mnamo mwaka 2014, kabla kiwango hicho hakijashuka kidogo na kufikia dola za kimarekani 872.2 kwa mwaka 2015 (World Bank Group 2018d).

Ikilinganishwa na mataifa mengine wanachama wa jumuiya ya Afrika Mashariki hapo mwaka 2015, ni Kenya pekee ndiyo ilikuwa na pato kubwa la taifa kwa mtu mmoja mmoja(dola za kimarekani 1355.0) wakati Uganda (dola za kimarekani 675.1), Rwanda (dola za kimarekani 711.8) na Burundi ilikuwa ya mwisho kwa kuwa na (dola za kimarekani 300.7) (World Bank Group 2018d***). Lakini bado mgawanyo huu wa pato la Taifa kwa mtu mmoja moja ni wa kitakwimu tu kwani wenye utajiri wote huu ni wachache na***

***makampuni binafsi machache ya nje yanayoendesha biashara zao hapa Tanzania.***

Lengo kuu mojawapo sasa la Tanzania ni kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 (Planning commission 2000). Kwa tafsiri ya benki ya dunia ya mwaka 2017, ili nchi ifikie kiwango cha uchumi wa kati ni lazima pato la jumla la taifa lifikie kiwango cha angalau dola za kimarekani 996 kwa wastani kwa kila mtu kwa mwaka. Mgawanyo wa hali hii ya mapato unamaanisha kuwa chumi za chini ni zile ambazo wastani wa pato la mwananchi ni dola 995 au chini ya hapo kwa viwango vya mwaka 2017. Chumi za kati kiwango cha chini ni zile zenye uchumi unaofikia kati ya dola 996 hadi dola 3895 kwa wastani wa pato la mtu na chumi za kati kiwango cha juu ni zile zinazofikia dola 3896 hadi dola 12055 na chumi za juu ni zile zinazofikia dola 12056 au zaidi kwa wastani wa pato la kila mwananchi (World Bank Group 2018e). Kwa sasa Tanzania pamoja na nchi zingine 33 kama vile Uganda, Rwanda, Burundi, Sudani ya Kusini, Malawi na Msumbiji zipo kwenye kundi la nchi zenye uchumi wa chini. Tanzania ilifikia kiwango cha dola 910 hapo 2017 kwa kutumia kipimo hiki (World Bank Group 2018f).

Kwa kuangalia vigezo vingine ni kwamba serikali imefanikiwa kudhibiti mfumuko wa bei unaokaribia malengo ya kati yaliyowekwa na mamlaka (Benki Kuu ya Tanzania) ya asilimia 5 kwa hali ya kuridhisha kwa miaka kadhaa sasa. Kulingana na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), "wastani wa jumla wa mfumuko wa bei kwa mwaka wa 2015 ulishuka hadi asilimia 5.6 kutoka asilimia 5.8 ya mwaka 2014" na Baraza la Takwimu la Taifa la Tanzania linaonesha kuwa wastani wa mfumuko wa bei kwa mwaka 2016 (kwa Tanzania bara) ulikuwa ni asilimia 5.175. Vile vile nchi imeweza kupunguza **riba za kibenki** na kufikia kiwango kizuri cha kuridhisha kati ya asilimia 14-16 tangu mwaka 2003 (Focus Economics 2017).

Hali kadhalika **thamani ya shilingi ya Tanzania** pia imekuwa tulivu kwa mwaka wa 2016 kufuatia kuyumba hapo mwaka 2015 (World Bank Group 2018a). Mamlaka za shirika la takwimu la taifa na jumuiya ya Afrika mashariki zinasema kuwa kwa mwaka 2015,

dola 1 ya kimarekani ilinunuliwa kwa shilingi 1985 za kitanzania, mwaka 2016 thamani ya shilingi ilifikia 2120 kwa dola 1 ya kimarekani. Mwezi agosti 2017, dola 1 ya marekani ilikuwa ni sawa na shilingi za kitanzania 2238 na hadi mwishoni mwa mwezi juni 2018 thamani ya shilingi ilikuwa ni 2278 kwa dola 1 ya marekani (BOT 2018).

Mauzo ya bidhaa nchi za nje yanategemea sana bei za soko huko nje. Kulingana na **Fiseha Haile** wa benki ya dunia, ni kwamba bei za bidhaa zilianguka sana kwenye soko la dunia kwa miaka ya hivi karibuni kutokana na ukosefu wa uhitaji wa bidhaa zenyewe na pia kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa hizo. Bei za mafuta ziliporomoka sana kutokana na wingi wa uzalishaji. Hali kadhalika bei za chuma zilishuka sana, kwa mfano mwaka 2016 thamani ya dhahabu iliuzwa kwa dola za kimarekani 1106 kwa wakia ikianguka kwa karibu asilimia 75 ya thamani ya juu kabisa hapo katikati ya 2011.

Kwa mujibu wa Haile, (2017) thamani ya mauzo ya dhahabu ya Tanzania pia ilianguka kutoka dola za kimarekani bilioni 2.3 hapo 2011/2012 na kushuka hadi dola bilioni 1.3 mwaka 2014/2015. Hivyo basi bei za bidhaa muhimu zinazouzwa nje zimeshuka kwa kasi na hivyo kupunguza nguvu za kiushawishi wa kibiashara kwa washirika wake wa nje, hali iliyoharibu zaidi mahusiano ya kibiashara. Haile anaendelea kusema kuwa kupungua kwa asilimia 1 ya mauzo ya nje husababisha upungufu wa asilimia 0.65 ya thamani ya mauzo ya nje, na kwa vile Tanzania inategemea sana bidhaa ghafi na za aina chache, na hivyo inaweza kuathirika na mabadiliko ya bei za bidhaa. Mauzo ya nje ya Tanzania bado yanategemea mauzo ya bidhaa chache za chuma na bidhaa nyingi za kilimo ambazo bado hazijaongezewa thamani na hivyo kuwa dhaifu katika kuiongezea nchi nguvu za kiuchumi (Haile 2017).

Hapo mwaka 2015 Tanzania ilikuwa na nakisi kwenye akaunti ya uwiano wa mauzo na manunuzi ya nje wa asilimia 9.8 na inakisiwa kuwa nakisi hiyo itapungua kidogo hapo 2018 na kufikia asilimia 7.5. Akaunti ya uwiano ya mauzo na manunuzi ya nje ni jumla ya uwiano wa kibiashara yaani thamani ya bidhaa na

huduma kwenda nje ya nchi na zile zinazoingizwa nchini, mapato yatokanayo na riba na gawio na uhamishaji wa fedha nje ya nchi. Kulingana na United Nations Economic Commission for Afrika (UNECA) Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo nchi pekee yenye kuwa na uwiano mzuri kwenye mauzo ya huduma kati ya nchi za jumuiya ya afrika mashariki, lakini bado uwiano huu mzuri haujaweza kufuta kabisa pengo la ongezeko kubwa la uingizaji wa bidhaa nchini (UNECA 2016, uk. Vi).

Kulingana na Ndugu Mgina (2014) Serikali ya Tanzania imejitahidi sana kutafuta na kuanzisha njia mbalimbali za kiuchumi tangu uhuru wa nchi upatikane kama vile" ubinafsishaji wa viwanda vya umma, uboreshaji unaoendelea wa miundombinu dhaifu, kuweka na kusimika mitambo ya mitandao ya simu za mkononi na kuongeza upatikanaji wa huduma ya "intaneti". Kwa muda mrefu juhudi hizi zinakubalika na wadau wa maendeleo kwa nchi, kati ya nchi na kwa mashirika ya kimataifa ambayo yamesaidia kutoa misaada ya kifedha na ya kiufundi kwa Tanzania. Kulingana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD) na (UNDP) 2017, vyanzo vikuu vya ufanisi wa ukuaji wa uchumi vilikuwa na vinatarajiwa kuendelea kuwa pamoja na "sekta ya huduma, viwanda, ujenzi, habari na mawasiliano". Pamoja na hayo wizara ya Fedha na Mipango imetambua ukuaji wa haraka kwenye maeneo ya habari na mawasiliano, fedha na bima, ujenzi,mauzo ya jumla na reja reja na utengenezaji wa bidhaa kati ya mwaka 2005 na 2015. Hata hivyo kwa sehemu kubwa sekta hizi zinamilikiwa na wawekezaji wa kigeni (Ministry of Finance and Planning 2016, uk.5-6).

Ingawa **kiwango cha umasikini** kimepungua katika miaka ya hivi karibuni, bado idadi halisi ya watu masikini haijapungua kutokana na ongezeko kubwa la watu (World Bank Group 2017a). Kulingana na takwimu zilizotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango hapo 2011/2012, asilimia 28.2 ya watu wote nchini walikuwa wakiishi chini ya mstari wa umasikini.

Inaaminika kuwa ukuaji wa uchumi Tanzania unatokana na watu wachache na kampuni za kimataifa ambazo zinatawala

sekta zinazokua haraka, wakati sekta ya wawekezaji wazawa zikishindwa kutoa ushindani wa kutosha kitaifa na kimataifa. Wengi wa wananchi wametengwa kabisa katika mafanikio haya ya kiuchumi na hawawezi kufaidika na matunda ya ukuaji huu wa uchumi, ingawa wanashiriki katika kulipa kodi.

Inaonekana kuwa nchi ina upungufu mkubwa mno wa uwekezaji katika masuala ya utafiti na maendeleo ili kuongeza tija. Mbaya zaidi ni kwamba makampuni makubwa ya kimataifa hayatoi ujuzi wowote wa kisayansi kwa makampuni ya wazawa au kama wanafanya hivyo basi ni kwa kiwango kidogo mno. Ingawa hapa na pale panaweza kuwepo taarifa za kutia moyo lakini bado kuna changamoto kwenye katika kutengeneza ajira, elimu na huduma za afya.

Pamoja na mambo mengine kuna uwezekano pia kuwa hali hii imesababishwa na ukosefu wa sera thabiti ya uchumi na ushiriki wa kila mwananchi. Vilevile kuna changamoto ya ukuaji wa uchumi wa nchi usio na mahusiano ya moja kwa moja na maendeleo ya maisha ya wananchi wazawa.

Mpango wa taifa wa miaka mitano 2016/17-2020/21 unaonesha kuwa nchi itaingia kwenye uchumi wa viwanda ukilenga kwenye "ukuaji endelevu kwenye sekta ya viwanda ili kuongeza nafasi za ajira, kubadili hali ya uchumi,usawa katika maendeleo kwa wote, kupunguza bidhaa zinazoingizwa ndani ya nchi na kuhimiza uuzaji wa bidhaa zaidi nje ya nchi" (Ministry of Finance anf Planning 2016).

Ingawa sekta ya uzalishaji mali za viwandani, unaojumuisha "uzalishaji wa nguo, bidhaa za chuma, vyakula na vinywaji, sigara, uzalishaji bidhaa za kilimo, simenti na vifaa vingine vya ujenzi" una umuhimu maalumu katika kutengeneza nafasi za ajira na uuzaji wa bidhaa nje ya nchi; ukuaji wa sekta hii ulipungua, vile vile mchango wake kwenye pato la taifa ulipungua kati ya miaka ya 2005 na 2015 kulingana na taarifa ya wizara ya fedha na mipango. Jedwali lifuatalo linaonesha hali hiyo.

**Jedwali 1: Viashiria Vinavyoonesha Ufanisi wa Sekta ya Uzalishaji Mali za Viwandani**

| Years | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ukuaji wa sekta (%) | 9.6 | 8.4 | 11.5 | 11.4 | 4.7 | 8.9 | 6.9 | 4.1 | 6.5 | 6.8 | 6.0 |
| Mchango kwenye GDP (%) | 7.3 | 7.5 | 7 | 7 | 6.9 | 6.9 | 7.6 | 7.5 | 6.4 | 5.6 | 5.2 |

*Chanzo: NBS 2016 quoted in Ministry of Finance and Planning 2016, p. 29.*

Sekta hii ya uzalishaji mali inakumbana na changamoto mbalimbali, ambazo zimeorodheshwa katika mchoro ufuatao.

**Kielelezo 1: Changamoto za Sekta ya Uzalishaji Mali Tanzania**

**Changamoto katika sekta ya uzalishaji**

- Uwakilishi duni wa viwanda binafsi vya ndani.
- Kutoaminiana kati ya wanaoshikilia mamlaka ya kisiasa na sekta binafsi.
- Mnyororo wa thamani wa ndani ulio dhaifu.
- Uduni wa njia mbadala za uzalishaji mali kutokana na uduni wa ujuzi na uwezo wa kutumia rasimali asili mbalimbali za msingi za nchi.
- Uzalishaji wa chini unaosababishwa na upatikanaji hafifu wa fedha, teknolojia za kisasa na ujuzi wa kiufundi.
- Changamoto za mazingira ya biashara
- Usambazaji wa maji na nishati usio imara na kuaminika
- Maendeleo hafifu ya miundombinu ya usafiri.
- Hakuna motisha ya kutosha kwa sekta binafsi pamoja na sekta ya umma kwa ajili ya kuzipa kipaumbele shughuli za utafiti na maendeleo.

*Chanzo: Based on Ministry of Finance and Planning 2016, p. 30-31 (own layout).*

Matokeo yake, changamoto hizi hupelekea ukuaji mdogo na usioridhisha wa viwanda vidogo vidogo na huzuia kabisa ukuaji wa viwanda vyenye nguvu vya sekta binafsi (*Ministry of Finance and Planning 2016, uk.31*). Vile vile ifahamike kuwa viwanda vya huduma kama vile utalii huchangia sana kwenye ukuaji wa maendeleo ya kiuchumi kwani huchangia fedha nyingi serikalini kama mapato, lakini nazo pia zinakabiliwa na changamoto zinazofanana na hizi za uzalishaji mali viwandani. Hata hivyo

mtaalamu Wangwe anaongeza kuwa uzalishaji wa viwandani si wa bidhaa za aina mbalimbali na hivyo huathirika kutokana na mabadiliko ya bidhaa za kilimo na bei zake. Hata hivyo mapato ya ndani yanakuwa si makubwa sana kwani hupunguzwa na utegemezi wa kuagiza bidhaa nje na hivyo kukosekana kwa mwendelezo mzuri wa viwanda ambavyo ni muhimu kwa uzalishaji wa ndani na upatikanaji wa ajira. Vikwazo kama vile teknolojia ndogo, upatikanaji wa fedha za kutosha, ukosefu wa sera imara na utawala mzuri bado havijatatuliwa na hivyo kupunguza ukuaji wa viwanda na kuleta mabadiliko stahiki.

Matokeo haya yanaonesha wazi umuhimu wa kubuni mbinu mpya inayohitajika ili kuboresha maendeleo. Yafuatayo ni maelezo ya kina juu ya sekta muhimu na mambo yanayohitajika kwa ajili ya uzalishaji.

### *3.2.2. Mambo muhimu katika uzalishaji*

Kulingana na nadharia ya siku nyingi ya uchumi ni kwamba mahitaji ya uchumi yamegawanyika katika sehemu kuu tatu, nazo ni, nguvu kazi, ardhi na mtaji" (Seitel 2008b, uk.349).

Jedwali namba 2 linaonesha na kuelezea mahitaji hayo.

**Jedwali 2: Nyenzo za uzalishaji**

| Nyenzo za uzalishaji | Tabia/sifa zake |
|---|---|
| Nguvu kazi (kazi) | • Kila aina ya kazi ya mwanadamu hufanywa a) kutimiza mahitaji ya wengine na kwa wakati huo huo b) kujipatia kipato binafsi |
| Ardhi | • Chanzo asilia cha rasilimali zote za dunia<br>• Inajumuisha ardhi ambapo juu yake hujengwa viwanda vyote, na ardhi ya kilimo na misitu,madini ya aina zote, maji ya bahari, maziwa na mito na uoto wa asili. |
| Mtaji | • Bidhaa zote ambazo zimetengenezwa lakini bado hazijatumika, lakini zinaweza kutumika kuzalishia bidhaa zingine.<br>• Inajumuisha, mfano. majengo ya viwanda, mashine, nyenzo, bidhaa zilizotengenezwa tayari ambazo bado hazijauzwa. |

*Chanzo: Seitel 2008b, p. 349.*

Nchi ya Tanzania inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika mahitaji yote haya. Kwa maelezo ya Nitisha (2013) moja kati ya mahitaji makubwa kabisa katika kukuza uchumi wa nchi ni **rasilimali watu**. Idadi na uwezo wa watu waliopo ina uhusiano wa moja kwa moja na ukuaji wa uchumi wa nchi. Uwezo wa watu waliopo unajumuisha ujuzi, ubunifu wao, mafunzo na elimu yao. Upungufu wa watu wenye ujuzi hupunguza kasi ya ukuaji wa uchumi.

Ili kufanikisha ukuaji endelevu wa uchumi wa nchi ni lazima pawepo na watu wengi wa kutosha wenye ujuzi na uwezo unaotakiwa.

Kulingana na takwimu za sensa ya hivi karibuni kabisa, mwaka 2012 Tanzania ilikuwa na watu wapatao 44.9 milioni, kati ya hawa asilimia 79 walikuwa chini ya umri wa miaka 35. Kwahiyo nchi inaweza kuitwa “nchi ya vijana”, kwani idadi kubwa ya wananchi wake ni vijana. Wanaoweza kufanya kazi ni wale wote wenye umri kati ya 15-64, ambao kulingana na sensa ya 2012 ni aslimia 52.2 ya idadi ya wananchi wote wa Tanzania. Watu wanaoweza kufanya kazi wanaongezeka kila wakati kwani hapo 2006 walikuwa 21.0 milioni na kufikia mwaka 2014 idadi hii iliongezeka na kufikia 25.8 milioni na wengi wao wanaishi vijijini. Vile vile inaelezwa kuwa karibu asilimia 87 ya wananchi hawa wanajihusisha na shughuli za kiuchumi (Ministry of Finance and Planning 2016, uk.18, NBS 2015, uk.xvi). **Shughuli za Uchumi za nguvu kazi ya Tanzania ni kwa uchumi wa kujipatia mkate wa kila siku, asilimia kubwa haziingii katika soko la biashara ya dunia.**

Pamoja na kwamba Tanzania ina idadi kubwa ya rasilimali watu, utendaji wake katika soko la ajira hauridhishi na ukosefu wa ajira bado ni changamoto kubwa (UNECA 2016, uk.13). Kwa ujumla ukosefu wa ajira umepungua kidogo kutoka asilimia 11.7 hapo mwaka 2006 na kufikia asilimia 10.3 mwaka 2014. Hata hivyo idadi halisi ya wasio na ajira imeongezeka na kufikia 2.3 milioni hapo 2014 na uwiano kati ya ajira na idadi ya watu umepungua kutoka asilimia 79.2 hapo 2006 na kuwa asilimia 77.8 hapo 2014. Hii ina maana kuwa uwezo wa kutengeneza/kuzalisha ajira kwa nchi umesimama.

**Kielelezo 2. Ajira Nchini Tanzania – Muundo na Takwimu**




*Chanzo: Based on Ministry of Finance and Planning 2016, p. 18; NBS/OCGS 2012, p. iii; NBS/OCGS 2015d, p. xi; NBS 2015, pp. xvi, 37; NBS 2017, p. 22; UNECA 2016, p. 14 (own layout).*

Tatizo la ukosefu wa ajira haliko sawa kwa watanzania wote nchi nzima. Wakati tatizo la ajira Dar es salaam lilishuka kwa asilimia 10 kutoka asilimia 31.5 mpaka asilimia 21.5 katika kipindi cha kati ya 2006 hadi 2014, tatizo hili liliongezeka kutoka asilimia 7 mpaka asilimia 8.4 huko vijijini katika kipindi hicho hicho.

Ukosefu wa ajira kwa vijana unakisiwa kuwa asilimia 11.7 kwa nchi nzima na asilimia 28.8 kwa Dar es salaam (NBS 2015, uk.xx-xxii). Kulingana na maelezo ya Benki ya Dunia, nguvu kazi nchini Tanzania inatarajiwa kuongezeka maradufu ifikapo 2030 kwani karibu watu milioni moja huingia kwenye soko la ajira kwa mwaka. Wizara ya Fedha na Mipango inaeleza kuwa “ongezeko la nguvu kazi mpya kwa mwaka linakadiriwa kufikia 800,000” na Baraza la Ushirikiano na Maendeleo ya Kimataifa la Danish (2016) linasema “ karibu vijana 850,000 huingia kwenye soko la ajira kwa mwaka, lakini nafasi za kazi zinazozalishwa kwa mwaka katika sekta rasmi ni kati ya 50,000 na 60,000 tu. Kwa vile idadi ya watu

walio katika umri wa chini ya miaka 25 nchini ni zaidi ya asilimia 66 ya watanzania wote, basi tutegemee kuona tatizo hili la ajira likiendelea kuongezeka". Kulingana na uchunguzi za mamlaka mbalimbali zilizochunguza suala la ukosefu wa ajira nchini ni wazi kuwa nchi inaweza kuingia kwenye tatizo kubwa kutokana na hali hii. Vile vile inaonekana kuwa hakuna uhusiano wa ujuzi kwa wale wanaohitimu mafunzo vyuoni na mahitaji ya soko kwa sasa (Ministry of Finance and planning 2016, uk.13).

Rasilimali ardhi pia inakabiliwa na changamoto kadhaa kwa sasa. Tanzania ina bahati ya kuwa na sehemu ya nchi kavu kubwa yenye rutuba na ukanda mrefu wa pwani ya bahari, mito, maziwa na madini. Ingawa hizi zinaweza kuwa neema kwa ajili ya uchumi imara, mara nyingi neema hizi hutumika vibaya au kutokuendelezwa kabisa. Ukosefu wa mpango wa matumizi bora ya ardhi, kwa mfano, husababisha matumizi ya hovyo na kuingiliwa kwa ardhi ya kilimo na hifadhi za misitu au hifadhi za wanyama pori (Ministry of Finance and planning 2016). Tofauti na nchi nyingi inayopakana nazo,Tanzania imejaliwa eneo zuri la kimkakati la kijiografia, inayo ukanda mrefu wa bahari ya Hindi na ziwa Victoria, ziwa kubwa kuliko yote barani afrika na la pili kwa ukubwa duniani kwa maziwa yenye maji baridi, lakini pamoja na yote haya bado hayajaonekana kama ni neema inayokumbatiwa. Kwa upande mwingine athari za mabadiliko ya tabia nchi kama vile ukame, mafuriko na kupanda kwa usawa wa bahari ni vitisho tosha kwa rasilimali za nchi. Hata hivyo hakuna hatua stahiki zinazochukuliwa kuzuia mmomonyoko wa udongo (Watkiss 2011, uk.3 na 7). "Hali ya uchumi wa nchi inategemea sana hali ya hewa kwani sehemu kubwa ya pato la taifa (GDP) inategemea mazao ambayo yanategemea sana hali ya hewa hasa yale ya kilimo"(watkiss 2011, uk .3).

### *3.2.3. Sekta Muhimu*

Hizi ni sekta zinazoendesha uchumi wa Tanzania. Sekta ya kilimo inajulikana kama uti wa mgongo wa uchumi wa nchi kwa miaka mingi sasa. Ili kusukuma maendeleo ya viwanda ni muhimu sana kuwa na umeme wa kutosha na wa uhakika. Hata hivyo ili sekta

hizi za kilimo na umeme ziweze kuleta mafanikio katika kujenga uchumi wa viwanda ni lazima sekta ya miundombinu ya uchukuzi na usafirishaji pia ziboreshwe vya kutosha. Zaidi ya hapo suala la upatikanaji wa mitaji na upatikanaji wa soko la uhakika ni mambo ya kipaumbele kabisa.

- **Sekta ya kilimo:** Sekta hii ndiyo mwajiri mkuu hapa nchini (karibu theluthi mbili, asilimia 66.9) ya idadi ya watanzania wote ni wakulima (wizara ya fedha na mipango 2016, uk. 18), lakini huchangia chini ya theluthi tu (asilimia 29) katika pato la taifa (URT 2017, uk. 1). Hii inaonesha jinsi gani sekta hii ya kilimo ina mchango mdogo sana katika pato la taifa pamoja na kwamba ndiyo mwajiri mkuu.

  Sekta hii inahusisha zaidi kilimo cha kujikimu tu na mbaya zaidi ni kuwa inategemea maji ya mvua ambayo wakati mwingine hayana uhakika wa kupatikana (KPMG 2016, uk. 2). Kuboreka kwa sekta hii kungeweza kuinua sana uchumi wa nchi kwani inahusisha watu wengi sana nchini.

- **Sekta ya nishati**: Uzalishaji wa umeme pia unachangia sana ukuaji wa uchumi na uboreshaji wa maisha ya wananchi lakini pia una changamoto nyingi. Mpaka sasa Tanzania bado inategemea kwa kiasi kikubwa umeme unaotokana na maji ya mvua ambayo huathirika sana na mabadiliko ya hali ya hewa na mabadiliko ya tabia nchi. Kufuatia hali mbaya ya hewa kwa vipindi viwili palitokea upungufu mkubwa wa umeme uliolazimisha shirika la uzalishaji na usambazaji umeme (TANESCO) kuingia kwenye gharama kubwa ya uzalishaji wa umeme wa dharura, iliyoongeza uzalishaji wa umeme kwa kutumia gesi asilia kufikia kiwango cha asilimia 34 ya uzalishaji umeme (wizara ya fedha na mipango 2016, uk. 12).

  Gharama kubwa za uzalishaji inatishia uhai wa TANESCO. Uzalishaji wa umeme kwa njia ya mionzi ya jua, upepo na makaa ya mawe bado kabisa haujafanyiwa kazi vya kutosha, ingawa uchunguzi mbalimbali unaonesha kuwa nchi ina hazina kubwa katika nyanja hii ya uzalishaji wa umeme (AfDB 2015).

Hata hivyo uzalishaji kwa njia hizi bado unahitaji kuboreshwa sana ili kufikia uzalishaji wa megawati 10,000 kufikia mwaka 2025 kama mpango wa serikali ulivyo. Sambamba na hilo njia za usafirishaji zinahitajika kupanuliwa sana kwani sehemu kubwa ya wananchi hawajaunganishwa kwenye gridi ya taifa ya njia za umeme (Ujumbe wa Umoja wa Ulaya kwa Tanzania na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki 2016, uk. 3). Inakadiriwa kuwa asilimia 90 ya wananchi wote wanategemea nishati yao wenyewe inayotokana na maliasili ya miti na misitu hasa hasa kuni na mkaa na hivyo kuongeza uharibifu wa mazingira hasa ufyekaji wa misitu.

- **Sekta ya usafirishaji na mawasiliano:** Sekta hizi mbili ziliunganishwa hivi karibuni. Uwekezaji mkubwa pia umefanyika hivi karibuni katika sekta hizi, kwa mfano barabara za lami zimejengwa kuunganisha makao makuu yote ya mikoa (wizara ya fedha na mipango 2016, uk. 11-12). Kwa sasa serikali inajitahidi kuhakikisha mradi wa ujenzi wa Reli kwa kiwango cha kimataifa (Standard Gauge Railway) unafanikiwa. Awamu ya kwanza ya mradi huu imezinduliwa na itakuwa na urefu wa kilomita 2561 ambayo itaunganisha bandari ya Dar es salaam kwa upande wa bahari ya Hindi na Mwanza kwenye ziwa Victoria na Kigoma kwa upande wa ziwa Tanganyika na nchi zisizo na bandari za Uganda, Rwanda Burundi na Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (Bringinshaw 2007; Wizara ya fedha na Mipango 2016,uk. 19-20). Ingawa kuna maboresho kwenye usafiri wa anga na majini lakini bado kuna changamoto za upungufu wa nyenzo na huduma zitolewazo (Wizara ya Fedha na Mipango 2016).

  Kwa upande wa sekta ya mawasiliano, Tanzania ndiyo nchi yenye gharama za chini kabisa katika bara la afrika kwa bei za vifurushi vya intaneti (Lyimo 2016) na kwamba msingi wa mawasiliano ndio kwanza umekamilika kwa kutandaza nyaya za urefu wa kilomita 25000 kuunganisha mikoa 24 ya Tanzania bara ambayo ndiyo msingi hasa wa kuunganisha watumiaji wote (wizara ya fedha na mipango 2016, uk. 17-18).

- **Mtaji na masoko:** Upatikanaji wa mtaji wa kutosha ni muhimu kwa uzalishaji mali wa aina yoyote ile na inaaminika kuwa ndiyo dalili kubwa ya maendeleo kiuchumi. Hata hivyo kwa upande mwingine pamoja na kutokuwa na mitaji ya kutosha watu wanakuwa hawana ujuzi na taarifa ya mahali pa kuwekeza na wawekeze vipi. Kwa upande mwingine, kuanzishwa kwa mfumo wa kutuma fedha kwa njia ya simu kama vile M-PESA imeleta mabadiliko sana nchini Tanzania na kwa nchi nyingine nyingi za Afrika kusini mwa jangwa la sahara na huenda ikaondoa kabisa ombwe la ushiriki katika masuala ya fedha (Abiona/ Koppensteiner 2018).

  Pamoja na kwamba huduma mbalimbali za kifedha na za kibenki zinapatikana nchini, kama vile benki za akina mama na za kidini na zinginezo kwa ajili ya biashara ndogo ndogo na za kati, bado inakuwa vigumu sana kuwafikia na kuwahudumia wananchi walio wengi kwani wanakosa dhamana ya kutosha kupata mikopo. Dhamana zinazohitajika ni hati za milki za ardhi au akiba ya kutosha kwenye akaunti. Wananchi walio wengi hupata huduma kutoka taasisi za kifedha kutoka kwenye mifuko ya kuweka na kukopa iliyoanzishwa kijamii kama vile SACCOS na VICOBA lakini mifuko hii haitambuliwi kama sekta rasmi na haipewi kipaumbele na serikali.

  Pamoja na kupata mitaji ni muhimu pia kujua mahali soko lilipo ili kufanikiwa katika biashara. Kabla ya kuanzisha shughuli yoyote ya uzalishaji mali ni lazima kujua mahali pa kuuzia bidhaa na huduma (aidha soko la ndani au la nje la kimataifa). Kwahiyo upatikanaji wa soko ni jambo la kwanza kabisa kabla ya kuanza shughuli yoyote ya uzalishaji mali (mufuruki, 2017).

  Kwa kuangalia mazingira ya kufanyia biashara, Tanzania iko chini sana miongoni mwa nchi mbalimbali duniani. Kulingana na mpangilio wa Benki ya Dunia, hapo mwaka 2017 ilishika nafasi ya 137 kati ya nchi 190 (Benki ya Dunia 2018a, uk.4) ikilinganishwa na nafasi ya 132 mwaka 2016 (Benki ya Dunia 2017c, uk.7) na nafasi ya 139 kati ya nchi 189 hapo mwaka 2015 (Benki ya Dunia 2016,uk.5). (Jedwali 3 linaonesha hali halisi).

**Jedwali 3: Viwango vya urahisi wa kufanya biashara na viashiria vyake (2015-2017) – Tanzania**

| *TANZANIA* | **Juni 2014 hadi Juni 2015** | **Juni 2015 hadi Juni 2016** | **Juni 2016 hadi Juni 2017** |
|---|---|---|---|
| **Kwa ujumla** | 139 (kati ya nchi 189, kwa viwango vilivyowekwa juni 2015) | 132 (kati ya nchi 190, kwa viwango vilivyowekwa juni 2016) | 137 (kati ya nchi 190, kwa viwango vilivyowekwa juni 2017) |
| **Viashiria** | | | |
| Kuanzisha biashara | 129 | 135 | 162 |
| Kushughulikia vibali vya ujenzi | 126 | 136 | 156 |
| Kupata umeme | 83 | 87 | 82 |
| Kusajili vitu/mali | 133 | 132 | 142 |
| Kupata mkopo | 152 | 44 | 55 |
| Kuwalinda wawekezaji wadogo | 122 | 145 | 129 |
| Kulipa kodi | 150 | 154 | 154 |
| Biashara za kuvuka mipaka | 180 | 180 | 182 |
| Kulinda mikataba | 64 | 59 | 58 |
| Kushughulikia ufilisi | 99 | 100 | 108 |

*Chanzo: Benki ya Dunia 2016, uk. 5 na 239; Benki ya Dunia 2017c, uk. 7 na 244; Benki ya Dunia 2018a, uk.4 na 198.*

Pamoja na kwamba mabadiliko yalifanyika kati ya Juni 2015 na Juni 2016 kwa kupanua wigo wa wanaoweza kukopesheka, lakini ongezeko la kodi ya uandikishaji hati za ardhi na mali hapo 2016/17 imefanya hali kuwa ngumu zaidi na kuyafanya mazingira ya kufanya biashara nchini kuwa magumu zaidi (Benki ya Dunia 2018a, uk. 139).

Mpango wa miaka mitano wa maendeleo wa awamu ya pili (FYDP II) unasema kuwa "vikwazo vya kimfumo na kisera, upungufu wa ujuzi, na matatizo ya kupata ardhi ya viwanda bado vinazuia ukuaji wa sekta binafsi. Pamoja na haya, ukosefu wa upatikanaji wa taarifa muhimu kwa pamoja na kwa haraka (hata katika kituo cha uwekezaji) pamoja na usumbufu wa kodi na ada zinazotozwa na mamlaka kadhaa za udhibiti na utawala; bado zitaendelea kuwa vikwazo na vinaongeza gharama za kifedha na muda katika

kufanya biashara binafsi Tanzania" (wizara ya fedha na mipango 2016, uk. 12-13).

## 3.3. Maendeleo ya Jamii

Kulingana na uchunguzi wa kibajeti wa nyumba kwa nyumba uliofanyika mwaka 2011/12 inaonesha kuwa umasikini umeanza kupungua jinsi uchumi unavyozidi kukua. Umasikini wa mahitaji muhimu umepungua kutoka asilimia 34.4 hapo 2007 na kufikia 28.2% mwaka 2012 na ukosefu wa chakula kutoka asilimia 11.7 hadi asilimia 9.7 kwa mtiririko huo. Hii ni hatua kubwa katika kipindi cha miaka 20 iliyopita (Wizara ya Fedha na Mipango 2016, uk 13). Viashiria katika elimu, afya, maji na lishe pia vinaonekana kuboreka. Hata hivyo bado maendeleo ya wananchi wa Tanzania ni madogo tu na yanaonesha tofauti ya ukuaji kati ya mikoa inazidi kuongezeka kutokana na huduma zinazotolewa na mamlaka za halmashauri za serikali za mitaa (Wizara ya Fedha na Mipango 2016, uk. 13). Ingawa kiujumla umasikini umepungua kutoka asilimia 60 hapo 2007 hadi kufikia karibu asilimia 43 mwaka 2016,inakadiriwa kuwa watu takribani 12 milioni bado wanaishi katika umasikini **uliotopea** (Benki ya Dunia 2017d, uk. 18-19). Hata hivyo hali ya umasikini nchini haionekani kupungua katika idadi halisi ya watu kutokana na ukweli kuwa idadi ya watu inaongezeka kwa kasi (Benki ya Dunia 2017a). Hivyo basi ukuaji wa uchumi wa nchi hauonekani katika hali ya maisha ya wananchi wake.

Mgawanyo wa fedha kidogo pamoja na mafunzo hafifu waliyonayo wananchi bado ni changamoto zinazokwamisha juhudi katika kuleta maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi(Wizara ya Fedha na Mipango 2016, uk.13).

### *3.3.1. Hifadhi ya Jamii*

Kwa mujibu wa shirika la kazi duniani (ILO) kuanzisha na kuendeleza mifumo rasmi ya hifadhi ya jamii ya kutoa msaada wa kifedha na wa kiafya ni hatua kubwa katika kuendeleza jamii za binadamu (ILO 2011, uk. 7). Haijalishi ni njia gani zinatumika, jambo muhimu ni kuhakikisha ustawi wa maisha ya watu unalindwa, pamoja na

kupunguza umasikini, kuhakikisha watu wote wanaweza kufika na kupata huduma katika vituo vya afya, ili kuhakikisha kuwa watu wanaishi maisha bora na utu wao kuthaminiwa (ILO 2011, uk. 8).

Watanzania wachache (Takribani asilimia 8.1) ndiyo wanapata huduma ya hifadhi ya jamii kwenye mifumo rasmi ya kiserikali (UN 2014, uk. 2). Mifuko ya hifadhi ya jamii nchini inayohudumia wafanyakazi wa viwanda, mashirika ya umma na ya binafsi, serikali kuu na serikali za mitaa na wafanyakazi wa majumbani ni pamoja na NSSF, PPF, GEPF, LAPF na PSPF (ISSA 2017,uk. 224-228). Pia tarehe 1, Julai 2016 ulianzishwa mfuko wa fidia kwa wafanyakazi.

Mifuko hii ina umuhimu mkubwa mno kwani hutoa huduma za kulinda uhakika wa maisha endapo mwanachama atapatwa na ulemavu wa muda au hata wa maisha, maradhi, uzazi, umri wa uzeeni, na pia waathirika wa majanga mbalimbali (ISSA 2017, uk. 224-228).

Wafanyakazi kwa ujumla wana hiyari ya kuchagua ni mfuko gani wajiunge nao. Hata hivyo kuna kasoro za kiutendaji za mifuko hii kwani wakati mwingine waajiri hawapeleki makato ya wafanyakazi wao kwenye mifuko kwa wakati na hivyo kusababisha usumbufu kwa wanachama pindi wanapohitaji huduma kutoka kwenye mifuko hii.

Kulingana na taarifa ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2014, kiujumla zaidi ya asilimia 90 ya wananchi wote ikijumuisha wafanyakazi wote wa sekta isiyo rasmi, waliojiajiri,na wale wote wasio na ajira yoyote hawana hifadhi ya aina yoyote ile isipokuwa hukimbilia kwa jamii zao za ukoo kwa ajili ya kupata msaada endapo watapatwa na majanga (UN 2014, uk. 2).

Hata hivyo kwa sasa mifuko ya hifadhi za jamii imepanua wigo pia hata kwa waliojiajiri wenyewe ilimradi tu wakubali kutoa michango yao kila mwezi (ISSA 2017, uk. 224-228). Juhudi zinafanyika kuboresha utendaji wa mifuko hii na kuongeza idadi ya wanachama wanufaika. Hata hivyo bado elimu inahitajika kwa wananchi kwani bado ni idadi ndogo sana inayofaidika na mifuko hii ikilinganishwa na nchi zingine nyingi zinazoendelea (UN 2014,uk. 2).

Mnamo mwaka 2018 ilitungwa sheria mpya ya mifuko ya hifadhi ya jamii ambayo itafuta ile sheria ya mifuko ya hifadhi ya jamii mingi ya zamani kwa kuunganisha mifuko yote ya watumishi wa umma kuwa mfuko mmoja, na wale wa mashirika ya binafsi kwenye mfuko mwingine. Kwahiyo kutakuwa na mifuko miwili tu kwa ajili ya hifadhi ya jamii. Sheria hii inahusu Tanzania bara pekee.

Wazee na walemavu mara kwa mara huachwa wahudumiwe na ndugu na jamaa zao wa kiukoo bila msaada wowote kutoka serikalini. Sheria inatamka kuwa hakuna mwanachama yeyote atakayelipwa mafao kutoka mifuko hii mpaka amefikisha umri wa kustaafu kisheria. Kwa Zanzibar tayari yenyewe inatoa mafao kwa wananchi wote wenye sifa ya kulipwa mafao hayo. Shirika la 'Help Age' duniani limejihusisha sana na kampeni hii na kuondoa changamoto nyingi katika kufanikisha zoezi la kuanzisha malipo haya.

Mwisho kabisa mifuko hii inazo nguvu za kisheria za kuwekeza fedha za wanachama wake sehemu inayoona inafaa kuwekeza. Wengi wao wanawekeza kwenye masuala ya viwanja na ujenzi. Hata hivyo baadhi yao inalalamikiwa kuwekeza kwenye shughuli zisizolipa vizuri na hivyo kuhesabiwa kuwa wanafuja fedha za mifuko hii. Inatakiwa kufanya uchunguzi juu ya suala hili ili kuhakikisha kuwa michango ya wanachama iko salama na kwamba wanapata huduma panapotokea uhitaji.

### *3.3.2. Afya Uzazi na Vifo*

Idadi ya watu Tanzania imekuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa kwa miongo kadhaa sasa kutokana na uzazi mzuri unaoendelea nchini kutokana na hali bora zaidi ya huduma za afya. Kulingana na sensa ya watu ya mwaka2012, kundi kubwa la wananchi lipo kwenye umri wa uzazi na inakisiwa kuwa kila mwanamke mzazi huwa na watoto 5.5 kwa wastani, ingawa kuna tofauti za mkoa hadi mkoa (NBS/OCGS 2015a, uk. iv). Vile vile kuna tofauti kubwa kati ya uzazi wa wanawake wa vijijini na wenzao wa mijini, wale wa vijijini huzaa watoto 6.5 wakati wa mijini huwa na watoto 4.1 kwa wastani (NBS/OCGS 2015a, uk. 44-45).

Hali kadhalika wastani wa kuishi umepanda kutoka miaka 51 hapo mwaka 2002 na kufikia miaka 61 hapo mwaka 2012 na vifo vya watoto vimepungua kutoka watoto 95 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa wakiwa hai na kushuka hadi watoto 68 kwa kila watoto 1,000 hapo 2005 na kuendelea kushuka hadi kufikia watoto 46 kwa kila watoto 1,000 hapo mwaka 2012 (NBS/OCGS 2012;NBS/OCGS 2015b,uk. 57). Kwahiyo inaelekea lengo la milenia la kufikia watoto 38 kwa kila watoto 1,000 hapo 2015 linaelekea kufikiwa (UNDP 2014, uk. xvii). Hata hivyo tatizo kubwa kabisa ambalo linatishia maendeleo ya watu ni utapiamlo. Ikichunguzwa kwenye ngazi ya familia inaonekana kuwa shibe haijaboreka kabisa tangu mwaka 1997 na ni chanzo cha vifo zaidi ya theluthi kwa watoto wanaokufa wakiwa chini ya umri wa miaka mitano (UNDP 2014, uk. xii). Ingawa vifo vya utotoni vimepungua (wizara ya fedha na mipango 2016, uk. 70), lakini tatizo la vifo wakati wa kujifungua bado ni kubwa ikiwa ni watoto 22 kati ya 1000 hufariki punde tu baada ya kuzaliwa hai, na huchangia asilimia 50 ya vifo vya watoto wachanga.

Ili kutoa huduma za msingi za afya kwa wananchi serikali imejitahidi sana kwa kutumia vituo vya umma na vya watu binafsi. Kulingana na maelezo ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kulikuwa na zahanati 4679 na vituo vya afya 481 vilivyosambaa nchi nzima na inakisiwa kuwa asilimia 90 ya wananchi wanaishi umbali usiozidi kilometa tano kutoka kwenye huduma hizi. Hata hivyo hii haizungumzii sehemu kubwa ya wananchi hasa wa vijijini wanaoishi mbali zaidi kutoka kwenye vituo vya afya na wataalamu wa afya waliobobea. Wizara hii pia imeeleza kuwa hapo 2013, Tanzania bara ilikuwa na hospitali karibu 237 za serikali na binafsi ambazo kati ya hizi 57 zilikuwa hospitali za wilaya zinazomilikiwa na serikali na 35 zilikuwa hospitali teule zinazomilikiwa na mashirika ya kidini.

Hali kadhalika kulikuwepo hospitali 5 kwenye ngazi ya wilaya ambazo 4 kati ya hizo ni za jeshi. Kwenye ngazi ya mkoa kulikuwa na hospitali 27 za serikali na 10 za mashirika ya dini zikifanya kazi kama hospitali za rufaa kwenye ngazi ya mkoa kwa ajili ya hospitali za wilaya, na kulikuwepo hospitali 9 za kitaifa zinazofanya kazi za kitaaluma zaidi (MOHSW 2013, uk. 1).

Mwaka 2015 serikali ilianzisha kituo cha uchunguzi na tiba ya magonjwa ya moyo kiitwacho Taasisi ya Magonjwa ya Moyo ya JAKAYA KIKWETE. Hii ni hatua kubwa katika kuboresha huduma za afya nchini kwa ajili ya tiba na uchunguzi. Kituo hiki kinashughulika na utoaji wa tiba na uchunguzi wa magonjwa ya moyo kwa wananchi wa rika zote. Hii imesaidia sana na kupunguza gharama za kusafiri kwenda nchini India na kwingineko kufuata matibabu ya maradhi haya. Fedha zilizokuwa zinatolewa na serikali kugharamikia matibabu na safari za wagonjwa nje ya nchi sasa zinaweza kutumika kwa huduma zingine muhimu.

Pamoja na mafanikio haya matatizo ambayo bado yanahitaji utatuzi katika sekta hii ni mengi. Tukianza na uhaba wa madaktari bingwa katika ngazi zote za huduma ya afya, milipuko ya maradhi kama VIRUSI VYA UKIMWI NA UKIMWI, kifua kikuu na malaria, ugumu wa kufikia huduma ya afya na madaktari bingwa kutokana na umbali na ubovu wa njia za usafiri, umasikini wa kipato na elimu duni kwa wananchi ni mambo ambayo bado yanahitaji kutatuliwa (MOHSW 2013, uk.1-2). Kulingana na maelezo ya mpango mkakati wa sekta ya afya awamu ya tatu, asilimia 35 tu ya nafasi za huduma za afya zinashikiliwa na watu wenye taaluma inayohitajika. Jambo hili linaiacha sekta ya afya katika hali mbaya sana ya kiutumishi (MOHSW 2009, uk. 5). Mwisho wa yote sekta hii ya afya kwa kiasi kikubwa inakosa miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano, wizara haina watumishi wenye ujuzi wa kutosha kwenye masuala ya teknolojia ya habari na mawasiliano, Kwahiyo mawasiliano na wizara zingine inakuwa ni ya shida . Kwa sasa wizara ina miradi ya hapa na pale lakini bila kuwa na mpango wa kitaifa unaoratibiwa vizuri kuna hatari ya kulimbikiza mambo na mwishowe kutokupata matokeo mema kwa wadau wa afya. Wizara ya afya inatambua mahitaji makubwa ya habari na teknolojia kwenye kuboresha utoaji wa huduma ya afya kwa wananchi.

Pamoja na mapungufu yote haya bado Tanzania imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kupigana na maambukizi ya UKIMWI na kuzuia malaria.

Kulingana na maelezo ya wizara, maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI yamepungua kidogo na kufikia asilimia 5 mwaka 2011/2012 kutoka 6% hapo mwaka 2007/2008, kwa wenye umri wa miaka 15-49 (TACAIDS/ZAC/NBS/OCGS/ICF international 2013,uk. 112). Hata hivyo uchunguzi wa awali uliofanyika hapo 2016-2017 unaonesha kuwa maambukizi haya yameshuka na kufikia 4.7% kwa watu wa umri huo huo wa kati ya miaka 15-49 (NBS/OCGS 2017, uk.1).

Hapo mwaka 2012 maambukizi ya malaria yalikuwa asilimia 9.2 kwa watoto chini ya miaka mitano (TACAIDS/ZAC/NBS/OCGS/ICF international 2013, uk. 156), kulinganisha na asilimia 18 hapo mwaka 2007-2008 (TACAIDS/ZAC/NBS/OCGS/ICF international 2013,uk 156 na 160).

Taarifa ya wizara ya afya inaonesha kuwa wananchi wanaopata huduma ya bima ya afya ni wachache na kuwa bado juhudi zinahitajika kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuwa na bima ya afya (Wizara ya Fedha na Mipango 2016, uk. 197). Hakuna mfumo maalumu unaoeleweka wa sera ya afya isipokuwa kwa kiasi kikubwa huduma inapatikana kwa malipo ya papo kwa hapo. Hata hivyo kuna njia mbili kuu zinazotumika kwa bima ya afya ya lazima kwa jamii. Bima ya afya ya taifa ni ya lazima kwa watumishi wote wa umma na ni ya hiari kwa wengine wasio na ajira ya utumishi wa umma.

Njia ya pili ni mfuko wa afya wa jamii ulioanzishwa na serikali kwa msaada wa Benki ya Dunia ili kutoa msaada kwa wananchi wanaoishi vijijini ili wapate fursa ya kufikia huduma za afya na matibabu huko wanakoishi kwa gharama nafuu. Watu wengi zaidi wanafikiwa kwa kuzihusisha hospitali na vituo vya afya. Hata hivyo bado juhudi kubwa inahitajika kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa mifuko hii kwani hadi sasa ni asilimia 14 tu ndiyo wanaopata huduma kwa kutumia mifuko hii (UN 2014, uk. 3).

Tanzania pia inaweza kuchukua fursa kutokana na uwepo wa washiriki wa afya nchini. Mashirika yaliyopo ni yale ya kidini ya kimisionari, ENGENDER na mfuko wa BILL na MELINDA GATES ambayo yote inalenga kusaidia katika kujenga vituo vya afya, kutoa

huduma za afya, kwa kutoa wataalamu na mafunzo ya afya kufikia stashahada na digrii pia. Msaada unaotolewa kwenye mfuko wa BILL na MELINDA GATES unahusika na upunguzaji wa vifo vya watoto wachanga, kupambana na malaria na kudhibiti utapiamlo. Mfuko huu pia unajihusisha na kuleta mabadiliko katika mfumo wa afya kwa kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za afya na kuongeza nguvu kazi na kuboresha mawasiliano na ubora wa madawa na chanjo na kuboresha teknolojia.

Usambazaji na uuzaji wa madawa ya kulevya ni tatizo jingine kubwa linaloisumbua nchi. Vijana wengi wameathirika kwa kutumia madawa haya ya kulevya kama vile heroini, kokeini, bangi na mirungi. Kwa mujibu wa taarifa ya shirika la kimataifa linaloshughulikia mapambano ya madawa ya kulevya na sheria ya kuzuia utumiaji wa madawa haya, Tanzania ina watumiaji wa ndani na vile vile inatumika kama njia ya usambazaji na usafirishaji wa madawa haya. Wasambazaji wa madawa haya waliopo Tanzania wana mtandao mkubwa na wenzao dunia nzima na ndio wahusika wakuu na wahalifu wa madawa haya huko kusini Magharibi mwa nchi za Asia. Baadhi ya watumiaji wa madawa haya tayari wamekwisha kufungwa huko China na kwingineko. Vijana wanaotumia madawa haya ya kulevya hawawezi kufaa kwa shughuli yoyote ya uzalishaji mali kwani muda mwingi wanakuwa dhaifu na wanaharibika kiakili. Serikali ya Tanzania inapambana vikali na utumiaji wa madawa haya. Watumiaji wakuu wa madawa haya wamekwisha kamatwa na kampeni kubwa bado inaendelea nchini juu ya kumaliza tatizo la utumiaji na usafirishaji wa madawa haya.

### *3.3.3. Makundi yaishiyo kwenye mazingira magumu*

Makundi haya ni kama vile wanawake, wasichana, watoto, wazee na walemavu wa aina zote. Kama tahadhari maalumu haijachukuliwa makundi haya ni rahisi kusahaulika katika maendeleo ya kiuchumi wa nchi. Mifano ifuatayo inajadiliwa hapa: Uchumi jamii unajumuisha kila mwananchi bila kubagua kundi lolote ili kuleta maendeleo ya kiuchumi yanayotarajiwa kwa watu wote.

- ***Familia zinazoongozwa na wanawake:*** Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 karibu 42% ya wanawake nchini Tanzania wako katika kundi la umri wa miaka 15 au zaidi, wasio olewa/wasimbe ni 33%, walioachika ni 3.5%, waliotengana ni 1.2% na wajane ni 4.2%(NBS/OCGS 2015c, uk. 18). Kwa ujumla 33.4% ya familia zilikuwa zinaongozwa na wanawake ingawa kuna tofauti ndogo kati ya wanawake wa vijijini na wale wenzao wa mijini (32.6% kwa wale wa vijijini na 34.9% kwa wale wa mijini)(NBS/OCGS 2015c, uk. 13).

  Familia za mzazi mmoja huwa ni dhaifu kiuchumi kwani majukumu yote ya utafutaji wa mahitaji ya familia na maamuzi yote hutegemea mtu mmoja. Wanawake hawa huangalia malezi ya watoto pamoja na kuangalia mahitaji yao yote. Na hii ndio sababu kubwa ya kupigania kuwawezesha ili wawe na ujuzi na maarifa ya kutosha ili waweze kufanya shughuli za kuwaingizia kipato kikubwa cha kutosheleza mahitaji ya familia zao, hasa elimu, makazi na afya kwa watoto wao.

- ***Wazee*:** Wazee ni watu wote wenye umri wa miaka 60 na kuendelea. Kulingana na takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, watu wenye umri wa kuanzia miaka 60 na kuendelea ni sawa na 5.7% ya wananchi wote wa Tanzania (NBS/OCGS 2015c, uk. 8). Kati ya hawa wanaume ni 10% na wanawake ni 14%. Wazee ambao ndiyo walezi wa watoto wadogo ni kundi dhaifu hasa kiuchumi kwani hawana uhakika wa chakula. Kwa baadhi ya maeneo hasa eneo la kanda ya ziwa wanawake wazee hudhaniwa kuwa ni wachawi na mara nyingi hushambuliwa na hata kuuawa kabisa (LHRC/ZLSC 2018,uk. 157-158; URT 2016, uk.6).

- ***Watoto*:** Watoto kwa ujumla ni kundi dhaifu sana na wako katika hatari ya umasikini na unyanyasaji mbalimbali (LHRC/ZLSC 2018,uk. 140-154), kwani hawana uwezo wa kujitegemea na hivyo hutegemea watu wazima kwa mahitaji yao. Familia zenye watoto wengi huathirika zaidi na umasikini kwani vipato vya wazazi wao huwa havitoshelezi mahitaji ya wanafamilia wote. Ingawa mamlaka za kiserikali zimetoa mpango wa

kuwahudumia watoto wote bila malipo kwenye huduma za afya, lakini utekelezaji wake bado umekuwa wa mashaka.

Ili kupambana na umasikini wa kipato, baadhi ya familia huwatumikisha watoto. Huko vijijini watoto wenye umri wa kati ya miaka 5-17, 36.1% ya wavulana na 28.2% ya wasichana hulazimika kufanya kazi mashambani (URT 2016, uk. 6). Utumikishwaji wa watoto na mimba za utotoni huharibu sana nafasi ya kusoma kwa watoto hawa. Mienendo hii si tu inachangia kuwaharibia maisha watoto hawa lakini pia ni mzigo kwa jamii nzima na serikali kwa ujumla. Ikiwa ni mwanachama wa umoja wa mataifa,Tanzania imeridhia mpango wa haki za watoto na imeahidi kuheshimu na kutekeleza mpango huo wa elimu kwa watoto, mahitaji ya kiafya na pia kulindwa katika kutumikishwa na kudhalilishwa kingono. Utekelezaji wa haki hizi za watoto zitawawezesha watoto kuwa huru kiuchumi na kijamii na hivyo kusaidia katika ukuaji wa uchumi wa nchi kwa ujumla.

- ***Jamii za pembezoni au zenye kutengwa*:** Mara nyingi Jamii mbalimbali za wawindaji, wakusanyaji bidhaa za chakula, wachungaji, wakulima, wahamiaji na wale wasiojishughulisha na chochote cha maana, huwa haziwezi kufaidika na huduma za kijamii kutokana na mazingira magumu ya kijiografia na miundombinu ya kuwafikia huko wanakoishi (URT 2016, uk. 6). Mtawanyiko wa makundi haya husababisha ugumu wa kupata wawakilishi kutoka kwao inakuwa ngumu kwa serikali kujua changamoto walizonazo. Wengi wao hawana uwezo wa kupata elimu ya darasani, maji safi na salama na huduma za afya zinazoeleweka.

  Baadhi yao wanazingatia sana mila na desturi ya jamii zao na mara chache mno hushirikiana na jamii zingine kwa masuala mbalimbali kama vile kuoana na kutafuta kazi nje ya maeneo yao ya asili. Kwa ujumla utajiri wao hupimwa kwa idadi ya mifugo aliyonayo mtu kama vile ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku. Hivi karibuni baadhi ya wachungaji na wakulima wameweza kuchanganyika na jamii za watu wengine sehemu

ambako huanzisha makazi kwa mfano kwa kukodisha ardhi na kulima mazao yao. Wengine hupata nafasi za kiuongozi kwenye shughuli za kijamii na kwenye vyombo vya kijamii. Kwa upande mwingine wale wa jamii ya wawindaji wanaonekana kuwa wagumu sana wa kubadili mazoea na taratibu zao za asili.

- ***Watu wenye ulemavu wa ngozi*:** Hapa nchini Tanzania, mara nyingi watu wenye ulemavu wa ngozi – ALBINO wamekuwa wakibaguliwa, kushambuliwa na hata kuuawa kabisa. Hii inatokana na ukweli kuwa kwenye baadhi ya maeneo inaaminika kuwa viungo vyao vya mwili vinaleta utajiri (Wesangula 2015). Ingawa serikali, mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali pamoja na jamii wamejitahidi kuwaelimisha watu juu ya tabia hii ovu na kandamizi, bado watu wenye ulemavu wa ngozi wanashindwa kupata huduma za matibabu na mahitaji mengine maalumu kwa ajili ya ngozi zao kama vile mafuta ya kujipaka, kofia na miwani za kuwakinga na jua na kadhalika.

  Wesangula anaendelea kusema kwa ujumla watu hawa kwa kiasi kikubwa bado wanaonekana kama ni watu wasiofaa kwa lolote na wanabaguliwa sana kwenye shughuli za maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi na katika soko la ajira. Hali hii huwaweka pembeni kabisa mwa maendeleo na hivyo kubaki kwenye umasikini uliotopea (Macron/Vechiatto 2014).

  Kwa ujumla imekuwa vigumu sana kwa serikali kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa watu wanaoishi kwenye mazingira magumu kwa sababu jamii bado inaamini sana kwenye mila na desturi, na mfumo mzima wa jamii huwatenga kabisa watu hawa katika ujenzi wa uchumi wa taifa na maendeleo ya kijamii.

## 3.4. Maendeleo ya Kisiasa

Kimsingi kabisa Tanzania ni nchi ya amani na utulivu, na watu wake wanaishi hivyo. Tangu uhuru kumekuwepo na juhudi kadhaa za kuwafanya watu waishi katika hali bora ya maisha ili wajenge nchi yao. Mabadiliko yoyote nchini kamwe hayawezi kutenganishwa na sera za kisiasa. Mambo ya kisiasa Kama vile

serikali kuhusika na kutunga na kutekeleza sera mbalimbali yana mahusiano makubwa na matokeo ya ukuaji wa uchumi wa nchi. Serikali haina budi kuhakikisha kuwa sera zake zinalenga kuleta mabadiliko chanya kwenye ukuaji wa uchumi na maendeleo.

Ni wajibu wa serikali kuhakikisha mfumo wa kiuchumi unaoendesha nchi unawajali wananchi (kwa kuwashirikisha katika utekelezaji wa mfumo huo) na kwamba utekelezaji wa miradi unakuwa endelevu.

Kulingana na shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo, Tanzania bado inahitaji kutoa sera ya kiitikadi ya kiuchumi inayoeleweka sawasawa na ugatuzi wa madaraka ili kufanikisha mfumo imara wa uchumi. Rais wa kwanza wa Tanzania mwalimu Julius Nyerere aliongoza nchi chini ya mfumo wa chama kimoja, uliotaifisha njia zote kuu za uchumi na kuziweka mikononi mwa umma na kuanzisha UJAMAA ambao ulikuwa ni njia ya kuanzisha maisha ya pamoja vijijini, njia ya kiafrika ya maisha ya kujitegemea. Hata hivyo mfumo huo haukufanikiwa sana kwani ulileta manung'uniko kwa wengi na hivyo pole pole ukaanza kufa ilipofika miaka ya mwishoni mwa 1970 na mwanzoni mwa miaka ya 1980.

Mwalimu Nyerere aling'atuka madarakani mwaka 1985. Mh. Ali Hassan Mwinyi alimpokea mwalimu Nyerere na kuanzisha mabadiliko ya kisiasa na pole pole kuingia kwenye mfumo wa uchumi wa soko huria kutokana na sera ya UJAMAA kuanguka kutokana na utekelezaji wa sera kuwa hafifu na pia kutokana na uongozi wa maagizo kutoka juu tu kwenda ngazi za chini. Tangu kuachana na sera ya UJAMAA, Tanzania ilipoteza dira yake ya maendeleo ya kiuchumi na kujitegemea na kuingia kwenye uchumi unaoongozwa kwa kiasi kikubwa na bidhaa za viwandani na biashara na utalii. Tangu 1985 hadi leo nchi ikategemea maendeleo yanayotokana na uwekezaji wa nje kwa biashara ya makampuni ya kimataifa.

Kutokana na hali hiyo serikali iliandaa mpango wa tozo za kodi kwa kuendeleza uchumi na kuzisahau sekta binafsi ya wazawa. Hii ilipelekea kushuka kwa tija ya wafanyakazi wa Tanzania na vile vile kukosa uwakilishi kwenye masoko ya kimataifa.

Mnamo mwaka 1992 utawala wa vyama vingi ulirejeshwa tena nchini. Hata hivyo bado CHAMA CHA Mapinduzi (CCM) kimebakia kuwa chama tawala kikishindana na Chama Cha Demokrasia Na Maendeleo (CHADEMA), Chama Cha Wananchi (CUF), NATIONAL Convention For Construction And Reform (NCCR-MAGEUZI), Alliance For Change And Transparency (ACT - WAZALENDO), National League For Democracy (NLD) na vyama vingine 13 vilivyoandikishwa kwa msajili wa vyama vya siasa. Madhumuni ya utawala wa vyama vingi vya siasa ni kupanua na kukuza demokrasia nchini na vile vile kuboresha utawala bora.

Kwa kawaida chama tawala huunda serikali wakati vyama vya upinzani vinatarajiwa vitoe ushauri wa namna mambo yanavyoweza kuboreshwa na kudhibiti nguvu ya serikali ili kuweza kupata mwafaka wa kuendesha mambo kwa pamoja ili kukuza uchumi wa nchi na kujiletea maendeleo.

Idadi ya watu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo Tanzania ni mwanachama na inajumuisha nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Sudani ya Kusini ilikua kwa 2.9% hapo 2014 na 2015 kutoka watu 145.4 milioni na kufikia watu 149.7 milioni (EAC 2016b, uk. 15). Jumuiya hii ni soko la muhimu sana kwa bidhaa za Tanzania lakini kusimama kwa mchakato wa muungano kamili wa kijumuiya kumezuia unufaikaji wa kutosha wa nchi kutokana na soko hili.

Pamekuwepo na sera na matamko mbalimbali ya kisera tangu uhuru na yafuatayo yanaelekeza umuhimu wa sera na matamko haya ili kuonesha hali halisi ya kisiasa ilivyo kwa sasa.

### *3.4.1. Sera ya elimu*

Ingawa Tanzania imepata mafanikio makubwa katika kuhakikisha watu wanapata elimu na kupunguza kutojua kusoma na kuandika, bado elimu inayotolewa haina uhusiano wa moja kwa moja na uchumi na tija kwa taifa. Kuanzia Januari 2016 kila mtoto wa umri wa kwenda shule anaweza kuipata elimu msingi bila ada.

Serikali ilikwishapiga marufuku malipo ya mafunzo kwenye shule za msingi tangu mwaka 2011 kupitia mipango yake miwili ya elimu

kwa shule za msingi na utekelezaji kwa elimu ya sekondari mwaka 2015 (El-Noshokaty/Gebert 2017, uk.1).

Kuondolewa kwa ada mashuleni kuliwawezesha mamia ya watoto kuandikishwa shuleni. Serikali ya Tanzania ilipiga hatua kubwa sana katika lengo la nne la kimataifa la kuleta maendeleo endelevu na hivyo kuhakikisha kuwa watu wote wanapata elimu bora na endelevu katika maisha yao yote. Hata hivyo mabadiliko haya yana changamoto zake. Ili kufanikisha utekelezaji mzuri wa sera hii pametokea ongezeko kubwa la mahitaji mbalimbali. Ongezeko hili la wanafunzi wa shule za msingi na sekondari linamaanisha pia ongezeko la waalimu wa shule hizi, ongezeko la vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama vile vitabu, madawati n.k. Zaidi ya hayo ni lazima fedha za kutosha zipelekwe na kupokelewa kwa wakati mashuleni kwa ajili ya kununulia vifaa hivi. Pamoja na haya walimu lazima wapewe mtaala mzuri na wa kudumu. Pamekuwepo na mabadiliko ya mara kwa mara katika mtaala ambayo yamesababisha mkanganyiko na hivyo kuchapisha vitabu vyenye makosa na matokeo ni kufifisha ubora wa elimu inayotolewa mashuleni.

Vile vile Dr. kitima ameeleza kuwa pamekuwepo na mabadiliko kadhaa katika juhudi za kupanua wigo wa elimu nchini, lakini mabadiliko hayo yamefanywa kisiasa zaidi kuliko kitaaluma na matokeo yake hayalengi uchumi wa nchi wala kukuza demokrasia inayokusudiwa, isipokuwa ni wakati wa mwalimu Nyerere tu ambapo elimu ya kujitegemea ilimlenga mwanafunzi mwenyewe na pia maslahi ya taifa kwa ujumuishi wa kila mtu (Kitima 2017, uk. 3).

Ndugu Sambaiga anasema kwamba dira ya taifa ya 2025 inahimiza kupata wasomi wengi na wenye sifa na ujuzi wa kuwawezesha kutatua matatizo ya nchi kwenye nyanja za jamii, kupambana na changamoto za maendeleo ya nchi ili kukabiliana na ushindani uliopo wa kikanda na wa kidunia (taasisi ya elimu Tanzania 2013, uk.9).

Kulingana na takwimu za tume ya vyuo vikuu nchini vyuo vikuu vilivyopo nchini vimefikia 77 (Sambaiga 2017, uk. 11; TCU 2015).

Hata hivyo elimu itolewayo nchini bado haiendani na mabadiliko ya kiuchumi wa taifa.

Mpango wa miaka mitano wa maendeleo wa awamu ya pili unasema kuwa bado kuna tofauti kati ya wahitimu wa vyuo vikuu na mahitaji halisi ya soko la ajira (Wizara ya Fedha na Mipango 2016, uk.13). Inaonekana kuwa wahitimu wa shule walio wengi hawana ujuzi wa kazi yoyote, hata ile ya kurudi vijijini na kuwa wakulima kama wazazi wao, hawana. Hali ya elimu mashuleni haiwaruhusu kupata ujuzi wa aina yoyote wa kuwawezesha kuendesha maisha yao, ni wachache sana wanaoweza kujiunga na vyuo vya ufundi au vyuo vya elimu ya juu. Hii inaonesha kuwa vijana wengi hawana nafasi ya kujifunza ufundi wa aina mbalimbali ili kuwawezesha kuanzisha na kuendeleza biashara. Pamoja na hayo bado inaelezwa kuwa mfumo wa elimu nchini hauna nafasi ya kuongeza ajira kwa vile tuna mtaala na mafunzo duni na njia za kujifunzia pia ni duni. Pia mabadiliko ya mara kwa mara yanayotokea kwenye mitaala ya kufundishia kulingana na maamuzi binafsi yasiyopata muda wa kutosha wa majadiliano na wadau mbalimbali, na ukosefu wa falsafa maalumu ya elimu, upanuzi wa elimu ya msingi na sekondari bila kuwa na mpango madhubuti uliopangwa na kujadiliwa kwa muda wa kutosha na kuunganishwa na mpango wa maendeleo wa taifa (Kitima 2017, uk. 6-7). Kutokana na utafiti wa kisayansi uliofanywa na Simon (2013) na Massawe (2014), ndugu Sambaiga anasisitiza kuwa ni muhimu kwa vyuo vya elimu kutoa mafunzo kwa wanafunzi yanayowaandaa vijana kulingana na mahitaji ya soko la ajira (Sambaiga 2017, uk. 11).

### *3.4.2. Nguvu kazi na sera ya ajira*

Sambamba na dira ya maendeleo ya taifa 2025, sera ya ajira ya taifa inalenga kuongeza ukuaji wa ajira kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchi, kupunguza ukosefu wa ajira na hivyo kuwa na ajira zenye hadhi kwa watanzania wote wenye sifa (URT 2008, uk. vii).

Kwa sasa tatizo la ajira bado ni kubwa hasa kwa maeneo ya mijini na miongoni mwa vijana. Kwa ujumla vijana bado wanapata changamoto nyingi za ajira kwani wengi wao wanajihusisha na

shughuli za kichuuzi ili kuwawezesha kuishi. Kwahiyo nchi inahitaji mfumo madhubuti wa kiuchumi utakaoongeza nafasi za ajira, lakini pia kuwapa vijana uwezo wa kujiajiri wenyewe na kuajiri wengine pia.

### *3.4.3. Sera ya ushirikiano wa kimataifa.*

Kama yalivyo mataifa mengine ya kiafrika, Tanzania inahitaji sana kuongeza ushirikiano wa kimataifa wa kiuchumi ili iweze kuleta ushindani wa kweli na kuvutia wawekezaji wazawa na wa nje na kuongeza biashara kwa kuondoa vikwazo vya biashara ili kupunguza au kuondoa umasikini kati ya wananchi na kuboresha mashirikiano ya kibiashara kwenye masoko ya kimataifa. Tanzania ni mwanachama wa kiuchumi katika mashirika kadhaa ya kikanda, Afrika na katika jumuiya ya kimataifa. Hii ni pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Shirikisho la nchi za Kusini mwa Afrika, Shirikisho huru la kibiashara barani yaani the Continental Free Trade Area (CFTA), mpango wa sheria maalumu ijulikanayo kama African Growth Opportunity Act (AGOA) (CTI 2016a).

Jumuiya ya Afrika mashariki inajumuisha nchi wanachama zipatazo sita. Iliundwa kwa mara ya pili hapo mwezi Novemba 1999 na inakusudia kuweka biashara huru katika eneo lote la nchi hizi. Hii ina maana ya kuondoa ushuru wa forodha kati ya nchi hizi na badala yake kuweka kodi inayokubaliwa kwa wote kwa bidhaa zinaoingia na kutoka ndani na nje ya nchi hizi (EAC 2017a). Kwa kuongezea nchi hizi zinaangalia uwezekano wa kuanzisha sarafu moja ya fedha itakayotumika katika nchi zote wanachama kwa shughuli za kibiashara ndani ya nchi hizi kwaajili ya soko la pamoja litakaloruhusu uhuru wa bidhaa, watu, ajira na mtaji kwa nchi hizi wanachama (EAC 2017b). Jambo la nne na la mwisho ni kuwa na shirikisho la kisiasa la nchi hizi. Kwa kuwa jumuiya hii inakisiwa kuwa na idadi ya watu wapatao 150 milioni ikiwa na pato la taifa la dola bilioni 146 za kimarekani kulingana na takwimu za 2016, basi ushirikiano huu wa kikanda ungeiwezesha Tanzania kuwa na soko kubwa la kibiashara na fursa nyingi za kiuchumi lakini pia kujiongezea nguvu ya ushawishi wa kisiasa si barani afrika pekee lakini hata kimataifa kwa ujumla (EAC 2017e).

Hata hivyo, kutokana na changamoto za ndani na pia kwa kujali zaidi maslahi ya kila taifa, ushirikiano huu wa jumuiya ya afrika mashariki unaenda pole pole sana hadi kufikia sasa.

## 3.5. Maendeleo ya kiteknolojia (sayansi, teknolojia na ubunifu)

Ili kukuza uchumi kwa kiwango cha kufaa ambacho kinahusisha uchumi jumuishi na endelevu ni lazima taifa lifikie hatua ya kujitegemea kiteknolojia na maarifa. Uchumi jamii utasaidia Tanzania kukuza maarifa na teknolojia yake yenyewe.

Teknolojia inahusika na matumizi ya mifumo ya kisayansi na maarifa. Maendeleo katika teknolojia yanaweza kusaidia sana katika kuongeza tija kwa kutumia nyenzo au bidhaa kidogo tu. Kwa kawaida nchi zinazowekeza vya kutosha katika kukuza teknolojia huonekana kukua haraka kuliko zile zisizojali maendeleo ya teknolojia katika uzalishaji mali wao. Uchaguzi na matumizi ya teknolojia sahihi vile vile vinachangia sana katika kukuza tija na kujenga uchumi.

Kwahiyo ni jambo la muhimu kabisa kuwekeza katika kujenga teknolojia inayohitajika kwa hali ya Tanzania katika kuanzisha viwanda vya kimkakati na shughuli za majumbani kwa ujumla. Kuongezeka kwa kipato cha mtu mmoja mmoja kupitia kwa shughuli za kiuchumi lazima zihusishwe na matumizi ya teknolojia inayokidhi ushindani wa soko. Hadi sasa Tanzania imeamua kutenga kiasi cha 1% ya pato la taifa kila mwaka kwa ajili ya kuendeleza matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Hata hivyo lengo hili bado halijafanikiwa kikamilifu, kwani matumizi ya serikali katika utafiti na maendeleo yalikuwa 0.4% ya pato la taifa hapo 2014/15 (Wizara ya Fedha na Mipango 2016, uk.17). Kuhusiana na kukua kwa teknolojia za kisasa na kuja kwa mfumo wa kidijitali, Tanzania bado iko katika kiwango cha chini ikiwa ni ya 126 kati ya nchi 139 hapo 2016 na bado inaendelea kubaki nyuma ya nchi kama Uganda ambayo ni ya 121, Nigeria ya 119 na Kenya ikiwa ni ya 86(world economic forum 2016, uk. 16).

Matumizi haya ya teknolojia ya upashanaji habari na mawasiliano kwa njia ya mitandao kwa watu binafsi na kwa shughuli za kibiashara unaonekana bado ni mdogo sana (Esselaar/Adam 2013). Kulingana na mpango wa maendeleo wa miaka mitano awamu ya II, Tanzania bado ina matumizi madogo sana ya njia hizi za kisasa kutokana na gharama za kuzipata kuwa kubwa, na vile vile kuziboresha na kuwa za kisasa, lakini pia kutokana na vizuizi vya kupata haki za utumiaji na vile vile kuwa na ujuzi mdogo wa teknolojia hizi mpya. Lakini pia sekta binafsi imekuwa vigumu kuchangia katika mfuko wa utafiti na maendeleo kutokana na uelewa mdogo wa umuhimu wa teknolojia hizi katika masuala ya kifedha na kujenga uchumi. Pia hakuna wadau wa aina mbalimbali wanaojitokeza na hakuna washiriki wa kutosha katika suala hili. Inaonekana wazi kuwa kuna umuhimu wa haraka wa kusambaza matokeo mbalimbali ya tafiti kwa watu wote na kuhusisha matokeo hayo na viwanda na kuwajulisha watunga sera.

## 3.6. Maendeleo ya mazingira

Maliasili hupatikana kutoka chini au juu ya ardhi. Maliasili hizi zinajumuisha mimea, viumbe wa majini na muonekano wa nchi ulivyo, pamoja na mafuta, gesi asilia, vyuma na madini. Maliasili za nchi yoyote zinategemea tabia nchi na mazingira yake yalivyo na matumizi ya maliasili hizo hutegemea ujuzi na uwezo wa nguvu kazi iliyopo, teknolojia inayotumika udhibiti wa serikali iliyopo, upatikanaji wa mitaji na mgawanyo wa mapato. Maliasili zote ni lazima zitumike kwa namna endelevu na kufaidisha vizazi vyote vya nchi vilivyopo na vijavyo.

Tanzania ni nchi iliyojaliwa sana neema ya kuwa na maliasili nyingi (Wizara ya Fedha na Mipango 2016, uk. 58) na matumizi yake endelevu yanaweza kuwa ni ufunguo wa uhakika wa mabadiliko ya kiuchumi. Kwa mfano nchi ina utajiri mkubwa wa aina nyingi za wanyamapori mbalimbali, misitu ya asili, fukwe nzuri na safi, milima, mito, maziwa, madini na gesi na tabia nchi nzuri ya kitropiki na utamaduni mzuri unaovutia watalii wa kutoka sehemu mbalimbali dunia (UNDP 2016b, uk. 2).

Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa linasisitiza kuwa ukuaji wa uchumi wa Tanzania unategemea sana mazingira yake mazuri na rasilimali zilizopo kwani 80% ya jamii ya watanzania hasa wa huko vijijini wanayategemea mazingira hayo (UNDP 2016 b, uk. 2).

Hata hivyo Tanzania ina rasilimali safi endelevu, lakini bado haijatumika kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi na kijamii katika nchi.

Maliasili endelevu zenyewe ni pamoja na uzalishaji wa umeme wa maji, makaa ya mawe, upepo, jua na mabaki ya takataka za mimea. Kati ya hizi inayotumika kwa kiwango cha kuridhisha ni uzalishaji wa umeme wa maji pekee (AfDB 2015, uk. 32-35).

- Maji ndiyo yamekuwa njia kuu na ya kutegemewa katika kuzalisha umeme nchini Tanzania mpaka sasa, ikiwa na uwezo wa kuzalisha megawati 562 kwa taarifa ya mwaka 2015. Mradi mwingine unaotarajiwa kuanzishwa ni wa ujenzi wa kituo cha umeme kwenye maporomoko ya stiegler's Gorge huko kwenye hifadhi ya wanyama ya selous (oirere 2017). Ingawa matumizi ya maji katika kuzalisha umeme ni makubwa lakini maji kwenye mito hupungua kutokana na ukame na hivyo kupunguza utegemezi wa njia hii ya uzalishaji umeme. Hata hivyo umbali kati ya vituo vya uzalishaji na mahali unapohitajika umeme ni jambo ambalo lazima liangaliwe, ikichukuliwa kuwa mfumo wa usambazaji umeme bado ni duni.

- Miradi midogo midogo ya hadi megawati 10 ya uzalishaji wa umeme kwa njia ya maji inamilikiwa na vikundi binafsi na havikuunganishwa kwenye gridi ya taifa. Ingawa mwaka 2015 vituo vidogo vidogo vilivyounganishwa kwenye gridi ya taifa vilichangia karibu megawati 15, vinaweza kuwa na uwezo mzuri kwa umeme usio kwenye njia za kitaifa (EAC/KAS/ForumCC 2016, uk. 29).

- Uzalishaji wa umeme kwa njia ya makaa ya mawe unatazamiwa kuwa na uwezo mkubwa kama njia mbadala ya uzalishaji umeme ingawa ukubwa wake bado haujajulikana. Makisio yanakadiriwa kuwa megawati 650 na vituo 50 vimekwisha

kuchunguzwa kama ilivyoelezwa kwenye taarifa ya 2015. Uzalishaji kwa njia hii unajulikana kuwa njia ya uhakika kwani hauathiriki na mabadiliko ya tabia nchi wala ya hali ya hewa (EAC/KAS/ForumCC 2016, uk. 29).

- Uchunguzi wa upepo kama njia ya uzalishaji umeme inayojiendesha yenyewe ulionesha kuwa wa matumaini huko Kititimo (Singida) na Makambako (Iringa). Maeneo haya yanaonesha kuwa yana upepo wa kutosha kuendesha mitambo ya kufua umeme wa kuingizwa kwenye gridi ya taifa. Hata hivyo panahitajika utafiti zaidi juu ya fursa na changamoto zilizopo za njia hii ya uzalishaji umeme.

- Kulingana na maelezo ya benki ya maendeleo ya Afrika, Tanzania ina uwezo mkubwa wa kuzalisha umeme kwa njia ya jua kwani inazo saa kati ya 2800-3500 za jua kali kwa mwaka, na mionzi sambamba na usawa wa ardhi ya 4-7 kilowati kwa kila mraba wa mita 2 kwa siku. Aina tatu za umeme wa jua zinaweza kutofautishwa; 1) bila ya kuunganishwa kwenye gridi, (2). Uliounganishwa kwenye gridi. (3). Joto tu la jua. Njia zote hizi zinaweza kutumika kama mbadala wa uzalishaji umeme vijijini na au hata mijini.

- Uzalishaji wa umeme kwa kutumia mabaki ya mimea kama takataka ulichangia 18 megawati kwa umeme wa gridi na karibu 58 megawati kwa umeme wa viwanda vya kilimo kama ilivyotolewa na benki ya maendeleo ya Afrika. Matumizi ya umeme wa aina hii ya kibiashara yameanza kujitokeza na umeme huu unajumuisha mabaki ya maganda ya miwa, maranda ya mbao, mabaki ya katani na pumba za mchele (EAC/KAS/ForumCC 2016, uk. 30-31).

Umeme wa aina hii pia hutumika majumbani kwa kupikia, kuongeza joto wakati wa baridi na kwa shughuli zinginezo (AfDB 2015, uk. 35; EAC/KAS/ForumCC 2016, uk. 32), na hivyo sekta ya misitu Tanzania inachangia sana kuleta mabadiliko ya kiuchumi (UNDP 2016, uk. 4). Kwa mfano 90% ya wananchi wote wanategemea nishati inayotokana na mazao ya misitu kama vile kuni na mkaa.

Pamoja na hayo sekta hii ya misitu huchangia karibu 50% ya mahitaji ya ujenzi kama vile mbao, boriti, papi na mirunda. Vile vile sekta hii huchangia karibu 10-15% ya mauzo yote ya nje na kuliingizia taifa 10% ya mapato ya nje. Sekta hii imeajiri watu wanaokadiriwa kufikia 1 milioni kwa shughuli ya kutengeneza na kusambaza mkaa nchini (AfDB 2015, uk. 35).

Pamoja na yote haya bado shirika la maendeleo la umoja wa mataifa linasisitiza kuwa "pamoja na uchangiaji chanya wa sekta hii katika kukuza maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi, lakini umasikini wa hali ya juu ukichangiwa na ongezeko kubwa la haraka la watu, yamechangia sana kukuza tatizo la uharibifu wa mazingira ". Ukataji hovyo wa miti umesababisha kutoweka kwa misitu, upotevu wa bayo anuwai na uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji na mvua. Matumizi ya rasilimali yasiyo endelevu husababisha upungufu mkubwa wa rasilimali hizo ambazo ndizo kinga ya uhai wenyewe wa binadamu na usalama wake wa maisha kwani husababisha ukosefu wa chakula na hivyo kuzidisha umasikini zaidi. Utegemezi mkubwa wa shughuli za kilimo na ongezeko la haraka la watu vyote vinachangia kuongeza joto katika mazingira na rasilimali zilizopo (UNDP 2016b, uk. 4).

Pamoja na kwamba inajulikana kuwa mazingira na rasilimali huleta maendeleo jumuishi ya muda mrefu kwa jamii, lakini matokeo yanaonesha kuwa kwa kiasi fulani hayatumiki kwa maendeleo endelevu, na wakati huo huo mchango wake katika maendeleo endelevu hauonekani. Inawezekena hii inatokana na mambo mawili kwa pamoja kutokuhimiza sheria zilizopo na ukosefu wa ufahamu wa sera zilizopo vile vile fursa na changamoto zake. Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni linasisitiza sana juu ya utumiaji wa redio za kijamii kuwaelimisha watu juu ya namna ya kuhifadhi mazingira na viumbe hai mbalimbali viliopo (UNESCO 2016).

Kwa nyongeza, taarifa ya mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi inaeleza kuwa matokeo mabaya yanayosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi kama vile kuongezeka kwa joto, kupungua kwa mvua zinazonyesha, na vipindi vya majira

kubadilika na kusogea na majanga ya mafuriko na ukame yote yanaathiri shughuli za kilimo, nishati na biashara pamoja na mazingira kwa ujumla wake na hivyo kuifanya hali kuwa mbaya kupindukia. Inahitajika mipango sahihi ya haraka ya kukabiliana na mabadiliko haya ili kuirejesha nchi katika hali yake ya kawaida.

## 3.7. Uchambuzi Yakinifu wa Kutambua Uwezo-Udhaifu-Fursa na Changamoto za Tanzania

Matokeo ya uchambuzi wa hali ilivyo nchini yamejumuishwa kwenye jedwali lifuatalo kulingana na sehemu kuu nne, nazo ni Uwezo uliopo, Udhaifu, Fursa na mwisho Changamoto zilizopo. Uchambuzi huu unafanyika kwa lengo la kufanya utekelezaji wa mfumo wa uchumi wa soko shirikishi wa jamii ufanikiwe.

**Uwezo** ni yale mambo yaliyo nchini ambayo yanaipa nchi uwezo wa kufanya mambo vizuri, wakati **madhaifu** ni yale mambo yanayoifanya nchi isifanye mambo yake vizuri ikilinganishwa na nchi zingine. **Fursa** ni yale mambo ambayo nchi inayo au inaweza kuyapata nje na ingeweza kuyatumia kwa manufaa yake, na mwisho **changamoto** ni yale mambo ambayo yanaweza kuleta matatizo kabisa nchini.

**Jedwali 4. Uwezo, madhaifu, fursa na changamoto.**

| Uwezo | Madhaifu |
|---|---|
| • Ukuaji wa uchumi uliotulia<br>• Idadi kubwa ya vijana(nguvu kazi ya kutosha )<br>• Upatikanaji wa ardhi yenye rutuba na maliasili nyingi za aina mbalimbali<br>• Nchi ipo pazuri kijiografia (bandari, bahari,maziwa n.k)<br>• Umoja wa kitaifa, amani na maelewano,lugha moja,mshikamano wa kweli.<br>• Miundombinu imeboreshwa na mtandao wa mawasiliano umesambazwa pote nchini.<br>• Elimu kwa wote na ongezeko la vyuo vya elimu ya juu.<br>• Afya: ongezeko la hospitali za kisasa (kama vile hospitali ya moyo ya Jakaya Kikwete) | • Umasikini –idadi ya masikini ni kubwa na tofauti kati ya wenye nacho na wasionacho inaongezeka<br>• Teknolojia na viwanda – elimu ndogo ya teknolojia, uwekezaji mdogo kwenye teknolojia ya kubadili mambo kwenye viwanda vidogo na vya kati,utegemezi mkubwa katika njia za asili za kilimo.<br>• Sekta binafsi na biashara – ni dhaifu kwa upande wa wazawa na kampuni za wazawa ni chache kwa biashara za kimataifa.<br>• Soko la ajira – wasio na ajira ni wengi pamoja na wasomi wa vyuo vikuu wasio na ujuzi wa kutosha kulingana na soko la ajira<br>• Elimu – thamani ya elimu ni ya chini (vitendea kazi duni, ufundishaji duni)<br>• Afya – mfumo dhaifu wa utoaji huduma (kwa mfano, ukosefu wa wataalamu wenye ujuzi unaofaa wa kiweledi, na bima ya afya ipo chini sana, haijawafikia wengi)<br>• Nishati na maliasili- upatikanaji wa umeme usio na uhakika na matumizi mabaya ya maliasili.<br>• Hali ya uchumi – ukosefu wa dira na itikadi ya kiuchumi, utekelezaji hafifu wa mbinu bora za zamani. |
| **Fursa** | **Changamoto** |
| • Soko na biashara – makubaliano kati ya nchi na nchi na ushirikiano wa kikanda kama vile, jumuiya ya afrika mashariki, jumuiya ya nchi za kusini (SADC),shirikisho la biashara afrika,mpango wa makubaliano ya kibiashara na marekani kuhusu mazao ya kilimo na madini.<br>• Kubadilishana teknolojia baina ya mataifa<br>• Mawasiliano - gharama ndogo ikilinganishwa na nchi zingine za Afrika<br>• Huduma za afya – kuna wadau wa afya kwa ajili ya kuboresha huduma za afya<br>• Mitaji – uboreshwaji wa soko la mitaji (mfano, M-PESA)inavotumika barani afrika<br>• Hali ya ushindani – ongezeko la bidhaa za Tanzania (hasa mazao ya kilimo) inayotokana na ongezeko la watu kikanda.<br>• Baadhi ya nchi jirani hazina bandari<br>• Mifumo ya soko – uwepo wa mifumo kwa ajili ya uchumi wa soko huria la kijamii (nchi za Ujerumani na zile za kiNordik) ambayo inaweza kukubalikaTanzania. | • Masoko huria na biashara – utawala wa makampuni makubwa ya kimataifa dhidi ya biashara za wazawa.<br>• Teknolojia – ushindani mdogo kwenye ulimwengu unaobadilika haraka kiteknolojia.<br>• Mazingira – hali ya hewa isiyoridhisha na mabadiliko ya tabia nchi yanayotokea<br>• Hali ya ushindani wa kibiashara:mazingira mazuri kwenye nchi zingine<br>• Hali ya kisiasa isiyotulivu katika nchi zinazopakana na Tanzania. |

Kama uwezo na fursa vikisimamiwa na kuendeshwa vizuri na kama madhaifu yakishughulikiwa na yakibadilishwa na kuwa uwezo na changamoto zikapunguzwa kabisa, Tanzania itaingia kwenye kundi la uchumi wa soko endelevu na jumuishi kwa watu wote. Maelezo yaliyopo kwenye kitabu hiki yanakusudiwa kuwa mwongozo wa mfumo wa uchumi wa soko huria wa kijamii unaokusudiwa kuanzishwa nchini Tanzania.

# 4. Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii kwa Tanzania

Baada ya kutathimini nadharia ya Uchumi wa Soko Jamii kwa ujumla na kujua mafanikio ambayo nchi imefikia katika nyanja tofauti za kiuchumi na kijamii, ni dhahiri kwamba taifa linahitaji kuweka upya mtazamo wake na fikra yake ya kiuchumi. Serikali ya Tanzania ilianzisha mipango mikuu mitatu ili kuwa na maendeleo endelevu, nayo ni: Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mpango Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Mkakati Jumuishi wa Maendeleo ya Viwanda 2025. Ili kuwa na utekelezaji wa mipango wenye mafanikio inaaminika kwamba ni vyema kila mwananchi ashiriki na afaidike na matunda yatokanayo na ukuaji wa uchumi. Mfumo wa Uchumi wa soko Jamii kwa Tanzania unaonekana ni chaguo sahihi ili kujenga uchumi ambao ni imara, jumuishi na endelevu.

## 4.1 Dira na Dhima

Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii kwa Tanzania (SMET) una dira ya kuwa na taifa imara lenye maendeleo endelevu na taasisi zitakazojikita kuwezesha ukuaji na maendeleo ya kiuchumi yatakayowagusa watu wote. Katika Dira ya Maendeleo ya Kitaifa 2025, Tume ya Mipango ilikusudia kutengeneza miongozo mipya itayozingatia uchumi wa soko baada ya sera za maendeleo kupata changamoto kwa miaka kadhaa. Tume ilihimiza uwepo wa dhana ya ubunifu, ujasiriamali na ushindani, pamoja na uwekezaji wa kutosha katika maendeleo ya watu (Planning Commission 2000). Kwa kuzingatia hilo, mfumo wa SMET unaongeza chachu na thamani katika dira ya maendeleo ya kitaifa 2025.

Miaka kumi na nane baada ya kuandaa dira ya maendeleo ya kitaifa, maeneo mengi yanaonekana hayataweza kufikiwa kwa ukamilifu mpaka kufikia 2015, kwa mfano, ubora wa juu wa maisha, jamii iliyoelimika, utawala bora au uchumi wa ushindani. Kwa kuzingatia hali ya sasa ya taifa, mfumo wa SMET unatoa mikakati na nguzo za kimaadili zitakazoboresha hali ya uchumi na maisha kwa baadaye. Sera za sasa za umma zinakosa

miongozo ya wazi, jumuishi na itikadi zitakazowezesha uwepo wa maendeleo kwa wote. Kwahiyo, mfumo wa SMET ni matokeo ya tafakari ya pamoja itakayoleta ufumbuzi halisi wa changamoto mbalimbali, kwa kuzingatia ushirikishwaji wa jamii. Mfumo huu unapendekeza uwepo wa mpango wa sera unaoainisha wajibu wa wadau wote muhimu katika kuunga mkono juhudi za kuleta maendeleo. Mfumo umezingatia mikakati ya muda mfupi na mrefu na kupendekeza maboresho yanayoweza kufanyika katika sekta muhimu.

Maono ya kipindi kifupi ya SMET ni shughuli zote za maendeleo ya nchi kuzingatia uwepo wa uchumi jumuishi ambapo biashara huru na ushindani vinakua na uwiano mzuri unaosimamiwa na serikali, ilihali jamii na uwepo wa mazingira rafiki vinakuwa msingi wa maamuzi.

## 4.2 Nguzo za Kimaadili

Ili mfumo huu wa Uchumi wa Soko Jamii ufanikiwe Tanzania unategemea jinsi gani watekelezaji watakavyoelewa na kuhusianisha mfumo na shughuli za kibiashara katika ngazi zote kuanzia vijijini, wilayani, mikoani, kitaifa na kimataifa. Maadili yanaweka msingi kwa washiriki wote katika uchumi na maendeleo ili kuhakikisha maamuzi yao na kile wanachofanya kinakua na mwongozo. Kifupi cha nguzo hizo za maadili ni "**KWA NCHI YETU**".

**K** – *Knowledge,* **Ujuzi** na uelewa kwenye taarifa muhimu kuhusu shughuli za kiuchumi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko, soko la ndani na ziada kuuzwa nje huongeza ufanisi na kuzuia gharama zisizo za lazima. Ujuzi wa kitaalamu pia ni msingi wa kuwa na nguvukazi yenye uwezo. Nguvukazi iliyoelimika ni chanzo cha ubunifu na uwepo wa huduma bora. Mbali na haya, ujuzi na uelewa kwenye namna masoko yanavyofanya kazi na kuwa na taarifa muhimu kuhusu, kwa mfano, bei za bidhaa, kiasi na aina ya bidhaa inayohitajika sokoni, wazalishaji wa bidhaa husika, hali ya ushindani n.k ni vitu muhimu kuwezesha uchumi wa soko jamii uwe na ufanisi.



**W** – *Wisdom,* **Hekima** ni jambo muhimu kwenye siasa kufanikisha uwepo wa utawala bora. Mfumo wa SMET ni wa kijamii zaidi kwa sababu binadamu ni chanzo au kitovu cha yote. Mfumo unazingatia uwepo wa uchumi jumuishi, ambapo watu wote wanajitoa kufanya shughuli za kiuchumi na wanafaidika na matunda ya ukuaji wa uchumi. Ili kufanikisha hayo, mfumo huu wa kiuchumi unahitaji wanasiasa wanaowajibika na wanaotekeleza kwa ufanisi mipango na mikakati yote ya muda mfupi na mrefu bila ya kuingiliwa na kuathiriwa na mataifa ya nje na uwepo wa rushwa. Kwa hiyo, nchi inahitaji watendaji wenye hekima kwa kiasi fulani ili kufikia malengo makuu yaliyowekwa na kutetea maadili yake bila ya vikwanzo.



**A** – *Accountability*, **Uwajibikaji** unahakikisha wadau wote kwenye uchumi wanafanya kazi ili kufikia maendeleo yenye usawa. Wadau wanapaswa kuwa wawajibikaji katika maamuzi yao ambayo kwa namna moja au nyingine yanaathiri maisha ya watu na taifa kwa sasa na baadaye. Maamuzi katika kazi yana athari kwa kundi fulani la watu. Ni muhimu kuzingatia utawala wa sheria, haki ya mali binafsi na utaratibu wa kidemokrasia. Mfumo imara wa mahakama usioingiliwa, uchumi unaotegemea kunufaika na matunda yake, na uchaguzi huru na wa haki ni njia ya kuondoa matendo mabaya katika nyanja tofauti za wadau.



**N** – *National first*, **Uzalendo** ni “ile hali ya kulipenda taifa lako (...) na kujivunia” (Kamusi ya Cambridge 2018). Watanzania wanaweza kujivunia utajiri wa kitamaduni, jamii yenye amani na uwepo wa rasilimali nyingi. Wananchi wanapaswa kujengewa uwezo na kufahamu uwepo wa haya yote ili kuwa na taifa imara na huru. Ingawa, uzalendo hauna maana ya kujiondoa au kutoshiriki. Mtazamo finyu na ule wa ndani zaidi unaweza kujenga taifa lililodumaa na kuathiri maendeleo ya kipindi kirefu cha baadaye. Kwahiyo, taifa linahitaji kutafuta uwiano wa kati ya kujiamini lenyewe na kufungua mipaka na dunia.



**C** – *Community*, **Jumuiya** inatoa nafasi ya mshikamano, kufanya kazi kwa pamoja na kusaidiana ili kufikia mafanikio. Pia ni sehemu ambayo watu wanaweza kupata utambulisho wa pamoja, kulingana na yale yanayowatofautisha au wanayofanana. Katika dunia ya sasa ambayo kutofahamiana kunaongezeka, dhana ya jamii inaweza kutumika kuunganisha tofauti zilizopo. Kwa sababu haiwezi kupelekea ubaguzi na uvunjifu wa haki za kiraia, jumuiya ni kiungo muhimu ili kuwa na jamii iliyo na umoja na amani.



**H** – *Human dignity,* **Utu wa kibinadamu** ni suala muhimu katika uwepo wa maendeleo endelevu. Ni vigumu nchi kudhani imeendelea kama wananchi hawawezi kuwa na rasilimali na mazingira rafiki kwa ustawi wa maisha. Kwahiyo, mfumo wa SMET unahusisha dhana ya kutopima maendeleo kwa kuangalia kukua kwa uchumi pekee bali pia kuruhusu watu kuboresha hali zao za maisha. Maamuzi ya kisiasa na kiuchumi lazima yalinde maisha ya watu, mazingira na taasisi. Matunda ya kiuchumi yasipatikane kwa kukiuka haki za kibinadamu.



**I** – *Integrity*, **Uadilifu**: Wadau wote kupitia mfumo huu wa kiuchumi wanapaswa kuzingatia uaminifu. Ili kusimamia na kulinda wengine dhidi ya matumizi mabaya ya mamlaka, taasisi huru zinapaswa kusimamia mapato na matumizi ya fedha na kutoathiriwa na wanasiasa na wadau wengine kwenye uchumi.



**Y** – *Youth*, **Vijana:** Uwepo wa vijana kwenye jamii na nguvu kazi kubwa kwenye soko la ajira kuna tafsiri kubwa mbili, ya fursa na changamoto kwa taifa. Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii kwa Tanzania unawaweka vijana kama sehemu muhimu, kama taifa jipya na viongozi wa baadaye. Kwahiyo, ili kuwa na mafanikio ya nchi siku za usoni, ni vyema kuongeza wigo wa upatikanaji wa elimu bora, kukidhi mahitaji ya lazima na



kuruhusu watoto wakue vizuri katika uwepo wa huduma nzuri za afya na mazingira rafiki ya watoto na kijana kujiendeleza.

**E** – *Evaluation*, **Tathmini** ya sera za kimaendeleo na shughuli zote za kiuchumi ni hatua muhimu kufanyika ili kufanya maamuzi sahihi, kujifunza kulingana na makosa na kutekeleza mbinu mpya kuleta mageuzi. Wadau wote muhimu kwenye uchumi lazima wafanye tathmini ya matokeo ili kujua uwezo na mapungufu yao. Ili kuwa na ufanisi, kufanyika kwa tathmini lazima kuambatane na kuchukua hatua kwa wakati na kufanya maamuzi yenye tija.



**T** – *Transparency*, **Uwazi** katika kufanya maamuzi na kutekeleza kunapaswa kuzingatia kila mdau anapaswa kuwa na uelewa katika kile kinachofanyika au katika yale yatakayofanyika. Uwazi ni nyenzo muhimu katika demokrasia pia kwa sababu watu wana uhuru na wanapaswa kupewa taarifa kuhusu maamuzi ya viongozi ambao waliwachagua na wafanye tathmini ya utekelezaji wa sera na baadaye kushiriki uchaguzi wa awamu nyingine wakiwa na taarifa sahihi. Kwa upande wa sera za kiuchumi na fedha, uwazi hupunguza hali ya kutokua na uhakika. Kama wadau kwenye uchumi wanajua dhamira ya serikali, watapanga mipango yao na kuwekeza kulingana na mazingira halisi.



**U** – *Unity*, **Umoja/Mshikamano**: Watanzania wanaishi kwa uelewano, amani na mshikamano toka nchi ipate uhuru. Umoja wa kitaifa ni tunu muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi kwa kuwa huwezesha nchi na mazingira kuwa imara na rafiki kwa uwekezaji na biashara. Umoja unaweza kutumika kuweka msingi wa mshikamano na unapaswa kutunzwa na kuimarishwa siku zote.



## 4.3 Mikakati

Mfumo wa SMET umehamasishwa na uzoefu na mafundisho yaliyopatikana kutoka nchi kadhaa ambazo zilifanikiwa kupitia Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii. Lengo ni kusukuma maendeleo

ya kiuchumi mbele, kufikia maendeleo yenye usawa, na hatimaye kupunguza umasikini kwa kiwango kikubwa. Katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, taarifa zinaonyesha ukuaji wa uchumi pekee hautoshi kuondoa umasikini nchini Tanzania. Mbali na wastani wa ukuaji wa uchumi kuwa 7%, mfumo wa sasa umeonyesha si toshelevu kuweza kuleta maendeleo na kuboresha hali ya maisha kwa jamii nzima. Kukosekana kwa uwiano mzuri kati ya aliyenacho na asiyenacho na utofauti wa vipato ngazi ya mikoa umeendelea kuongezeka (Matotay 2014).

Mfumo wa Uchumi wa soko Jamii unawezesha uwepo wa biashara ya ushindani huru – yenye ufanisi – inayoambatana na huduma za bima na usalama – zinazofanikisha huduma za mifuko ya hifadhi ya jamii iliyobora kwa wananchi – inapunguza changamoto za mfumo wa soko huru. Katika mfumo huo wa kiuchumi, soko la ajira linakua lenye kuruhusu mabadiliko, ambapo kiwango cha mshahara kinaendana na nguvu ya soko na kuhamasisha ajira mpya. Hata hivyo, kiwango cha vijana wanaoingia katika soko la ajira Tanzania kinasababisha idadi kubwa watu wanaotafuta kazi, na hivyo kupelekea uwepo wa mishahara midogo na kiwango kikubwa cha wasio na ajira. Kwahiyo, ili kukabiliana na wimbi la umasikini kwa ufanisi, soko la uchumi linapaswa kukidhi mahitaji ya wasio na ajira na kutoa sera za kijamii. Haya yanaweza kufanikishwa na uwepo wa utaratibu kama uwepo wa kima cha chini cha mshahara chenye kukidhi mahitaji ya kila mwajiriwa na kinachotekelezeka. Sera za kijamii zinazolinda maslahi ya wafanyakazi zinazoweza pia kuhusisha msaada wa kifedha wa moja kwa moja kutoka serikalini kwa kundi la watu wasio na kipato cha uhakika na kuwajengea uwezo.

Benecke (2008) na Kohler (2007) katika machapisho yao wameainisha maeneo muhimu ya kisera ambayo yanahitaji mifumo ya udhibiti na taasisi husika ili kutoa miongozo ya kiutendaji katika uchumi na kanuni za Uchumi Jamii kusaidia kuwezesha kufanya maamuzi. Mikakati ya SMET itakua kwenye muundo kulingana na maeneo ya kisera ambayo yamefafanuliwa hapa chini. Kama maeneo hayo yatatekelezwa kulingana na kanuni na nguzo za Uchumi Jamii pamoja na maadili (“KWA NCHI

YETU") ya SMET, basi mikakati hii itaweza kuipeleka Tanzania kwenye hatua nzuri zaidi ya kimaendeleo.

### *4.3.1 Mipango na Uratibu*

Mipango na uratibu wa Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii kwa Tanzania unahusisha uwekaji wa malengo na kuhakikisha taasisi na wadau wote muhimu wanajua nafasi zao, majukumu na wajibu wao. Utekelezaji wa mfumo, SMET, pia unahitaji hali ya kufanya kazi kwa pamoja na ushirikiano ili kufikia malengo yaliyowekwa. Kwa kuangalia mfumo wa uchumi mkubwa na muundo wa jamii kwa mapana yake, nchi inapaswa kuweka malengo na kuratibu shughuli za umma kuanzia ngazi ya chini kabisa, ngazi ya mikoa na kitaifa, na kuweka mwongozo wa kisheria kwa serikali. Pia serikali inapaswa kutoa mwongozo wa aina za bidhaa za umma na kuweka vipaumbele kwa ajili ya utekelezaji (Benecke 2008, uk. 15). Hii inahusisha:

- **Kuweka mfumo wa kisheria unaoaminika**
  Kanuni zinapaswa kuweka wazi aina ya shughuli ambazo zinafanywa na taasisi nyingine za umma (mfano: sera za kifedha kufanywa na Benki Kuu)[1] na majukumu yapi yanafanywa na sekta ya umma (Benecke 2008, uk. 15). Uwazi na uimara wa utaratibu ni kitu muhimu ili kuweka mazingira rafiki kwa ajili ya uwekezaji, biashara na ustawi wa mifuko ya hifadhi ya jamii. Mfumo wa kisheria na matokeo yake kwenye ngazi zote kuanzia ile ya chini unahitaji uratibu wa uhakika kutoka serikalini kwa faida ya taifa. Mfano, kwa sasa nchi ya Tanzania inakosa uratibu wa wazi wa shughuli za umma ili kuhakikisha kinachofanywa na ngazi za juu kinaleta matokeo ngazi za chini. Hili ni muhimu "ili kuweka misingi ya uchumi imara, ufanisi na utawala unaoungwa mkono na wananchi na kwenda sambamba na misingi ya utawala bora" (KAS 2009, uk. 1). Serikali inatakiwa kutoa mwongozo wa kisheria na kuonyesha majukumu ya

1 Nchini Tanzania, kwa mfano, kifungu cha 5 cha "Sheria ya Benki Kuu, 2006" (BoT 2006) inaeleza majukumu ya msingi ya Benki Kuu ya Tanzania, baadhi ya majukumu hayo ni, "kutekeleza majukumu ya Benki Kuu na, bila ya kuingilia jukumu kuu lililotajwa awali, kuanzisha, kutekeleza na kuhusika moja kwa moja na sera za fedha, ikiwa na pamoja na sera ya kiwango cha kubadilisha fedha, kutoa sarafu, kuratibu na kusimamia mabenki na taasisi za kifedha" (Kifungu 5.-(1)) na "itakua huru na kuwajibika" (Kifungu 5.-(3)).

taasisi za umma na bodi za usimamizi, kuratibu vizuri taasisi zote na kutofautisha majukumu yake na yale yanayofanywa na sekta binafsi. Kwa kukasimisha mamlaka kwenye taasisi huru, na kuzipa uwezo na mamlaka, serikali inaweza pia kuongeza nguvu kwenye mapambano ya rushwa, ambayo ni hatua muhimu ya maendeleo ya kiuchumi kwa taifa.

- **Kuweka na kulinda utaratibu unaolinda heshima na utu wa mtanzania**
  Mikakati na mipango ya serikali inapaswa ilenge kulinda watu wake. Kwa mfano, uvunjifu wa haki za wafanyakazi au ajira kwa watoto ni mambo yasiyovumilika katika nchi huru inayofuata utawala wa kidemokrasia. Uhuru wa kukusanyika ni suala muhimu katika jamii ya kidemokrasia, na msingi wa wananchi kuanzisha, kubuni na kuleta chachu ya mabadiliko katika uchumi. Kwahiyo, lazima ziwepo taratibu ambazo zinaheshimu haki za binadamu, lakini pia kuwepo kwa mfumo huru wa mahakama. Wajibu wa serikali na watunga sheria sio kuzuia kila jambo, bali kuzijengea uwezo taasisi ambazo zitalinda usalama na kuhakikisha ulinzi wa wanyonge dhidi ya wenye nguvu. Ili kukuza ulinzi wa watu wote na kusimamia haki za binadamu, taasisi hizo husika zinapaswa kuwa sehemu ya sauti ya jumuiya za kiraia. Ili kuyafikia matokeo ya muda mrefu na mafaniko endelevu kwa kuzingatia haki kati ya kizazi na kizazi, ni vyema kuhakikisha mazingira yanalindwa na shughuli za kiuchumi zinafanyika bila ya kuleta athari hasi kwenye ardhi, maliasili na uoto wa asili. Utaratibu unapaswa kuwekwa katika ngazi zote kuanzia serikali za mitaa, mikoa mpaka taifa.

- **Toa mwongozo na uelekeo**
  Katika mfumo wa SMET, jukumu la serikali ni kutoa motisha zaidi kuliko kuingilia katika shughuli zote za kiuchumi. Ili kuwa na taasisi za umma zinazowajibika, serikali inaweza kutumia nyenzo tofauti – mf. njia za udhibiti na motisha za kifedha – kulingana na umuhimu wa lengo na matokeo ya hatua kwenye uchumi. Kwa mfano, ajira kwa watoto au utumwa mamboleo vinakinzana kabisa na utu wa binadamu na ni mambo yasiyovumilika ndani ya mfumo wa kiuchumi

wa SMET. Ni mambo ambayo serikali inapaswa kulinda watu wake kupitia mfumo wa sheria na mahakama, uliojengewa uwezo. Pia, ni jambo gumu kuzalisha bila ya kuwa na matokeo na/au madhara kwenye mazingira. Kwahiyo, ili kuwa na njia nzuri za kupunguza madhara, serikali inaweza kutumia njia zenye motisha kwa pande zote (kutoza kodi au kutoa ruzuku) ambazo zinatoa mwanya kwa taasisi na makampuni kulingana na uwezo na nafasi yao katika sekta husika. Nchini Tanzania, ajira kwa watoto imeonekana ikigusa sana shughuli za migodi na kilimo bila ya kuzingatia mustakabali wa baadaye wa watoto katika kupata elimu. Kumekua na motisha ndogo kwa taasisi za wazawa katika kutoa mwanya wa ruzuku na kodi. Kwa kuzingatia hatua ambazo zimeratibiwa vizuri, kuutumia mfumo wa SMET kutaboresha mustakabali wa watoto na kuleta hamasa ya biashara kufanyakazi na kushindana kwa haki kufikia maendeleo endelevu nchini. Kufanyakazi kwa uwazi ni hitaji la msingi la kuwa na mwelekeo mzuri kwa wadau wote (Benecke 2008, uk. 15).

- **Kutoa kipaumbele kwenye bidhaa na huduma za umma**
  Kwa kuzingatia kanuni ya jamii mahalia kuwa na uwezo wa kujihudumia yenyewe, serikali lazima itoe huduma za jamii[2] "kama soko haliwezi kutoa huduma hizi au zinatolewa kwa upungufu kuliko mahitaji"; hii ni pamoja na, kwa mfano, utolewaji wa miundombinu ya kutosha kama barabara za umma na fursa ya elimu ya msingi pamoja na huduma za afya zinazojitosheleza (KAS 2009, uk. 5). Ingawa, serikali inapaswa kufanya kwa kiasi fulani; kuingilia kati ni muhimu hasa kama jamii inaathirika (KAS 2009, uk. 5). Kwa mtazamo huu, serikali ya Tanzania inahitaji kuhusika katika kuboresha miundombinu hasa ya vijijini, kwa mfano.

2 Huduma za umma zina sifa sifuatazo: si-pinzani na hazimtengi mtumiaji. Huduma hizi si-pinzani kwa maana ya pale zinapotumiwa na mtu fulani basi hazipunguzi kiasi chochote kinachoweza kutumiwa na mtu mwingine. Huduma hizi pia hazimtengi mtu katika kuzitumia, kila mtu ana uhuru wa kuitumia.

***Eneo la kiutafiti la kujifunza kuhusu utolewaji wa bidhaa na huduma za umma: miundombinu***

Imethibitika kwamba miundombinu inaleta matokeo chanya kwenye ukuaji wa uchumi. Kwa upande mwingine, upungufu wa miundombinu unaathiri kwa sehemu kubwa na kulemaza ustawi wa biashara na taasisi nchini Tanzania. Utafiti wa Benki ya Dunia unaonyesha miundombinu duni imechangia kwa 34% kudumaza tija ya wazalishaji wa bidhaa wa Tanzania, taarifa hiyo pia imeonyesha ukosefu wa miundombinu ya usafirishaji inayojitosheleza ni changamoto kubwa zaidi kwa wazalishaji wa bidhaa, ikifuatiwa na upatikanaji wa huduma ya maji (Shkaratan 2012, uk. 3).

Usafirishaji ni muhimu ili kufanikisha mawasiliano na biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine. Kuhusu miundombinu ya barabara, taarifa ya Benki ya Dunia ya mwaka 2012 imeonyesha Tanzania inafanya vizuri zaidi kuliko nchi nyingine Afrika. Ingawa bado kuna changamoto nyingi za kufanyiwa kazi ili kuendelea kutoa mchango wa kufanikisha biashara, mawasiliano na hatimaye kukuza uchumi. Ingawa mikoa na nchi jirani zinaunganishwa na barabara, bado mtandao wa barabara nchini ni mdogo ikilinganishwa na nchi nyingi barani Afrika. Hii maana yake ni kwamba, maeneo mengi vijijini hayafikiki kwa urahisi, maeneo ambayo ndipo watu wengi zaidi wanaishi kwa sasa. Ni 24% tu ya wakazi waishio vijijini wanaweza kufikiwa na barabara misimu yote katika eneo la mzunguko wa chini ya kilomita mbili. Kiwango hiki ni kidogo kuliko nusu ya wastani wa kiwango kinachopaswa kwa nchi zenye uchumi wa kati. Kuendelea kuimarisha mtandao wa barabara ni jambo la msingi ili kuwaunganisha watu na kurahisisha mawasiliano, hasa kuyafikia masoko ya bidhaa za kilimo (Shkaratan 2012, uk. 15-17).

Soko la ndani Tanzania la usafirishaji wa anga ni miongoni mwa masoko makubwa zaidi kusini mwa jangwa la Sahara. Ingawa, taarifa nyingi za kiutafiti zinaonyesha viwanja vingi nchini Tanzania vinahitaji maboresho makubwa, kulindwa na kupanuliwa ili kukidhi mahitaji ya ongezeko la wasafiri, hasa kutokana na utalii. Kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Julius Nyerere cha Dar es Salaam, mbali na kuwa kikubwa zaidi nchini, pia kinahitaji uwekezaji na maboresho. Kimekua kikielemewa kwa miaka mingi na kinahitaji upanuzi ili kuhudumia wasafiri wengi zaidi na kutoa huduma bora (Shkaratan 2012, uk. 15-19). Taarifa za ulinganifu za uridhikaji wa wasafiri zinaonyesha uwanja

wa ndege wa Dar es Salaam ukishika nafasi ya chini kabisa duniani, maeneo ambayo yamekua yakiangaliwa ni kama usafi, usalama, faraja na urahisi wa kuunganisha safari. Kutofanya vizuri kwenye maeneo haya kunahatarisha ukuaji wa sekta ya utalii, eneo ambalo ni muhimu kwenye uchumi wa nchi (Sleeping in Airports 2017). Pia, viwanja vingi nchini havina uwezo wa kuruhusu ndege kubwa kutua: njia ya kutua ndege ni fupi na zisizo na ubora. Ili kuendeleza shughuli zake, kukuza usafiri nchini na kuziunganisha nchi nyingine duniani vyema maboresho ya kisasa yafanyike na kutanua miundombinu ya usafiri wa anga nchini (The Citizen 2016).

Kwa upande wa upatikanaji wa maji na usafi wa mazingira, Tanzania bado inakumbwa na changamoto kubwa. Kulingana na utafiti wa Kessy na Mahali wa mwaka 2012, 57% ya wakazi wa vijijini na 77% ya wakazi wa mjini hawapati maji safi na salama. Ingawa, nchi inaendelea na juhudi za kuboresha usafi wa mazingira, kwa takwimu za mwaka 2011 – 88% ya watanzania bado haipati nyenzo sahihi za kukabiliana na changamoto hizo (Kessy/Mahali 2017, uk. x). Uwekezaji unahitajika ili serikali ifikie malengo yake ili wananchi wapate maji safi na salama, na vifaa vya kutunza usafi wa mazingira. Serikali inahitaji kuwa na taarifa sahihi ya hali ya sasa kwenye sekta husika na kutengeneza mikakati madhubuti ya jinsi gani ya kufikia malengo ya kutoa huduma bora ya maji kwa 85% ya wakazi vijijini na 95% ya wakazi wa mjini kwa 2020 na kufikia 100% mwaka 2025. (Tanzania Invest 2016a). Tanzania imeweza kupata fedha kutoka vyanzo tofauti ili kuboresha huduma ya maji na miundombinu ya usafi wa mazingira. Kwa mfano, mkopo ulitolewa na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) ili kuboresha hali hizo kwa Arusha (Tanzania Invest 2015), pia nchi ilipata mkopo kutoka India ili kutoa huduma bora Zanzibar (Tanzania Invest 2016b). Mwisho, Benki ya Dunia ilikubali kutoa mkopo wa kufanya maboresho ya huduma ya maji na mazingira kwa wakazi 1.9M wa Dar es Salaam (Tanzania Invest 2017). Kwahiyo, kulingana na vyanzo vya fedha vilivyopo na vikiambatana na mikakati ya utekelezaji, huduma ya maji na usafi wa mazingira ulio bora kwa wananchi wengi unapaswa kutolewa na serikali.

Eneo jingine linalohitaji kuvutia uwekezaji na kukuza tija ni huduma ya nishati, mfano umeme. Katika eneo hili la nishati ya umeme, shirika linalomilikiwa na umma la TANESCO ndilo linaloongoza kutoa huduma katika soko nchini Tanzania. Hata hivyo, shirika

linakabiliwa na changamoto nyingi katika kipindi cha hivi karibuni, kutokana na masuala ya kitaasisi na kimuundo. Zaidi ya yote, shirika limekua likipata hasara kutokana na uwepo wa bei ndogo ya nishati isiyoakisi gharama za uzalishaji na ugumu katika ukusanyaji wa mapato, ambayo imekua ikisababisha madeni na kutishia uwezo wa shirika kutoa huduma bora (Reuters 2017). Mbali na hilo, huduma isiyoridhisha ya nishati nchini pia imesababishwa na kutokuwepo na uchakavu wa miundombinu. Ili kuhakikisha ubora wa huduma ya nishati na miundombinu, nchi inahitaji kutoa kipaumbele kwenye maeneo kadhaa ikiwemo kuhakikisha wakazi wengi hasa wa vijijini wanaunganishwa kwenye umeme wa gridi ya taifa. Kwa sababu, kwa mwaka 2012 watu karibu 70% walikua wanaishi vijijini na kasi ya kuwaunganisha na huduma ya umeme ni 7% tu. Maboresho ya kuwafikishia wananchi wengi huduma ya umeme yanaonekana kwenye mikakati ya serikali, ambapo imepanga kuongeza hatua na kuwaunganisha wakazi wengi zaidi wa vijijini (Tanzania Invest 2018b). Kwa hivi karibuni, wastani wa matumizi ya umeme kwa kila mtu nchin Tanzania ni 108 masaa ya kilowatt kwa mwaka (kWh) ambayo ni madogo sana ikilinganishwa na nchi nyingine duniani. Kwa kulinganisha, wastani wa matumizi kwa kusini mwa jangwa la Sahara kwa mwaka yanafikia 550kWh na wastani duniani ni 2,500kWh kwa mwaka. Maendeleo ya kiuchumi yanapaswa kuleta hamasa ya kuongeza mahitaji ya umeme nchini ambayo yanakadiriwa kukukua kwa 10-15% kwa mwaka. Kwahiyo, serikali inapaswa kuongeza uzalishaji wa nishati ya umeme. Mwaka 2015, serikali ilipanga kuongeza uwezo wa uzalishaji kwa zaidi ya 500% kufikia mwaka 2025 (Tanzania Invest 2018b). Ili kuhakikisha uendelevu na ubora wa huduma, upanuzi wa huduma ya nishati unapaswa kupangwa kwa umakini, ikiambatana na mikakati mizuri inayotekelezeka pamoja na uwepo wa miundombinu mizuri, inayoaminika na kutosheleza.

### *4.3.2 Mali Binafsi*

Ndani ya mfumo wa SMET sekta binafsi imepewa umuhimu mkubwa katika kuendesha shughuli za kiuchumi. Mtu mmoja mmoja na makampuni binafsi lazima yapewe ulinzi wa kikatiba wa mali zao. Umiliki wa mali binafsi bado unabaki kuwa muhimu kwa wazawa kushiriki vizuri kwenye soko la ndani na la kimataifa.

Utaratibu huo “unatoa motisha ya kuongeza kipato kupitia kazi na ni msingi wa ujasiriamali wenye ubunifu” (KAS 2009, uk. 2). Kulingana na utafiti wa Global Property Guide, haki ya kumiliki mali binafsi ni “suala la muhimu ambalo linaathiri shauku ya uwekezaji kwenye milki ya makazi” (Global Property Guide 2008). Mali binafsi ni vyema zitengenezwe na kulindwa na sheria ili kuzuia migongano na kuwalinda wanunuzi ambao umiliki wao haupaswi kuwa na changamoto. Kwahiyo, mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii hauwezi kufanya kazi vizuri bila ya haki miliki ya mawazo na mali.

Katiba ya nchi ya mwaka 1977 inatoa mwongozo wa “haki ya kumiliki mali” (Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kifungu cha 24). Ingawa, katika taarifa ya kipimo cha ukokotoaji wa haki miliki – ambapo **0** ina maana ya hakuna ulinzi na **100** ni ulinzi wa haki miliki uliokamilifu – **tanzania ilipata alama ya 34**. Kiashiria hiki hupima kiwango cha ulinzi wa haki miliki ndani ya taifa kwa kuangalia sheria, matukio ya upendeleo, uwezo wa watu na biashara na ubora wa mahakama katika uhuru wa kutoingiliwa na nguvu za kisiasa na kiwango cha rushwa (Global Property Guide 2018).

Katika taarifa ya Benki ya Dunia ya Ufanyaji wa Biashara ya 2018, Tanzania ilishika nafasi ya 142 kati ya nchi 190 katika urahisi wa kusajili mali. Usajili wa mali unachukua wastani wa siku 67 na unagharimu kiasi kinachokaribia 5.2% ya thamani ya mali. Kupitia ripoti hiyo, hali imeonekana kuwa mbaya kutokana na mabadiliko yanayofanyika mara kwa mara na kufanya Tanzania ipate alama ya 50.13 kati ya alama 100. Kwahiyo, alama ya Tanzania ni ndogo kuliko wastani wa 50.43 wa kitaifa kwa mataifa yaliyo kusini mwa jangwa la Sahara (ambayo pia ni ndogo kwenye ukanda wote wa Afrika) na ni alama ndogo kuliko nchi nyingi jirani kama Burundi, Kenya, Malawi, Msumbiji, Rwanda na Uganda (World Bank Group 2018a). Ripoti hiyo pia imeonyesha njia za digitali na utunzaji wa taarifa zote kuhusu maeneo na kanzi data zinachangia kurahisisha usajili wa mali.

Hakuna soko rasmi la ukodishaji wa mali binafsi nchini Tanzania. Kutokana na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, ardhi yote

inamilikiwa na serikali. Mtanzania anaweza tu kukodisha kwa kipindi cha miaka kuanzia 5 hadi 99. Kwa wawekezaji wa nje haki ya kumiliki ardhi ni finyu zaidi. Wageni wanaweza kukodisha ardhi kwa matumizi ya uwekezaji kwa kupewa kibali hicho na serikali au kwa kukodisha kwa ubia na mwekezaji mzawa (Export.gov 2016).

Ni jambo jema kuwa na makubaliano ya wazi, utaratibu na mipaka kuhusu umiliki wa mali unaotolewa na serikali. Kutaifisha njia za uzalishaji, bidhaa na huduma kunawezekana hasa kama kunafanywa ili kulinda maslahi ya umma na mmiliki wa awali anafidiwa ipasavyo kulingana na taratibu zilizopo. Pale ambapo sheria kuhusu mali binafsi zinatekelezwa, ubunifu na uvumbuzi unaweza kuibuliwa na kuwa chachu ya watu kujiajiri na kuwa wawajibikaji ndani ya taifa, na baadaye kupelekea mfumo wa ushindani ambao huleta uendelevu wa shughuli za kiuchumi na kuongeza wigo wa kodi ambao huongeza mapato ya serikali.

### *4.3.3 Utaratibu wa Fedha*

Inaaminika kwamba “soko katika uchumi linahitaji sera za kiuchumi za muda mrefu na hasa zile zinazoleta uimara wa uchumi mkubwa” na “uhakika kwenye mfumo wa kuimarisha uchumi ni jambo la lazima ili kuwa na uwekezaji na maamuzi ya muda mrefu katika soko na kwa walaji” (KAS 2009, uk. 4-5). Hili linahusisha mipango mizuri ya sera za fedha ambayo haina mtazamo kwenye mipango ya kiuchumi ya muda mfupi pekee. Vipengele vifuatavyo ni muhimu ili kuleta uendelevu na mafanikio katika utaratibu wa fedha:

- **Linda uhuru wa sera ya fedha**

  Maamuzi kuhusu fedha lazima yakasimiwe kwa benki kuu, ambayo uhuru wake unapaswa kulindwa. Benki Kuu ya Tanzania – ilianzishwa mwaka 1965 kulingana na Sheria ya Benki ya Tanzania. Benki Kuu inalenga kulinda uimara wa bei za bidhaa nchini (Nord et al. 2009, uk. 42).

  Katika kipindi cha miaka kumi, Benki Kuu imekua na uhuru zaidi, lakini imebaki kuwa na changamoto ya kuweza kuingiliwa na maamuzi ya kisiasa. Sheria ya Benki ya Tanzania imefanyiwa

mabadiliko mwaka 1995 na 2006 ili kuleta ufanisi na uhuru wa sera ya fedha nje ya nguvu za kisiasa. Hata hivyo, serikali huteua watendaji wa Benki Kuu, hivyo kuwa na nguvu ya udhibiti katika utendaji wake wa kazi. Miongozo na maamuzi ya juu ya benki kuu hutolewa na Bodi ya Wakurugenzi. (BOTA 2006, 9(1)) Muundo wa bodi hii huamuliwa na serikali. Gavana wa Benki Kuu, ambaye huongoza Bodi ya Wakurugenzi, anateuliwa moja kwa moja na Rais, pamoja na magavana wasaidizi watatu. Wote wanaweza kuteuliwa tena baada ya vipindi vyao kuisha (BOTA 2006, 8(1)-(3)) na Rais wa nchi ndiye mwamuzi wa viwango vyao vya mishahara na posho zao za kustaafu, ambapo utaratibu kupitia nyenzo zilizopo unamruhusu kutekeleza (BOTA 2006, 14(1)). Kwahiyo, Rais wa nchi ana udhibiti wa nusu ya wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu. Pia, wajumbe wengine wanne, ambao si Wakurugenzi wakuu, wanateuliwa na Waziri husika, ambaye pia ameteuliwa na Rais wa nchi (BOTA 2006, 9(4)).

Ili kuongeza ufanisi wa Benki Kuu, inashauriwa kwamba serikali itoe uhuru zaidi kwa Benki Kuu kufanya shughuli zake. Ili kufikia hilo, viongozi wa benki kuu wanaweza wakatokana na wataalamu ambao nafasi zao zinatangazwa na kushindaniwa kwa uwazi na baadaye wakapendekezwa. Inashauriwa Rais afanye uteuzi baada ya mapendekezo na tathmini ya bunge. Hata kuondolewa kwao kazini kunaweza kufuata utaratibu huohuo.

- **Linda uimara wa uchumi mkubwa**
  Tanzania ilijiunga na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwezi Septemba mwaka 1962. Mpaka sasa, jumla ya nchi wanachama wa IMF ni 189. Shirika lilianzishwa mwaka 1944 katika Mkutano wa Bretton Woods, shirika linalenga katika kuimarisha ushirikiano wa kifedha wa kimataifa na kuhakikisha masuala ya fedha yanakua imara ili kufikia ukuaji endelevu wa kiuchumi duniani (IMF n.d.). Kuimarishwa kwa uchumi mkubwa kumeendelea kusisitizwa na Shirika la Fedha Duniani na Jumuiya ya Ulaya. Vigezo vya Maastricht vimeweka viashiria vitano vinavyotumika kupima uimara huo: a) viwango vidogo vya mfumuko wa bei, b)

viwango vidogo vya riba ya muda mrefu, c) kiwango kidogo cha deni la taifa, d) kiwango kidogo cha upungufu katika bajeti ya serikali, na e) sarafu imara (Afxentiou 2000).

Serikali inatakiwa kuhakikisha uwepo wa kiwango kidogo na imara cha mfumuko wa bei ambacho kinawakilisha uhitaji mkubwa wa bidhaa kwenye soko, mbali na uwepo wa mfumuko mkubwa wa bei na usio imara, ambao unahatarisha ukuaji wa uchumi na sekta ya kifedha. Pia, inaweza kupelekea athari kwenye mapato ya serikali na madeni kwa wadau kwenye uchumi. Kutokana na vigezo vya Maastricht, mfumuko wa bei vyema uwe 3% (The Reut Institute 2006). Kiwango kidogo cha mfumuko wa bei pia kinawakilisha uchumi ulio imara na kuonyesha mwelekeo mzuri kama hakitabadilika. Mabadiliko katika viwango vya riba katika kipindi kirefu kunaweza kupelekea mabadiliko ya mfumuko wa bei. Vigezo vya Maastricht vimeweka viwango vya riba vya muda mrefu kwenye ukomo wa 9%. Kiwango kidogo cha deni la taifa ikilinganishwa na pato la taifa kinaruhusu serikali kutumia mapato ya kodi kushughulikia mahitaji ya ndani, mbali na kulipa mikopo ya nje. Pia, kiwango kidogo cha deni la taifa kinaleta utulivu wa kifedha kipindi cha misukosuko. Vigezo vya Maastricht vimewekewa ukomo wa deni la taifa mpaka 60% ya pato la taifa. Wakati huo huo, kiwango kidogo cha upungufu kwenye bajeti ya serikali kunapunguza uwezekano wa deni la taifa kuongezeka. Kwahiyo, upungufu wa pato la taifa umewekewa ukomo wa 3% kwenye vigezo vya Maastricht. Mwisho, uimara wa sarafu unawezesha maendeleo ya mikakati ya muda mrefu katika ukuaji wa biashara ya kimataifa. Pia, inapunguza hatari mbalimbali katika soko la kubadilishana fedha na hupunguza hatari ya madeni ambayo yapo kwenye fedha za kigeni. Katika suala la uimara wa sarafu, vigezo vya Maastricht vimeruhusu mabadiliko yenye ukomo wa juu wa 2.5% (The Reut Institute 2006).

Kulingana na malengo yaliyofafanuliwa hapo juu, kwa Tanzania, Benki Kuu ndiyo inawajibika kuyatimiza hayo. Lengo lake kuu ni kuhakikisha bei ya bidhaa inakua imara. Kuna kauli ya Benki isemayo: “uzoefu unapendekeza kanuni moja muhimu:

Benki Kuu iliyo na mambo mengi ya kufanya inaweza isiweze kufanya hayo yote kwa ufanisi. Hii inafanana na kile ambacho kilitokea kwa Benki Kuu ya Tanzania, ambapo haikufanikiwa kufikia malengo yake mengi ya kisera" (BoT n.d.). Kubadilika kutoka katika malengo mengi ya kisera kwenda kwenye lengo moja la kisera kumeonekana kwenye sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 na sheria iliyotangulia kabla ya Benki Kuu ya mwaka 1995. Kutokana na sheria hiyo, "lengo kuu la Benki itakua ni kutengeneza, kutafsiri na kutekeleza sera za fedha, inayopelekea lengo la uchumi la kudumisha uimara wa bei ya bidhaa, ambayo inakua rafiki kwa uwiano mzuri na ukuaji endelevu wa uchumi wa taifa la Tanzania" (BoT n.d.). Kwahiyo, Benki Kuu inasema "Benki inaweka nguvu zake pamoja katika kufikia bei imara ya bidhaa na kutangaza kuwa mfumuko wa bei ni adui wa kwanza" (BoT n.d.). Kutokana na taarifa za Benki Kuu hii inamaanisha kwanza "kiwango cha mfumuko wa bei (...) kinapaswa kuwa kidogo kadiri inavyowezekana, kwa ukomo wa muda mrefu wastani wa kiwango uwe kati ya 0-5% (kulingana na mabadiliko ya asilimia ya mwaka uliopita)" (BoT n.d.).

Kama ilivyoelezwa kwenye kifungu cha 3.2.1, Tanzania imekua na mfumuko wa bei imara wa kiasi kinachokaribia 5%, na uimara kwenye viwango vya riba ya 14-16% mpaka hivi karibuni. (Focus Economics 2017). Kwahiyo mpaka sasa, benki imeweza kufikia malengo yake makuu, hatua ambayo ni muhimu kwa uimara wa kifedha. Hata hivyo, uhuru zaidi unahitajika ili kufanya uongozi wa benki uwe na nguvu na wenye ufanisi. Benki kuu lazima iwe huru na kutoingiliwa na maamuzi mengine ya kiserikali ili itekeleze majukumu yake ya msingi. Taasisi za uratibu wa kibenki lazima zizuie kudorora kwa soko la mtaji duniani na kuepusha madhara yanayoweza kutokea kwenye soko la ndani ya nchi. Pia, masoko ya mitaji, benki za kibiashara na taasisi nyingine za kifedha au ushirika, vinahitaji kuwezeshwa ili viweze kutoa fedha kwa wale wanaotaka kuanzisha biashara na shughuli nyingine za uchumi ambazo ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi.

#### *4.3.4 Utaratibu wa Biashara*

Sokoni wadau huonana na kufanya biashara, katika hilo hubadilishana bidhaa na huduma ili kupata faida. Njia nyingi “zimewekwa katika miongozo tofauti ya sheria za biashara, ikiwa ni pamoja na makampuni ya wanahisa, makampuni binafsi, makampuni ya serikali na ushirika” (Benecke 2008, uk. 17). Wajibu wa serikali ni kuweka mazingira rafiki ya ushindani na makampuni ya kibiashara yanapaswa kushindana kwa haki. Taratibu za kisheria, kwa mfano mambo yanayohusu madeni, kamati za wafanyakazi, kodi na taarifa za wajibu zinapaswa kuwekwa wazi na kufahamika vizuri (Benecke 2008, uk. 17). Inaaminika kwamba, uwepo wa biashara za wazawa kwenye soko la kitaifa na kimataifa kuna mchango mkubwa kwenye mafanikio na uendelevu wa uchumi katika nchi.

- **Kuimarisha sekta binafsi Tanzania**

  Sekta binafsi nchini bado ni changa na ni makampuni machache tu ya watanzania ambayo yanaweza kushiriki kikamilifu kwenye biashara za kimataifa. Nchi inatakiwa kuhakikisha mazingira ya kibiashara yanahamasisha ustawi wa sekta binafsi; hii inahusisha uwepo wa mazingira mazuri katika michakato ya usajili wa biashara, utolewaji wa leseni, mifumo ya kodi n.k. Hata hivyo, wadau wengi wametambua umuhimu wa kuimarisha sekta binafsi.

  Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) na Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania (CTI) wamejitolea kuendeleza sekta binafsi nchini. Hizi ni asasi za biashara ambazo zinaamini katika “maendeleo ya kiuchumi nchini yakiongozwa na sekta binafsi” (TPSF, n.d.), ambayo yanaweza kufikiwa kama nchi itaweka mazingira mazuri na rafiki ya biashara. Kwa upande mwingine, taasisi hizi zinatoa utetezi wa sekta binafsi na kuijulisha serikali kuhusu mahitaji ya sekta binafsi nchini na maeneo ya vipaumbele ambayo wanapaswa kuyashughulikia. Kwa upande mwingine, taasisi hizi zinatoa taarifa kwa wajasiriamali binafsi na wawekezaji ili wapate majibu na kuweza kukabiliana na hali ya mazingira ya kibiashara (CTI 2016b).

Pia, kuna Taasisi ya Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) ambayo imeanzishwa mwaka 1988 katika mtazamo wa uhuru wa kibiashara Tanzania chini ya awamu ya Ali Hassan Mwinyi ili kuwezesha maendeleo ya sekta binafsi imara na kuhamasisha ushiriki wa nchi katika biashara ya kimataifa. Taasisi ya TCCIA ina uwakilishi nchi nzima kupitia ofisi za mikoa na vituo vya wilaya na inashiriki maonyesho mengi ya kimataifa. Katika ngazi ya kitaifa, mkoa na wilaya, TCCIA wanatoa uwakilishi na huduma ya utetezi kwa wanachama wake na kutoa taarifa kwa wajasiliamali kuhusu haki zao (TCCIA 2016a). Miongozo na sera kuu ya TCCIA inaundwa na wawakilishi karibu 150 wa sekta tofauti na wafanyabiashara kutoka mikoani ambao hushiriki Mkutano Mkuu wa kila mwaka. Maazimio ya sera huongozwa na Halmashauri Kuu ya Kitaifa ambayo huweka mikakati yote pamoja kama ilivyopendekezwa na Wakurugenzi tayari kwa ajili ya kuifanyia kazi. Bodi ya Wakurugenzi wanawajibika kutekeleza na kufanikisha malengo ya TCCIA (TCCIA 2016b).

Serikali ya Tanzania pia inatambua umuhimu wa ubinafsishaji kwenye uchumi. Kwa mfano, mwaka 1992 Serikali ya Tanzania ilianzisha Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) (TANESCO 2017). Tume hii ililenga kuleta hamasa ya ubinafsishaji wa mashirika ya umma, ili kuongeza ufanisi. Pia mwaka 2001, Rais wa Tanzania wa kipindi hicho, Benjamin Mkapa, aliunda Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) ili kukuza majadiliano kati ya sekta binafsi na ya umma kuendeleza uchumi ulio imara na kuimarisha sekta binafsi nchini. Baraza linaundwa na wanachama 40; kati ya hao 20 ni kutoka sekta ya umma (kutoka serikalini) na 20 kutoka sekta binafsi. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwenyekiti wa Baraza (TNBC) (2015).

Kwahiyo, inaonekana miundo mingi ipo tayari nchini Tanzania ambayo inaweza kuruhusu maendeleo ya uchumi imara ikiambatana na mazingira rafiki ya kuwajenga wajasiriamali. Hata hivyo, matokeo ya moja kwa moja ya warsha na majadiliano mbalimbali bado hayajaonekana. Katika ripoti ya ufanyaji biashara ya 2018 iliyotolewa na Benki ya Dunia, Tanzania ilikua

nchi ya 137 kati ya 190 na ilishuka alama 5 ikilinganishwa na mwaka 2017 (World Bank Group 2018a, uk. 4). Mbali na ukweli kwamba taasisi nyingi za wajasiriamali zinafuata mrengo huo, wanakosa utaratibu mzuri na hawajaweza kuunda jumuiya itayokua na sauti kuweza kuwa na ushawishi kwenye vyombo vya maamuzi ili kuimarisha sekta binafsi na mazingira ya biashara.

Mbali na hayo, sekta muhimu zinaendelea kuwa chini ya umma, kama mifano ifuatayo inavyoonyesha:

- **Kampuni ya Reli Tanzania (TRL)** ni moja kati ya mifumo miwili ya reli nchini. Mtangulizi alikua Shirika la Reli Tanzania (TRC), ambalo lilianzishwa mwaka 1977 na kumilikiwa na serikali. Mwaka 2007, shirika la TRC lilibadilishwa na kuwa kampuni ya TRL. Mabadiliko yaliyofanyika yalikua sehemu ya sera ya kiuchumi, ambazo zilipendekeza ubinafsishaji wa uchumi wa Tanzania na kubinafsisha mashirika mengi. Kwahiyo, TRL ilikua ni kampuni binafsi, ambayo ilikua na umiliki wa wabia wakubwa wawili: kampuni ya India ya RITES Ltd. (51%) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (49%). Hata hivyo, mwaka 2011, Serikali ya Tanzania ilichukua hisa zote na kufanya TRL kuwa shirika linalomilikiwa na umma chini ya Wizara ya Usafirishaji kama ilivyokua kwa TRC (TRL 2015).

- **Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)** ni moja kati ya makampuni ya simu nchini Tanzania. Toka mwaka 2001, TTCL ilikua chini ya utaratibu wa hisa, ambapo mwongozo wa mkataba kati ya serikali (mmiliki mkuu) na wawekezaji binafsi uliwekwa. Ndani ya mwaka 2001, Serikali ya Tanzania ilikuwa ikimiliki 65% ya TTCL na wengine waliobaki waligawanyika katika makundi mawili ya wanahisa: Ushirika wa DETECON wa Ujerumani na kampuni ya Uholanzi ya Mobile Systems International Cellular Investments Holdings BV (MSI). Makubaliano haya hayakurejewa upya mwaka 2016 na Serikali ilitangaza makubaliano ya uhamisho wa hisa, ambayo yalifanya ubia na makampuni binafsi ufike

mwisho. Baada ya hapo, TTCL ikawa kampuni inayomilikiwa na serikali (TTCL 2017).

- **Kuanzisha na kukuza biashara ndogondogo na za kati (SMEs)**
  Katika ripoti ya Benki ya Dunia ya ufanyaji wa biashara ya mwaka 2018, Tanzania ilishika nafasi mbaya duniani – na kuwa ya 162 kati ya 190 – katika eneo la kuanzisha biashara (World Bank Group 2018a). Hata hivyo, ili kuimarisha sekta binafsi nchini, wafanya maamuzi wanapaswa kurahisisha uanzishwaji wa biashara ndogo na za kati (SMEs). SMEs, mara nyingi humilikiwa na familia, wana sehemu muhimu katika mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii, na wana mchango mkubwa katika suala la ubunifu na wanashiriki vizuri katika uzalishaji wa bidhaa na huduma (Benecke 2008, uk. 17). SMEs wanaweza kupewa tafsiri kulinga na idadi ya waajiriwa, kwa mfano biashara zenye wafanyakazi chini ya 250 ni zile za kati na zile zenye wafanyakazi chini ya 50 ni zile ndogo, na tafsiri nyingine inaweza husu mapato au mauzo (European Commission 2018).[3] Kulingana na umuhimu mkubwa kwenye uchumi na faida kwenye jamii, msaada wa serikali kwenye biashara za aina hii ni wenye umuhimu mkubwa kwenye maeneo ya, kwa mfano, punguzo la kodi na msaada wa ushauri kwenye masuala ya kisheria, utawala, teknolojia na huduma za mikopo (Benecke 2008, uk. 17).

  Kwanza kabisa, wajasiriamali wapya wanahitaji kujua mfumo wa ujumla wa kisheria ili waweze kupanga mipango yao kwa wakati. Kwa sasa Tanzania, jambo hili ambalo ni la msingi lina changamoto na mkanganyiko. Mfumo wa uwekezaji na kodi haueleweki vizuri. Haya yanaweza kuwakatisha tamaa wawekezaji na wajasiriamali kujenga miradi ndani ya nchi na kupunguza kasi ya maendeleo ya uchumi. Kwahiyo ni muhimu kurekebisha mifumo ili ieleweke na kuweka pamoja mfumo wa uwekezaji na kodi na kutoa taarifa zinazojitosheleza kwa wadau.

3 Kwa kuongezea, OECD wamesema: "Namba hii hutofautiana kati ya nchi na nchi. Mara nyingi ukomo wa tarakimu kubwa kabisa kwa SME ni waajiriwa 250, kama ilivyo kwa Jumuiya ya Ulaya. Ingawa, baadhi ya nchi wameweka ukomo wa waajiriwa 200, ambapo Marekani wamewekwa kwa SMEs ihusishe biashara na kampuni zenye waajiriwa pungufu ya 500. Kampuni ndogo kwa ujumla ni zile zenye waajiriwa pungufu ya 50, na biashara ndogo zina waajiriwa wasiozidi 10, na kwa baadhi ya maeneo ni waajiriwa wa 5." (OECD 2005, uk. 17).

Uwazi na uimara ni mambo ya muhimu ya kusaidia ufanyikaji wa maamuzi ili kustawisha soko. Hata hivyo, uwazi wa mfumo wa kodi sio jambo pekee linalopaswa kuzingatiwa. Inahitajika pia kushughulikia changamoto mbalimbali za kijamii na kiuchumi. Wadau kwenye biashara hawapaswi kuhisi kwamba watakumbana na utitiri wa kodi na tozo mbalimbali maana ukubwa na wingi wa kodi unahatarisha uwezo wa kuanzisha na kukuza biashara.

Kwa Tanzania, badala ya kuhamasishwa na kutiwa moyo, wajasiriamali wanalipa kodi na tozo kubwa na nyingi hata kabla ya kuanza biashara. Kwahiyo, mjasiriamali mpya anahitaji kiasi kikubwa cha mtaji ili kuanza kufanya shughuli ya kiuchumi – na watanzania wengi hawana mitaji ya uhakika – na ili wafanikiwe lazima wawe na uhakika wa kupata faida kubwa na kwa haraka katika biashara wanazoanzisha. Lakini katika mtazamo tofauti, falsafa ya Uchumi Jamii inalenga kuiwezesha sekta binafsi, ikiwa ni pamoja na SMEs, lakini pia katika uanzishwaji wa makampuni mapya.

Imependekezwa kwamba njia tofauti za kusaidia zinapaswa kuandaliwa na kugawiwa kwa walengwa ili kujenga SMEs. Kodi na tozo zikusanywe baada ya wafanyabiashara kuanza shughuli ya uchumi na kuanza kupata kipato na si kabla, kwa mfano, msaada wa kifedha kutoka serikalini na kufikiwa na programu maalumu na taasisi katika kipindi cha mwanzo cha kuanza biashara itawezesha wadau wenye vigezo wapate mtaji wa kutosha wa kuanzisha biashara na kufikia hatua ya kuhimili ushindani na kujitegemea. Ili kuongeza uwezekano wa kufanikiwa, misaada ya kifedha inaweza kwenda sambamba na utolewaji wa mafunzo kwa wajasiriamali, kuwafundisha masuala ya utawala, masoko na ujuzi wa kutunza taarifa za fedha. Hatua hizi zina gharama, lakini zinapaswa kuangaliwa kama uwekezaji wa muda mrefu. Baada ya kipindi kifupi cha kuendeleza biashara, SMEs wana nafasi ya kujitegemea na kuwa walipa kodi muhimu. Pia, SMEs wanaboresha uchumi wa nchi kwa kuchangia kwenye uzalishaji na kuongeza ajira zenye faida kubwa kwa taifa na jamii kwa ujumla. Kwahiyo, kwa

kuwezesha biashara zinazofaa, serikali inaweza kuwa na ustawi wa kudumu na kupunguza wimbi la ukosefu wa ajira.

Ila, motisha hizo lazima ziwe kwenye utaratibu na usimamizi maalumu. Serikali na taasisi za umma haziwezi kusaidia mradi bila ya kufanya uchambuzi wa hatari zinazotegemewa na kujua uwezekano wa kufanikiwa kwa maana umakini usipokuwepo inaweza pelekea hasara kwa taasisi za umma na kwenda kinyume na dhana ya uwajibikaji wa kila mmoja. Kwahiyo, walengwa wa hizo ruzuku wanapaswa kukidhi vigezo vilivyoandaliwa vizuri na kujenga mawazo yao ya kibiashara kwa kuzingatia tathimini za hali halisi, soko na mpango wa bajeti ya biashara husika. Katika kipindi cha uwezeshwaji wa mradi, mjasiriamali anapaswa kufuatiliwa katika vipindi tofauti vya utekelezaji ili kujiridhisha na maendeleo yake katika biashara.

- **Kuhakikisha ushirikishwaji wa wadau wote katika kuandaa taratibu za kufanikisha biashara na ajira**

**Chama cha Waajiri Tanzania (ATE)** ndio taasisi kuu inayohusika na masuala ya waajiri Tanzania. Chama hiki kilianzishwa mwaka 1960 ili kulinda maslahi ya waajiri. Hivi karibuni, chama kimekua na wanachama 1,400 waliosajiliwa moja kwa moja na wanachama 6,000 ambao si wa moja kwa moja. Waajiri wote Tanzania wanaweza kuwa wanachama wa ATE, ila ukweli ni kwamba karibu 70% ya waajiri wanaishi na kufanya shughuli zao Dar es Salaam. ATE inatoa taarifa kuhusu haki, mwongozo wa kisheria na ushauri kwa wanachama kuhusu mambo yanayojitokeza kupitia warsha na vikao mbalimbali. ATE pia inawakilisha wanachama wake kwenye majadiliano na serikali na taasisi za umma (ATE 2018).

**Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA)** ni taasisi inayofanyakazi kama mwamvuli wa kuviweka pamoja vyama vya wafanyakazi upande wa Tanzania bara. Shirikisho hili lilianzishwa mwaka 2000 na lina wanachama 320,000 (Revolvy n.d. a). Shirikisho la vyama vya wafanyakazi kwa Zanzibar linajitegemea nje ya TUCTA na lilianzishwa mwaka 2002 na linaitwa **Shirikisho la Vyama vya Wanyakazi Zanzibar (ZATUC)**.

Mashirikisho yote mawili yanafungamana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi la Kimataifa (Revolvy n.d. b).

Ushirikiano imara na unaoweza kufika mbali kati ya taasisi kutoka sekta binafsi, waajiri, waajiriwa na taasisi za kisiasa ni ule unaoruhusu wadau wote kuelewana na kutafuta suluhu ya matatizo pamoja ili kukidhi hitaji la uchumi wa nchi. Mashirika mengi yamekua yakitaka mabadiliko ya taratibu na kuondolewa kwa vikwazo kuwezesha ujasiriamali. Ingawa, taasisi hizi hazijaweza kutoa uzito katika mijadala ya kisiasa. Majadiliano ya mara kwa mara yenye mtazamo mzuri kati ya wawekezaji, wajasiriamali na watunga sheria ni muhimu sana ili kuwa na mfumo wenye ufanisi.

### *4.3.5 Utaratibu wa Ushindani*

Benecke amesisitiza: "Kiwango cha ushindani ni matokeo ya mchakato wa soko, lakini taratibu za mfumo wa ushindani zinawekwa na serikali. Serikali inaweza kuingilia kwenye matukio maalumu kama kuleta uwiano wa nguvu sokoni, usalama wa kibiashara na kwenye jambo lenye maslahi kwa umma. Kwa ujumla, ushindani unapaswa uwe huru kwa kadiri inavyowezekana ili kuimarisha shauku ya kufikia malengo, hata hivyo unatakiwa kudhibitiwa ili kuzuia athari mbaya kwa jamii na mazingira" (Benecke 2008, uk. 17).

Chini ya Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uchumi wa Tanzania ulikuwa ni ule uliokua ukitegemea mipango na kuratibiwa na serikali kuu kwa kiasi kikubwa. Itikadi yake maarufu ya Ujamaa ilithamini tunu za amani na umoja kwenye jamii ya watanzania, lakini hakukuwa na ushindani katika soko, kwa kuwa kulikuwa na juhudi ndogo ya kuhamasisha sekta binafsi. Kwahiyo, kuanzia mwaka 1985 serikali mpya ya Rais Ali Hassan Mwinyi ilibadili sera za uchumi kuelekea biashara huru, kuanzia miaka ya 1990, juhudi ziliwekwa kuanzisha mifumo inayofaa kuwezesha ubinafsishaji. **Hata hivyo mwelekeo huo**, haukuzingatia uwekezaji wa wazawa katika sekta binafsi na kuleta teknolojia ili kukuza ushindani katika uchumi, jambo ambalo linachukuliwa kuwa ni msingi wa maendeleo ya uchumi

jumuishi. Sekta binafsi iliyo rasmi ambayo imeendelezwa mpaka sasa haijaunganishwa moja kwa moja na mipango ya maendeleo ya kitaifa.

Utaratibu mpya wa ushindani ndani ya Tanzania unajijenga katika mikakati ifuatayo:

- **Kukuza ushindani na masoko huria**
  Taswira ya ujumla ya mashirika ya umma[4] inaonyesha kwamba Tanzania iko mbali katika uelekeo wa kufikia uchumi wa soko huria, kwa sababu serikali bado inadhibiti sekta zote muhimu hali inayosababisha sekta binafsi kutozalisha kwa ufanisi. Hili lingeweza kuwa kwa ajili ya kusimamia ubora na upatikanaji wa huduma muhimu kwa jamii, usimamizi usio mzuri wa uongozi kwa baadhi ya mashirika ya umma unatishia uendelevu wa uchumi, kwa mfano Shirika la Umeme la Tanzania (TANESCO), na kwahiyo, inaweza kuathiri ufanisi wa utolewaji wa baadhi ya huduma kwa baadaye. Kukosekana kwa ushindani na hasara za kifedha hakuleti si tu motisha bali pia rasilimali za kuwekeza kwenye tafiti au miundombinu mipya, ambayo italeta mafanikio na ubora wa huduma.

  **Shirika la Umeme la Tanzania (TANESCO)** ni shirika la umma la kuzalisha na kusambaza nishati ya umeme. TANESCO ilianzishwa mwaka 1964 likiwa na hisa za serikali na makampuni binafsi (Tsakhara 2015, uk. 3). Mwaka 1975, serikali ya Tanzania iliamua kununua hisa zote na TANESCO ikawa inamilikiwa rasmi na umma chini ya Wizara ya Nishati na Madini. Mpaka mwaka 1992, TANESCO imekua ndio taasisi pekee ya kuzalisha na kusambaza nishati ya umeme. TANESCO bado inashikilia sehemu kubwa ya shughuli za nishati kwa Tanzania bara. Shirika linasimamia mchakato wote kuanzia uzalishaji wa nishati ya umeme mpaka usambazaji na kuuza nishati kwa Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) (TANESCO 2017). Serikali pia bado inamiliki hisa zote za kampuni na inaweza kuingilia maamuzi kuhusu upangaji wa bei na kwenye uandaaji wa mpango mkakati. Mwisho wa mwaka 2016, kwa

4 Angalia kiambatanisho Na. 1

mfano, mwongozo wa TANESCO uliamua kupandisha bei kwa 8.53% (Ng'wanakilala 2017). Siku mbili baadaye, kiongozi mkuu wa shirika aliondolewa, na ongezeko la bei liliondolewa, kwa sababu serikali kuu ilitazamia kwamba maamuzi haya yangeweza kuingilia sera ya maendeleo. Kuingilia huko kisiasa kunaweza kupelekea hasara na kudumaza uwezo wa kifedha wa shirika. Mbali na mwelekeo rasmi wa uhuru na ubinafsishaji, sekta ya nishati kwa sehemu kubwa inasimamiwa na serikali, ambapo inaleta athari hasi kwenye ufanisi na kufikia malengo ya sekta hii muhimu kwenye uchumi.

Sera ya soko huria, kitaifa na kimataifa na upangaji huru wa bei za bidhaa ina mchango kwenye kuimarisha ushindani na kuboresha matumizi bora ya rasilimali chache zilizopo na kukuza maendeleo.

Wakati huo huo, ruzuku kwenye "baadhi ya bidhaa katika kipindi na mazingira fulani" (Benecke 2008, uk. 17) zinaweza kuzingatiwa. Kwa Tanzania kuna kitu kinachoitwa "**Bodi**". Taasisi hizi zina ushawishi katika uzalishaji viwandani na zina lengo la kuimarisha ushindani na kusimamia ubora wa uzalishaji wa bidhaa katika sekta husika. Bodi hizi kwa Tanzania zipo kisheria, zimepewa mamlaka na Bunge la Jamhuri ya Muungano. Kwa mfano, Bodi ya Pamba Tanzania ilianzishwa na Sheria ya Bunge Na. 2 ya mwaka 2001 (TCB 2016) na Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) iko chini ya Sheria Na. 18 ya mwaka 2009. Bodi hizi za mazao zinatekeleza majukumu yake kwa niaba ya serikali katika sekta fulani (CBT 2016). Bodi huwa zinapanga bei ya zao na kiasi cha uzalishaji. Utekelezaji wa Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii unamaana kuong'olewa kwa usimamizi wa bei – na kwahiyo kuziondoa au kuzibadili bodi hizi – kwa kadiri inavyowezekana na kuruhusu kanuni ya nguvu ya soko kuamua hali ya soko. Baadhi ya tofauti zinazoweza kujitokeza zinaweza kupokelewa kama usimamizi ni muhimu kuweza kuleta malipo mazuri kwa wazalishaji au kuwezesha mahitaji ya msingi kwa walaji, lakini ni hali ya kipindi kifupi na cha mpito. Baada ya kipindi fulani, eneo la kisekta litakuza tija na mfumo wa ushindani kuruhusu uzalishaji unaoendana na mahitaji ya soko.

- **Kufuatilia masoko ili kuwa na ushindani wa haki**
  Ushindani wa haki ni nguzo ya Uchumi Jamii, mfumo pia unahitaji "serikali na jumuiya ya kimataifa kusimamia umiliki na nguvu ya soko" (KAS 2009, uk. 4) mfano kuondoa hali ya kuwa na mzalishaji mmoja wa bidhaa. Mwaka 2003, Sheria ya Ushindani (FCA) ilianzishwa ikiwa na lengo la kuzuia hali ya wadau kutawala soko (FCA 2003, Kifungu 5(6)) na matumizi mabaya ya hali hiyo (FCA 2003, Kifungu 10). Ili kufikia lengo hilo, Tume ya Ushindani ilianzishwa (FCA 2003, Kifungu 62(1)). Tume ya Ushindani (FCC) ni taasisi ya umma, ambayo inalenga kuweka mfumo imara wa soko huru kwa kuhakikisha ushindani wenye ufanisi kwa wadau wote kwenye biashara (FCC 2015a). Tume inawajibika kupambana na mienendo isiyo ya haki na isiyofaa kwenye soko. Kwa kupunguza matendo yaliyo nje ya ushindani, FCC inachangia kwenye maendeleo ya nchi (FCC 2015a). Haki ya ushindani inapelekea kuongeza ufanisi, uzalishaji na uwekezaji, na mwisho kuboresha utolewaji wa bidhaa na huduma. Kulingana na sheria, FCC inaweza kuzuia hali ya wadau kutawala soko, hasa kwa kupunguza nguvu za wadau kuungana (FCC 2015b). Tume inaweza kufanya uchunguzi na kuchukua hatua za hali hizo zisizohitajika sokoni. Kutokana na FCA "Tume itakua huru na kutekeleza majukumu na mamlaka yake bila kuingiliwa kwa uhuru na bila woga" (FCA 2003, Kifungu 62(2)). Ingawa, wajumbe wote wanachaguliwa na Kwahiyo wanategemea wafanya maamuzi wa kisiasa. Mwenyekiti wa FCC anateuliwa na Rais wa Tanzania kwa kipindi cha miaka minne (FCA 2003, Kifungu 63(3)) na wajumbe wengine, akiwepo Mkurugenzi Mkuu, wanateuliwa na Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji (FCA 2003, Kifungu 63(4)). Wajumbe wote wa Tume wanaweza kutumika kwa vipindi viwili (FCA 2003, Kifungu 63(8)) na posho zao zinaamuliwa na Rais na Waziri (FCA 2003, Kifungu 63(9)). Tume inaweza kuwa chombo chenye nguvu, ingawa, ili iweze kutekeleza majukumu yake vizuri, Tume inahitaji iwe huru na isiingiliwe na mamlaka kutoka nje au ushawishi wa kisiasa.

  Ingawa nguvu ya soko lazima idhibitiwe, ushirikiano wa wafanyabiashara ngazi ya chini lazima uruhusiwe, kwa

kadiri inavyowezekana, ili kufanya wadau washindane kwa kiwango cha juu na kuimarisha maendeleo ya asili ya kijamii na kiuchumi. Hiki ndicho kinachopaswa kufanywa na ushirika (Benecke 2008, uk. 18) na ni muhimu hasa kwenye sekta ya kilimo nchini Tanzania. Mkakati huo unaruhusu, kwa mfano, "wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa kuondoa ushindani kwa kuanzisha umoja ambao unawaruhusu wao kushindana na wakulima wakubwa" (Benecke 2008, uk. 18).

- **Kutoa taarifa za masoko kwa uwazi kwa wadau wote**

  **Vyombo imara na huru vya habari na vinavyojitegemea** ni muhimu vikawepo kulingana na miiko na miongozo ya SMET. Uhuru wa kuongea na uhuru wa mtu mmoja mmoja unalindwa na kutunzwa. Uhuru wa vyombo vya habari una thamani katika kuelekea kwenye maendeleo. Kama jukwaa kwa ajili ya uhuru wa kujieleza, kusambaza mawazo tofauti na sehemu ya kubadilishana mawazo, chombo cha habari kinakuza uelewa baina ya watu. Utangazaji wa mijadala au mipango pamoja na mawazo ya waandishi wa habari kuhusu hali ya kiuchumi, kijamii na kimazingira unaruhusu watu kuhoji, kuchukua nafasi na kutafuta suluhu. Vyombo vya habari pia ni njia muhimu ya kuujulisha umma na kufikia malengo ya kufikisha ujuzi na uwazi wa taarifa kwa washiriki wote wa soko. Taarifa kuhusu habari mpya, matokeo ya utafiti, sera za umma, hali ya kiuchumi, mafanikio ya mipango ya mtu na matukio ya kimataifa vinapaswa kuwasilishwa kwa uhuru kwa wadau wote kwa gharama nafuu. Vyombo vya habari, pamoja na taasisi za walaji na wazalishaji, wanapaswa kuandaa programu ya kuhabarisha, kufundisha au kuonya wadau wa soko. Kama watu watapata taarifa vizuri kuhusu bidhaa, huduma, michakato, vyanzo vya fedha na fursa nyingine, wataweza kushiriki vizuri kwenye shughuli za kiuchumi.

  Ingawa uhusiano unaweza usiwe wa dhahiri, uhuru wa vyombo vya habari na mtazamo wa serikali kuhusu vyombo hivyo una athari katika masoko. Masoko yanategemea hali shwari na hayawezi kufanya kazi bila kujiamini. Wawekezaji na

makampuni wanaweza wasiwekeze nchini kama hawana imani na serikali au mfumo uliopo. Uwekezaji unahitaji kuegemea katika uwezo wa serikali kutoa taarifa kuhusu maamuzi na changamoto ambazo zinaweza kuathiri uchumi na uwezo wa kulinda uhuru na usalama wa watu. Sheria ya sasa ya vyombo vya habari ya Tanzania inapaswa kuwekwa kwenye usawa ili kusaidia Uchumi Jamii kwa ajili ya kulinda uhuru wa kujieleza ambao pia unalindwa na Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kifungu 1 (URT 1977).

#### *4.3.6 Utaratibu wa Kimataifa*

Ili kuimarisha maendeleo jumuishi ya uchumi, Tanzania inapaswa kujenga uwezo wake kwa kutumia uhusiano wa kikanda na kimataifa, kama ambavyo Ujerumani ilifanya katika kutekeleza Mpango wa Marshall wa Marekani baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia (Haase/Schneider/Weigelt 2008, uk. 395). Washirika wengi wa nchi wako tayari kutoa msaada wa kifedha na kitaalamu. **Kikundi cha Benki ya Dunia** kilianzisha “Mkakati wa Kusaidia Nchi (2012-15)” kwa ajili ya Tanzania, ambao bado unaendelea. Taasisi hii imeainisha maeneo makuu manne ya kiutekelezaji nchini: kujenga uwezo wa rasilimali watu na usalama wa kijamii, ukuaji endelevu wa kiuchumi na jumuishi unaozingatia uwepo wa sekta binafsi imara, kukuza utendaji wa utawala bora na maendeleo ya miundombinu na huduma za umma. Benki ya Dunia inatoa msaada wa kifedha na ujuzi kwa taasisi za kitanzania (World Bank Group 2017b). Katika safari yake kuelekea maendeleo yanayoongozwa na sekta binafsi pamoja na masoko huru, Tanzania pia inasaidiwa na **Shirika la Biashara Duniani (WTO)** (WTO 2018). Tanzania ilikua mwanachama wa Mkataba wa Kimataifa kuhusu Forodha na Biashara (GATT) mwaka 1961 na kwahiyo ni mwanachama wa WTO toka ilipoanzishwa mwaka 1995. Pamoja na hilo, mashirika mengi ya **Umoja wa Mataifa (UN)** yana uwakilishi nchini Tanzania na yanalisaidia taifa katika juhudi zake za kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi.[5] Pia, **balozi** nyingi na **taasisi za misaada** za kitaifa zinahusika kwenye utekelezaji wa sera na miradi ya maendeleo.

5 Angalia Kiambatanisho Na. 2: Taasisi na Mashirika ya Umoja wa Mataifa yaliyoko nchini Tanzania.

Zaidi ya hayo, uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine kibiashara ni muhimu katika kufanya maamuzi na kuwa taifa imara linalojitegemea. **Jumuiya ya Afrika Masharika (EAC)**, miongoni mwa nyinginezo, inawakilisha fursa kubwa katika kutanua soko na ulinzi wa maslahi ya kikanda katika ngazi ya kimataifa. EAC inalenga kuimarisha ushirikiano wa kisiasa, kiuchumi na kimazingira kwa wanachama wote sita (EAC/KAS/Forum CC 2016, uk. vii).

Ikiwa na idadi ya watu milioni 168.5, Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ni soko muhimu kwa bidhaa za Tanzania na hilo linaakisi kanuni kadhaa za Uchumi wa Soko Jamii: unaomaanisha soko huru na wazi na pia ushirikiano wa kikanda na maendeleo endelevu (UNECA n. d.). Toka mwaka 2010, EAC ilifikia hatua rasmi ya **kuungana** katika kufanya biashara huru, kwa maana ya kuondoa vikwazo vyote vya kibiashara kati ya nchi wanachama wa jumuiya, kuanza kutekeleza mfumo jumuishi wa usimamizi wa mipaka na uhuru wa bidhaa na watu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine ndani ya jumuiya. Nchi wanachama walishaonyesha nia yao ya kuwa na umoja wa sarafu (Le Monde 2013). Hata hivyo, mvutano wa ndani kuhusu masuala ya kifedha na kukosekana kwa utashi wa kisiasa wa nchi wanachama ndani ya jumuiya unapunguza kasi ya mchakato wa kuungana (Diawara 2016).

Kwa kujihusisha na uhusiano wa kimataifa na biashara kunasaidia nchi kuweza kushindana na kujifunza kwenye viwango vya kimataifa au misingi ya kutoa huduma na kutengeneza bidhaa.

### *4.3.7 Utaratibu wa Matumizi ya Fedha*

"Sera ya matumizi ya fedha ni muhimu katika manunuzi ya serikali na kuwezesha upatikanaji wa bidhaa za umma na kulipa gharama za usimamizi na utawala" (Benecke 2008, uk. 18) na, kuimarisha ukuaji wa uchumi jumuishi pamoja na huduma za kijamii. Serikali lazima iwajibike katika kuweka miongozo ya aina na viwango vya kodi kwa wafanyabiashara na wananchi (Benecke 2008, uk. 18).

Kwa Tanzania, kodi hukusanywa na taasisi tatu katika ngazi tatu tofauti. Kodi na tozo za serikali za mitaa zinasimamiwa na Mamlaka

za Serikali za Mitaa na kodi zinazohusu manunuzi ya bidhaa na matumizi ya ndani kwa Zanzibar hukusanywa na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB). Ingawa, mamlaka zote hizi mbili zinawakilisha sehemu ndogo ya mapato yote ya ndani ya serikali, na sehemu kubwa inatokana na kodi inayokusanywa na serikali kuu. Kodi zote za upande wa serikali kuu zinasimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). TRA imegawanyika katika idara kuu tatu, ambazo ni Idara ya Kodi za Ndani, Idara ya Walipakodi Wakubwa na Ushuru wa Forodha na Bidhaa (TRA n. D., uk. 1).

Mazingira ya kifedha yanapaswa kuiwezesha serikali kukusanya mapato ili kugharamia upatikanaji wa bidhaa na huduma za umma. Yanapaswa pia yawezeshe uhamasishaji wa rasilimali za ndani. Hii ni muhimu sana kwa nchi kujizuia kuwa tegemezi kwa misaada ambayo huwa inakuja na changamoto nyingi, kama masharti, kucheleweshwa na kutolewa kidogo kuliko kiasi kilichotegemewa. Uhamasishaji mzuri wa rasilimali za ndani ni muhimu kwa nchi kupunguza mikopo ambayo huongeza deni la taifa. Mazingira ya usimamizi wa matumizi ya fedha yanapaswa kuwa rafiki na yenye kuvutia. Mbali na hayo, yanapaswa kutabirika, kwa viwango vya kodi nafuu, vinavyoweza kurejeshwa kwa wakati, vyenye urahisi wa kulipa na mfumo wa kodi wa haki kwa wadau na wenye motisha zenye maana.

Nchi inahitaji mabadiliko ya mifumo ya kodi ili kuleta hamasa ya ukuaji wa biashara na ulipaji wa kodi kwa wakati. Ifuatayo ni mikakati iliyoonekana kuwa muhimu kwenye mabadiliko hayo ya mifumo:

- **Kurekebisha mfumo wa kodi utakaosaidia maendeleo jumuishi ya uchumi**
  Kiwango bora cha kodi kinapaswa kuwa rafiki kwenye uwekezaji ili kuvutia mitaji na kuhamasisha tija kwenye shughuli za kiuchumi na kuruhusu serikali kufanya majukumu yake bila ya vikwazo. Kwa namna nyingine, kodi inapaswa kulingana na uwezo wa uchumi ili kuvutia wawekezaji na kuleta chachu ya ajira. Kodi ya kiwango cha juu kabisa au uwepo wa tozo nyingi vinaweza kupunguza hamasa na shauku kwa wadau kushiriki

katika maendeleo ya uchumi. Hivi karibuni, kiwango cha kodi nchini Tanzania kiliongezeka na kuwachukiza wawekezaji na wajasiriamali ambao wamelalamika kuhusu uwepo wa viwango vikubwa na tozo nyingi ambazo zinahatarisha shughuli zao. Kwa mfano, kodi kwenye eneo kama kuhamisha fedha kwa njia ya simu za mkononi, shughuli za kibenki, huduma za kitalii na usafirishaji wa mizigo zimeongezeka ndani ya miaka miwili iliyopita (Ng'wanakilala/Blair/King 2017). Kwa namna nyingine, kodi haipaswi kuonekana kama hatari, kwa sababu inakwenda kutumika kuleta huduma za kijamii. Pia, mapato yatokanayo na kodi ndiyo njia kuu ya serikali kupata mapato na lazima yatumike kuleta mgawanyo wa kipato ili kuendeleza haki ya jamii.

- **Kupunguza tofauti za kiuchumi kwa kutoza kodi zenye uwiano**
  Hii inapendekezwa ili kujenga mfumo wa kodi ambao, kwa muundo wake, unaongeza usawa na haki kwa jamii. Wakati utozaji wa kodi kwa uwiano utapelekea mgawanyo wa mapato kuwasaidia masikini kwenye jamii; utozaji wa kiwango sawa cha kodi kwa wote, kama vile kodi ya ongezeko la thamani (VAT), uleta tofauti na matabaka kwa sababu huwaathiri wananchi wenye vipato vidogo. Ni muhimu kuhakikisha kila mwenye kipato analipa kodi kwa kiwango chenye uwiano na kipato chake. Haipaswi kuwepo kwa kundi lolote la wanaopata kipato na hawalipi kodi ndani ya nchi.

- **Kubadili fikra kwa kuweka motisha kwenye kodi**
  Hili lina uhusiano na wazalishaji wa bidhaa ambao wameamua kuwekeza kwenye maeneo yasiyovutia kwa wawekezaji wengi au kutoa hamasa ya uwekezaji kwenye sekta fulani muhimu kwa ajili ya kuleta maendeleo jumuishi, kama utalii na kilimo, mbali na nyinginezo. Kupitia SMET, ni jambo lenye thamani kubwa kwa makampuni ambayo yanazingatia kuzalisha na kuleta tija kwa jamii na/au bila ya kuathiri mazingira, makampuni hayo yapewe motisha ili wengine wahamasike ili kuonyesha tabia na thamani kwa jamii, na kusaida kulinda mazingira.

- **Kurekebisha na kuufanya mfumo wa kodi kuwa endelevu**
  Hili ni muhimu ili kupata picha ya jumla ya aina tofauti za kodi zilizopo Tanzania na kufanya maboresho yatakayodumu kwa kipindi kirefu. Mbali na hilo, viwango na aina za kodi hubadilika mara kwa mara. Masuala yote haya mawili yanapaswa kushughulikiwa ili kuweka mazingira rafiki zaidi kwa wawekezaji. Wadau wanapaswa kujua mfumo na kuweka malengo ya uwekezaji, gharama na faida kwa kipindi cha muda wa kati na muda mrefu. Mfumo tata unaweza kuwakatisha tamaa wadau kushiriki shughuli za kiuchumi au kusababisha miradi yao kushindwa kwa sababu ya kupotoshwa na mipango. Kwa kuongezea, mfumo tata na usiofaa unaweka mazingira danganyifu ya ukwepaji wa kodi, ubadhirifu na hivyo kukosa mapato. Kwahiyo, itakua muhimu kurekebisha muundo na kurahisisha mfumo wa kodi nchini Tanzania.

- **Kuhakikisha ufanisi katika ukusanyaji wa kodi**
  Kupungua kwa mapato ya serikali na ufinyu wa rasilimali fedha, ambazo zingeweza kuwekezwa kwenye miundombinu na bidhaa na huduma za umma, vinaweza kuzuilika kupitia uwepo wa ufanisi kwenye mfumo wa ukusanyaji kodi. Kutokana na taarifa za TRA, hali imeboreka kuanzia mwaka 2016 na mapato ya kodi katika kipindi cha kwanza cha mwaka wa fedha wa 2016/17 yalikua 12.74% zaidi ya mwaka wa fedha uliopita. Bado, hatua muhimu inapaswa kupigwa kulingana na changamoto kadhaa zilizopo. Utata wa mfumo wa kodi kwa sasa unapelekea uwepo wa matokeo mawili. Kwanza, ni vigumu kuwatambua na kuwafuatilia wanaokwepa kodi. Pili, watanzania wengi hawajui aina ya kodi ambazo wanapaswa kuzilipa na hawawezi kuzijua hatua zote za kiutaratibu na kuzifuata. Kwahiyo, sehemu ya suluhu ni kuweka juhudi katika kuwajulisha na kuwa karibu na walipa kodi. Pia, sekta kubwa isiyo rasmi inaendelea kufanya ukusanyaji wa kodi uwe mgumu kwa wafanyabiashara wadogo na watu wengine waliojiajiri.

  Makampuni makubwa yanaendelea kuwa chanzo kikuu cha mapato ya kodi katika taifa (Ng’wanakilala/Blair/King 2017). Ili kuhakikisha ufanisi wa kukusanya kodi, zitakuwepo hatua

madhubuti kwa wale wote ambao hawatumii mashine za EFD na TRA wanapaswa kuhakikisha kila mfanyabiashara anapata nafasi ya kumiliki mashine hiyo. Kwa mfano, baada ya kusajili biashara, mashine hizi zingekua zinatolewa na kulipiwa kwa awamu kulingana na makubaliano ili biashara isibebe mzigo huo mwanzoni.

- **Mgawanyo wa mapato ya kodi kati ya mamlaka za serikali kuu na serikali za mitaa**
  Hili linaonekana lina umuhimu ili kuimarisha ugatuzi wa madaraka ngazi za chini na kuwezesha serikali za mitaa kutoa huduma zaidi. Kama ilivyoonekana hapo juu, mapato ya kodi Tanzania yanakusanywa zaidi na serikali kuu. TRA inakusanya kiwango kikubwa cha kodi kwa niaba ya serikali kuu. Kwa maana hiyo, katika makusanyo ya moja kwa moja, serikali za mitaa zinakusanya kiwango kidogo. Kwahiyo, **ili kukidhi** majukumu yao, serikali za mitaa wanategemea mgawanyo wa fedha kutoka serikali kuu. Hii inasababisha urasimu wa mfumo na ulimbikizaji wa madaraka ya serikali kuu. Kwakuwa kanuni ya jamii mahalia kujitegemea na kujiendesha ni miongoni mwa nguzo kuu za mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii, inategemewa kwamba ufanisi zaidi utapatikana kupitia utaratibu wa ugatuzi wa madaraka. Mfumo wa ugatuzi kwenye kodi utazipa serikali za mitaa uwezo zaidi wa kushughulikia na kutoa bidhaa na huduma kwa umma. Kodi zinaweza kukusanywa na mamlaka zote, kulingana na mpango wa pamoja ulioelekeza ambao unatambua mahitaji ya jamuiya ngazi ya chini. Hili linaweza kufanywa kama ifuatavyo:

  a) Kwa kukusanya na kugawanya kiasi kinachokidhi mahitaji ya serikali za mitaa kupitia mamlaka za serikali za mitaa zenyewe, au

  b) Kwa kukusanya kiwango fulani kinachotambuliwa kupitia mamlaka zote, za mitaa na serikali kuu, na serikali kuu kutoa mgawanyo kwa serikali za mitaa kulingana na mahitaji, kanuni ya mgawanyo inaweza kuwekwa kulingana na hatua ya maendeleo ya kiuchumi na hali ya kijiografia ya eneo husika.

### *4.3.8 Utaratibu wa Kijamii*

Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii una taratibu nyingi za kuilinda jamii. Pale ambapo wadau wote wanawajibika, hakuna mwanajamii mbali na hadhi yake kwenye jamii atakayekosa au kuondolewa na kutofaidi matunda ya ukuaji wa uchumi wa taifa. Kwahiyo serikali inahitaji yafuatayo:

- **Kutoa ulinzi kwa jamii kupitia mfumo wa hifadhi ya jamii ulio wazi na rahisi**
  Hili ni muhimu ili kupunguza umasikini na kuondoa utofauti unaokua kati ya aliyenacho na asiyenacho. Kiwango cha umasikini kwa jamii ya watanzania bado ni kikubwa na tofauti kati ya tajiri na masikini inaongezeka. Watunga sera wanapaswa kuhakikisha sera na miongozo inagusa mahitaji ya wadau wote. (a) "Inatakiwa iwe jukumu la kila serikali ya mtaa [...] kukuza ustawi wa jamii na uchumi wa watu wote ndani ya eneo leo la kimamlaka" (LGDAA 1982, 111.(1)). Serikali inatakiwa kukuza ushindani, kulingana na mahitaji ya umma kwenye kujenga uwezo wa kiuchumi na kijamii na kuhakikisha ushirikishwaji kwenye shughuli za kiuchumi kwa kuwawezesha watu na kuwafanya wazalishaji muhimu kwenye jamii. Mtu au kikundi cha watu kilichopungukiwa uwezo kinapaswa kufikiwa na huduma za hifadhi na usalama.

  Mfumo wa hifadhi ya jamii Tanzania kwa sehemu kubwa unategemea bima. Kwahiyo, wanachama wa mfuko wanachangia ili wapate huduma na hifadhi pindi tatizo linapotokea. Kuna mifuko mingi ya pensheni ya umma Tanzania kama ilivyoandikwa katika kifungu cha 3.3 cha chapisho hili. Mwanzoni mifuko mingi ilikuwa inahudumia sekta na kada mbalimbali za kitaalam.

  - **Mfuko wa Pensheni wa LAPF** ulianzishwa mwaka 1944 ili kutoa hifadhi kwa jamii hasa kwa waajiriwa wa "taasisi za asili". Mfuko wa LAPF kwa mara ya kwanza ulianzishwa chini ya Wizara inayohusika na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ila ukawa mfuko unaojitegemea kuanzia mwaka 2000 (LAPF 2018).

- **Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF)** ulianzishwa Julai 1978 kwa waajiriwa wa mashirika na taasisi za umma.

- **Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF)** ulianzishwa mwaka 1999 (PSPF 2018), na **Mfuko wa Pensheni wa Mafao ya Kustaafu (GEPF)**, ulianzishwa mwaka 2002, mwanzo ulihusika na waajiriwa wa huduma za umma na wale walioajiriwa Serikalini kwa mikataba na wale ambao si wanachama wa mfuko wowote (GEPF 2017).

- **Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)** ulianzishwa na kuchukua nafasi ya Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi (NPF) mwaka 1997. Ni mfuko wenye mpango wa lazima unaowezeshwa na michango (inayokatwa kutoka kwenye mshahara wote kabla ya kodi) ya waajiriwa na waajiri (NSSF 2017). Ni mfuko pekee wa pensheni ulioanzishwa kwa ajili ya wafanyakazi wote.

- Upande wa Zanzibar, mfuko huru wa hifadhi ya jamii ulianzishwa mwaka 1998: **Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)**. Ni mfuko wa kwanza wa hifadhi ya jamii kuanzishwa Zanzibar na ZSSF umeendelea kubaki wenyewe sokoni mpaka sasa (ZSSF 2018).

Kufuatia mabadiliko kwenye mfumo wa hifadhi ya jamii miaka ya 2000, kila mwajiriwa na hata yule aliyejiajiri sasa ana uhuru wa kujiunga na mfuko wowote. Inaleta utata na mfumo usioeleweka pale ambapo watu wapo kwenye mifuko tofauti ya hifadhi ya jamii na wanapata pensheni kulingana na taratibu za mifuko hiyo. Kwahiyo, Serikali ya Tanzania inahimiza mkakati wa kuunganisha mifuko ya hifadhi ya jamii kwa kuwa na mfuko mmoja pekee. Ingawa, upinzani ulikuwepo kutoka kwenye mifuko yenyewe – ambayo ilitaka kubaki kama ilivyo – na wanasiasa wengi na asasi za kiraia – ambao wanaogopa uwepo wa mamkala na nguvu itokanayo na mfuko mmoja na hofu ya fedha kutotumiwa vizuri na Serikali. **Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA)** ilianzishwa mwaka 2010 ili kusimamia mfumo wa hifadhi ya jamii na

kuhusianisha kinachotolewa na mifuko ya hifadhi. Mifuko yote ya hifadhi Tanzania inatoa viwango sawa vya mafao, ambavyo vinakidhi mahitaji yote ya kukabiliana na hatari kwa jamii (SSRA 2017).

Hivi karibuni, mifuko ya pensheni inaweza kuunganishwa na bima ya afya. Ila, baadhi ya mipango ya mifuko ya hifadhi ni kutojihusisha na bima ya afya. **Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)** ni mfuko wa bima ya afya. Wanachama na wategemezi (wanafamilia wa karibu) wanaweza kupata huduma ya afya katika vituo vyote vya afya vilivyosajiliwa (Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya 2018). Katika nchi nyingi, huduma ya afya ni sehemu ya hifadhi ya jamii. Ugonjwa ni miongoni mwa hatari za kijamii ambazo inaweza kumzuia mtu asiendelee na kazi na baadaye kupelekea kupata taabu na umasikini. NHIF inafuata mantiki ya bima, ambapo wenye afya huchangia kwenye mfuko na mwanachama yeyote anahakikishiwa hifadhi kupitia michango hiyo. Kwahiyo, mifuko ya hifadhi ya jamii na mfuko wa bima ya afya kwa Tanzania vinaweza kuunganishwa na kuwa mfumo mmoja. Kuunganishwa kwa mifuko yote kutawezesha uwepo wa uwazi zaidi na urahisi wa kuelewa mifumo kwa Watanzania, na kukuza ufanisi wa hifadhi ya jamii. Kwa sababu hifadhi ya jamii ni moja ya kanuni za SMET, na inafikiriwa kwamba, kama mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii utatekelezwa, Watanzania wengi watafaidika kutokana na mifuko ya hifadhi ya jamii, viwango vya pensheni au huduma ya afya kuliko ilivyo sasa.

- **Kuhakikisha hakuna mtu ambaye anaachwa nyuma kupitia mipango ya lazima na misaada ya kijamii**
  SSRA pia imekua ikitafuta uwezekano wa kupanua wigo wa huduma kwa Watanzania wote (SSRA 2017). Hali ya sasa ya mifuko ya hifadhi ya jamii na bima ya afya ni kutoa huduma kwa waajiriwa wa sekta rasmi. Kwa Tanzania, sehemu kubwa ya wananchi wameajiriwa katika sekta isiyo rasmi na hususan sekta ya kilimo. Kwahiyo, mifuko ya hifadhi itakua jumuishi na yenye ufanisi kama **sheria italazimisha kila mwananchi ajiunge na mfumo wa hifadhi ya jamii**. Hatua hii ni vyema

iende sambamba na kuwafundisha wananchi umuhimu wa kuwa na bima, hasa upande wa afya, ili wananchi wachangie kwa hiari. Ingawa, kwa hali ya Tanzania, ambapo idadi ya kaya masikini ni kubwa, kunaweza kuwa na changamoto, au isiwezekane na kwenda kinyume kwa kulazimisha kila mtu achangie fedha kwenye mifuko hii. Sera hiyo itahitaji ruzuku ya umma ili wananchi masikini waweze kupata huduma za hifadhi ya jamii. Kigezo cha kipato kinaweza kutumika ili kuzitambua kaya ambazo hazina uwezo wa kulipia huduma husika na kupewa msaada na serikali. Aina hii ya sera itaimarisha umuhimu wa msaada wa kijamii kwa Tanzania kupitia mpango wa hifadhi ya jamii. Ili kuhakikisha kwamba hakuna mwananchi atakayeachwa nyuma, kunapaswa pia kuwepo mafunzo ili kuleta hamasa na kumwezesha kila mwananchi kutafuta ajira, apate kipato kukidhi mahitaji na kuchangia kwenye mfumo wa hifadhi ya jamii. Pale ambapo ujuzi wa ujasiriamali na utambuzi wa fursa unafahamika, Watanzania wengi watakua wamewezeshwa kustahimili wenyewe. Kwa wale ambao watakua wanapata changamoto kubwa, msaada utakuwepo.

- **Kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora ya msingi kwa wote**

  Hili litakuza vipaji na ushindani wa rasilimali watu. Nchi inaweza kufungua mwanya wa kupata vipaji vilivyojificha na ambavyo havijaibuliwa kwa kuwekeza kwenye mafunzo na elimu. Kama ilivyoelezwa awali, kwa nadharia, kila mtoto Tanzania anaweza kupata **elimu bure ya msingi**. Kwahiyo, mtoto wa Kitanzania anaweza kwenda shule kwa miaka kumi bila ya kulipa ada yoyote (El-Noshokaty/Gebert 2017, uk. 1). Mabadiliko ya mwaka 2011 na 2016 yaliruhusu mamia ya watoto kupata elimu ya umma na idadi ya wanafunzi baadhi ya shule ilipungua (Africa Times 2016). Ingawa, mabadiliko haya yalileta changamoto nyingi. Kwa sasa, wanafunzi wengi wa shule za sekondari wanachukuliwa kama “wanapikwa nusu”, ikiwa na maana kwamba wanamaliza masomo yao bila ya kupata ujuzi na uelewa unaotegemewa. Wanakosa uwezo wa msingi, wanafunzi hao wanapata shida kuendelea na masomo kwenye taasisi za elimu ya juu.

Masuala yafuatayo yanapaswa kushughulikiwa ili kufikia malengo ya elimu jumuishi iliyo bora. Kwanza, kuna uhitaji wa haraka wa vifaa vya kufundishia. Madarasa yaliyosongamana, uhaba wa madarasa yanayofaa na makosa ya kiuandishi kwenye vitabu vya kujifunzia haviruhusu uwepo wa elimu bora. Walimu wanaelemewa na hawawezi kutoa msaada wa moja kwa moja (El-Noshokaty/Gebert 2017, uk. 1). Kwahiyo, ajira za kutosha za walimu na uwekezaji muhimu vinahitajika ili kuendana na uwezo wa shule kumudu ongezeko la watoto. Ujenzi wa madarasa mapya na marekebisho ya vitabu ni muhimu, ingawa haifahamiki kama inawezekana nchi ikawa na fedha za kutosha kukidhi mahitaji hayo. Njia za kiubunifu kuwezesha miradi ya elimu, kama vile vyama vya ushirika vya jamii, vinaweza kutafutwa na kusaidiwa. Tahadhari fulani inaweza kutolewa ili kulinda usawa wa fursa kwa watoto wote.

Pili, walimu wengi na wafanyakazi kwenye taaluma hawana taarifa za kutosha kuhusu mabadiliko mapya ya mitaala na wanapata shida kutekeleza mfumo mpya. Kila mabadiliko makubwa yanapaswa kwenda sambamba na ufanyikaji wa vikao vya kutoa taarifa na programu za mafunzo kwa walimu ili kuhakikisha uelewa wa pamoja wa malengo na njia za mfumo wa elimu Tanzania. Maandalizi mazuri ya wafanyakazi ni muhimu ili kuhakikisha utendani mzuri na wanafunzi kupewa mazingira rafiki ya kujifunzia. Mafunzo haya yanaweza kutolewa na serikali, lakini pia vyama vya walimu kama Chama cha Walimu Tanzania (CWT) au Chama cha Walimu wa Somo la Uraia Tanzania (CETA), kwa kuzingatia kwamba wadau watakaohusika wanakubaliana na maana na malengo ya mabadiliko husika.

Kwa baadaye, kila badiliko kwenye sekta ya elimu linapaswa kuandaliwa vizuri kabla ya kutekeleza, kwa sababu elimu kwa wote haiwezi kufikiwa kwa kuathiri ubora. Zaidi ya hayo, lengo la elimu ya msingi kwa wote halijafikiwa bado. Japokuwa ongezeko la mahudhurio shuleni haliwezi kubezwa, Waangalizi wa Haki za Binadamu walikadiria mwaka 2017 kwamba vijana milioni 1.5 bado hawaendi shule, wakihoji mafanikio ya sera za elimu

(Human Rights Watch 2017). Sababu za haya kutokea ni nyingi. Kwanza, elimu bure bado inaweza kuambatana na gharama kwa familia. Wazazi wanapaswa kulipia usafiri, vitabu na sare za shule. Kwa kaya masikini, gharama hizo bado ni mzigo kwao. Pia, juhudi zinahitajika kulipia gharama za usafiri na vifaa vya kujifunzia, angalau wanafunzi wanne kutoka kaya masikini. Zaidi ya hayo, kaya nyingi za vijijini, watoto husaidia wazazi wao, kwa mfano kwa kuchota maji na pia shughuli za shamba na kazi nyingine za kiuchumi. Pale ambapo watoto wanakwenda shule, familia zao zinapoteza nguvu kazi (El-Noshokaty/Gebert 2017, uk. 3). Suala hili ni gumu kulishughulikia, lakini hasara hiyo inaweza kufidiwa kama kwenda shule kutakua hakuna gharama nyingine yoyote na kuhakikisha mahitaji mengine ya msingi yanagharimiwa. Kwa mfano, programu ya msaada ya jumuiya ya kutoa chakula mashuleni imeonyesha matokea chanya kwenye mahudhurio na ufaulu wa watoto (Cattermole 2012).

Mwisho, ni muhimu kuboresha hali na mazingira, hasa kwa wanawake na walemavu kwenye jamii ili waweze kupata elimu, kuwawezesha kuwa huru kiuchumi na kijamii. Kwa upande mwingine, shule za Tanzania zinakosa vifaa na mazingira rafiki kwa wale wenye ulemavu na walimu hawapati mafunzo maalumu. Kwahiyo, ni vigumu na wakati mwingine haiwezekani kwa wanafunzi kwenda shule (El-Noshokaty/Gebert 2017, uk. 3). Hatua stahiki ni muhimu kuchukuliwa ili kuwezesha wanafunzi hawa wanakua sehemu ya kupata elimu: vifaa maalumu kwenye shule na vyombo vya usafiri, hasa kwa wenye ulemavu wa viungo, uwepo wa walimu maalumu ili wamudu kuwafundisha wanafunzi wenye ulemavu, pia uwepo wa vifaa maalumu vya kujifunzia, fomu maamulu za mitihani au mitaala maalumu, kama vile vitabu maalumu kwa wasioona, kwa mfano. Mahitaji haya ni uwekezaji ambao hauwezi kuonekana kwa haraka, pia yanapaswa yawe agenda ya kufanyiwa kazi ili kuwa na shule zenye mifumo jumuishi. Ni muhimu kuwa na mkakati wa muda mrefu ili kuweza kuboresha hali hii mapema iwezekanavyo. Pia, unyanyapaa – changamoto nyingine inayoathiri mahudhurio shuleni kwa wenye ulemavu – unaweza kupunguzwa kwa kuwaelimisha wanafunzi wengine na walimu. Kwa namna

nyingine, wasichana pia wana changamoto ya kupata elimu kutokana na vikwanzo mbalimbali. Kwa mfano, kumekua na ugumu kuhudhuria masomo kipindi cha hedhi kwa sababu ya kukosa taulo maalumu za kujihifadhi. Pia, kuwahakikishia uwepo wa vifaa vya usafi kunaweza kufanikisha mahudhurio yao shuleni na kuwafanya wawe kwenye hali nzuri. Wakati mwingine wasichana wanakabiliwa na unyanyasaji wa kingono, kushambuliwa na hata kubakwa wakiwa njiani kwenda au kurudi kutoka shule. Watekelezaji wa haya wakati mwingine wanaishia kutochukuliwa hatua, na mimba zinazotokea zinapelekea wasichana hao kuondolewa shuleni upande wa Tanzania bara (El-Noshokaty/Gebert 2017, uk. 4-5). Adhabu hii mara mbili inawapelekea mabinti wengi wadogo kwenye hali ya umasikini na kutengwa. Ili kukabiliana na hilo, inapaswa kuwa na mfumo wa elimu utakaowasaidia wasichana hawa kurudi kwenye jamii na kutafuta njia ya kujinasua kwenye shida hizo. Pia, mfumo mzuri wa uchunguzi na mahakama unapaswa kuhakikisha kwamba wahusika wanakabiliwa na adhabu kali ili kuzuia maovu hayo kutojirudia tena na kuhakikisha mazingira salama kwa watoto wote. Pia, wasichana wanapaswa kuwa huru kusema na kusikilizwa ili kuvunja mila na tamaduni potofu zilizopo, na kushughulikia kwa ufanisi changamoto ambazo zimeelezwa hapo awali.

- **Kuboresha mafunzo ya taasisi za elimu ya juu ili yaendane na mahitaji ya soko la ajira**
  Hili ni muhimu ili kuhakikisha wahitimu wa taasisi za elimu ya juu wanaajirika na kuwa na tija kwenye soko la ajira. Suala kuu katika soko la ajira nchini Tanzania ni upungufu wa watu wenye ujuzi. Ili kufikia maendeleo ya uchumi endelevu, nchi inahitaji rasilimali watu wa kutosha wenye ujuzi na uwezo unaohitajika. Kwahiyo, uhusiano kati ya mfumo wa elimu na sekta binafsi (na wadau wengine ambao hutoa ajira kwa wahitimu wa taasisi za elimu ya juu) unahitaji kuboreshwa.

Kuna aina tatu za elimu ya juu ambazo zinahusisha wadau tofauti. **Vyuo vikuu** wanatoa kile kinachoitwa elimu ya taaluma. Elimu ya kitaalamu kuhusu sayansi na teknolojia za

kisasa inafundishwa kwenye taasisi tofauti kama zile zilizo chini ya **Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)**. Mwisho, elimu ya ufundi, ambayo inahusisha kuendeleza mafunzo kwa vitendo, inatolewa na **Vyuo vya Maendeleo (FDCs)** na **Vituo vya Elimu ya Ufundi (VECs)** (Sumra/Katabaro 2016; uk. 26-27).

Sheria ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005 imeipa mamlaka **Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU)** (TCU 2016a). Tume ilianzishwa Julai 2005 na ilichukua nafasi ya iliyokuwa Tume ya Vibali vya Elimu ya Juu (1995-2005), nchini Tanzania taasisi hii huru itafanya utambuzi, inaidhinisha, inasajili na kutoa vibali kwa vyuo vikuu na vyuo vishiriki. Kwa ujumla, TCU inaunganisha elimu ya juu kwa kuratibu sera na kushauri wadau mbalimbali ambao wanahusika na sekta hii. TCU inavitambua **vyuo vikuu** 33 Tanzania, ambavyo kati ya hivyo 12 ni vya umma; 16 ni vyuo vishiriki, ambavyo kati ya hivyo 2 ni vya umma; na 21 ni kampasi vyuo, vituo na taasisi za vyuo. Ingawa takwimu hizi ni ndogo kuliko nchi nyingine nyingi, ila idadi ya vyuo vikuu na vyuo vishiriki imekua ikiongezeka toka nchi ipate uhuru. Maendeleo hayo muhimu, Tanzania sasa inaweza ikafundisha wataalumu wake yenyewe, watafiti na wanataaluma. Hata hivyo wahitimu wengi wa vyuo wanakosa ajira baada ya kumaliza masomo yao, kutokana na sababu nyingi. Mosi, wanafunzi wengi wa vyuo wanahangaika kutumia njia ngumu ambazo zinaweza kueleweka kama ujuzi wa msingi. Mbali na hilo, wanafunzi wa vyuo wanapaswa kukitumia vizuri Kiingereza, wakati elimu ya msingi na sekondari kwa sehemu kubwa zimefanywa kwa lugha ya Kiswahili. Masuala haya yanapaswa kupunguzwa kwa kuboresha elimu ya msingi, kama ilivyogusiwa hapo juu. Suala jingine ni pengo kati ya lengo la kuundwa kwa taasisi hizi na ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira. Kwa hakika, chuo kinamwandaa mwanafunzi kwa ajili ya uwezo wa kitaaluma, lakini ni wanafunzi wachache tu wanaopata ujuzi wa kufanya kazi kwa vitendo. Kwahiyo, eneo ambalo linapaswa kutazamwa ni watu washauriwe namna wanavyochagua taasisi za elimu ili wakajifunze kulingana na mipango yao ya kazi za baadaye. Kipaumbele si muhimu kiwe kwenye chuo anachotaka kusoma, na kupuuza taasisi zinazofundisha utaalamu na ufundi. Pia,

mtaala wa chuo unapaswa ulenge kukuza ujuzi na utaalamu. Mbali na hilo, mitaala ya vyuo inapaswa kuwawezesha wanafunzi kufanya kazi za kujitolea, ili wapate mafunzo kwa vitendo na ujuzi muhimu katika maeneo yao ya taaluma.

Katika mazingira ya sera za serikali kuelekea nchi ya viwanda, Tanzania inapaswa kujikita zaidi kwenye mafunzo ya kitaalamu na elimu ya ufundi kwa sababu watendaji wenye ujuzi wanahitajika kufanyakazi kwenye viwanda. Elimu ya ufundi nchini Tanzania inatolewa na vyuo vya ufundi, ambavyo vinasimamiwa na **NACTE**. NACTE ni taasisi iliyoundwa kisheria ikiwa na majukumu makuu matatu: kuanzisha utaratibu wa kuratibu elimu ya ufundi, kuhakikisha ubora wa elimu kwa kuzisaidia taasisi za ufundi na kushauri wadau wa kisiasa na elimu kuboresha elimu ya ufundi kulingana na mahitaji ya soko la ajira (NACTE 2015b). Hata hivyo, kuna taasisi nyingi zinazojihusisha na elimu ya ufundi. Mosi, wahitimu wa elimu ya msingi wanaweza kupata mafunzo na ujuzi muhimu kutoka kwenye **Vituo vya Ufundi** (Sumra/Katabaro 2016, uk. 30). Pili, **FDCs** vilianzishwa mwaka 1975, vikilenga watu wazima kutoka vijijini. Jumla ya FDCs 55 nchini – karibu vyuo viwili kila mkoa – vinatoa ujuzi katika sekta mbalimbali kama kilimo, uashi au ushonaji. Wanafunzi wa FDCs pia wanajifunza kutumia teknolojia inayohitajika kwenye sekta husika. Pia wanapokea elimu ya ujumla – uongozi, utawala bora, masuala ya jinsia – na lugha ili kuwahakikishia uelewa mzuri wa Kiswahili na Kiingereza (MCDGC 2017). Ingawa, kutokana na taarifa ya **Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)**, Vituo vya Elimu ya Ufundi na vyuo vya FDCs vinakabiliwa na changamoto nyingi. Kwa mfano, vituo haviaminiki suala ambalo linapelekea tatizo la kutotumika vizuri kulingana na uwezo. Kuhusu FDCs, VETA ambavyo vinaongoza kitaifa – vyuo hivyo vimewekwa chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Watoto na Jinsia – ili kutoruhusu uhuru wa aina yoyote na kuendana na mahitaji ya eneo, jambo ambalo limepunguza manufaa ya taasisi hizi (VETA 2018a) VETA ni taasisi ya serikali iliyo huru ambayo ilianzishwa mwaka 1994. Kama ilivyo NACTE, VETA inalenga katika kutengeneza utaratibu

wa uratibu na kuboresha taasisi za elimu ili kuhakikisha ubora na elimu ya ufundi kulingana na mahitaji (VETA 2018b). Mamlaka hii pia inasimamia VECs. Taasisi kama NACTE na VETA zinapaswa kufanyiwa maboresho ili kuwezesha uratibu mzuri wa taasisi ambazo ziko chini yake. Ni wadau muhimu wa kuwaunganisha wafanya maamuzi ya kisiasa na wadau wa elimu ili kuboresha sera ambazo zinaunganisha mahitaji na uwezo wa wadau wote. Hili linamaanisha uhuru walionao unapaswa kulindwa ili waweze kutoa uwakilishi mzuri wa mtazamo wa nje.

- **Kutumia uwezo wa rasilimali watu**
  Kwa mujibu wa taarifa ya Nitisha (2013), mtaji wa nguvukazi ni moja ya vigezo muhimu vya maendeleo ya kiuchumi katika nchi. Ubora na kiasi cha rasilimali watu kilichopo kina athari za moja kwa moja katika ukuaji wa uchumi. Mathalani Tanzania ina idadi kubwa ya watu ambao ni vijana kama ilivyoelezewa katika kifungu cha 3, nguvu kazi hiyo kubwa ni ile isiyo na sifa. Vigezo vya rasilimali watu vinategemea kwenye ujuzi, uwezo wa kubuni, mafunzo na elimu ya watu. Uhaba wa nguvu kazi yenye ujuzi huzuia ukuaji wa uchumi. Ili kuwa na nguvu kazi yenye sifa na iliyoandaliwa, mabadiliko yaliyopendekezwa awali yanahitajika.

  Mbali na hilo, ukosefu wa ajira kwa wahitimu wa vyuo ni jambo linaloenea nchini Tanzania. Kupambana na ukosefu wa ajira, kwanza ni muhimu kupunguza gharama zinazohusiana na muundo na misuguano, kwa kurahisisha uhusiano kati ya waajiri na waajiriwa. Huduma za kutafuta na kujaza nafasi za kazi pamoja na mafunzo zinatolewa nchini na Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA), wakala wa serikali iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu (TaESA 2012). Huduma hii inapaswa kuendelezwa na matangazo kwa umma yanapaswa kuandaliwa ili kutoa taarifa kwa Watanzania wote kuhusu fursa zilizopo na haki zao. Kuendelea kutoa elimu kwa watu wazima ili kupanua uelewa wao na kuboresha nafasi zao na utendaji katika soko la ajira. Hili linaruhusu kujiendeleza kwenye taaluma zao na kuendana na maendeleo, kama uwepo

wa teknolojia mpya. Pia ni njia ya kupambana na ukosefu wa ajira wa muda mrefu, kwa sababu watu waliopata mafunzo wanakua na ufanisi zaidi au wanaweza kuhama kwenda kwenye taaluma nyingine kama sekta yao ya awali haina uhitaji kwenye soko.

Kwa kuhitimisha, mtaji wa binadamu kwa mtanzania unaweza kutumiwa kwa ufanisi kama kuna maelewano kati ya wadau wa uchumi, siasa na elimu. Ushirikiano huu unaweza kuleta utendaji mzuri wa kiuchumi pia kupunguza tatizo la ajira na kupunguza umasikini. Juhudi hizi zote zinapaswa kuongeza ushindani wa kimataifa, mafanikio ya Tanzania na ustawi wa jamii.

- **Maendeleo endelevu**
  Matumizi endelevu ya maliasili ni muhimu ili kufaidika kutokana na rasilimali hizi sasa na baadaye. Kwahiyo, Tanzania lazima iunganishe na kuhusianisha malengo ya maendeleo katika suala la mazingira na uendelevu wake – kama Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa (UN) – kwenye sera za kijamii na kiuchumi. Masuala ya matumizi na uzalishaji endelevu, kupunguza uchafuzi wa mazingira, kupunguza utegemezi kwenye nishati ya mafuta lakini pia kuzingatia mahitaji ya mifumo ya uchumi wa sasa lazima vizingatiwe ili kuhakikisha kuna ukuaji jumuishi na endelevu wa uchumi nchini Tanzania.

### *4.3.9 Eneo la Kuzingatia: Sekta ya Kilimo*

Kilimo ni suala kubwa na muhimu kwenye ajenda ya maendeleo ya uchumi wa Tanzania. Katika maeneo mengi ya nchi, kilimo bado ni nyenzo muhimu katika maisha ya watu wa vijijini, na kinachangia kwa sehemu kubwa ubora wa maisha ya watu hao (Mufuruki et al. 2017). Nchini Tanzania, sekta hii na maendeleo yake bado ina mchango mkubwa kwenye ukuaji wa uchumi, upatikanaji wa kipato na kupunguza kiwango cha umasikini. Sekta hii inatoa ajira kwa takriban theruthi mbili ya wananchi wote na inaweza kuchangia kwenye mauzo ya nje na pato la taifa (Wizara ya Fedha na Mipango 2016, uk. 18). Uzalishaji wa mazao ni asilimia 20 hadi

40 tu ya uwezo wa uzalishaji, na masoko ya pembejeo pamoja na bidhaa za mazao ya kilimo bado hayajaunganishwa vizuri nchini. Kwakuwa maeneo ya vijini yako kwenye lindi la umasikini na zaidi ya asilimia 25 ya wakazi wa vijijini wanaishi chini ya mstari wa umasikini, ufanisi katika sekta ya kilimo unapaswa uendelee kufanyiwa maboresho (World Bank Group 2017d, uk, 18-19). Mbali na hayo, kilimo kinazalisha malighafi kwa ajili ya viwanda vya ndani. Kwa kuongezea mchango wake kwenye viwanda vya usindikaji, bidhaa za kilimo zinaongeza tija kwenye viwanda hivyo nakuongeza ufanisi wa mnyororo wa thamani wa bidhaa tofauti. Pia, viwanda vinatoa ajira kwa watu wengi (URT 2017, uk. 1).

Wakati huo huo, matokeo ya mabadiliko ya tabia nchi yameanza kuonekana Tanzania na yataweza kuathiri na kuwa tishio kubwa nchini katika kipindi cha miaka ijayo. Uelewa mdogo, kutokuwepo kwa taarifa na mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kunaongeza ukubwa wa tatizo. Kwa upande mmoja, watu wana elimu ndogo ya mabadiliko ya tabia nchi na matokeo yake. Vivyo hivyo, taasisi ambazo zimepewa jukumu la kushughulikia suala hili, hazina rasilimali na vitendea kazi. Kwahiyo ni muhimu kuwafundisha Watanzania kuhusu mabadiliko ya tabia nchi, kuboresha uelewa ndani ya taasisi, kuongeza bajeti na kufafanua mikakati ya kukabiliana na tatizo lililopo. Masuala ya kimazingira yanapaswa kuangaliwa kwa umakini na watunga sera na kuchukuliwa kama suala kuu kwenye utungaji wa sera huhusu masuala ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kimaendeleo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania karibu 80% ya Watanzania wanategemea mapato yatokanayo na kilimo ili waendeshe maisha yaos (Vice President’s Office 2012). Kwahiyo, sehemu kubwa ya jamii ya Watanzania wako kwenye hatari ya kupata madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi. Kilimo pia kinakabiliwa na ongezeko la joto duniani na hali mbaya ya hewa, kama vile ukame na mafuriko, na inaambatana na uhaba wa miundombinu, mambo yanayoiacha Tanzania kwenye hatari kubwa kukabiliwa na matokeo hasi ya mabadiliko ya tabia nchi. Uharibifu wa ardhi na misitu – mara nyingi vimesababishwa na binadamu – vinaendelea

kukuza tatizo. Athari mbaya za mazingira pia zinaonekana kiuchumi, kama ilivyofafanuliwa kipindi ambapo ukuaji wa uchumi ulikadiriwa kukua kwa 6.9% mwaka 2005 ulishuka hadi 6.8% kutokana na ukame wa mwaka huo (Ofisi ya Makamu wa Rais 2012). Hili linakazia umuhimu wa kilimo kwa Tanzania, hatari sekta iliyonayo kwenye mabadiliko ya tabia nchi, pia uhitaji wa sera endelevu za maendeleo.

Kama ilivyotajwa awali, takriban 66% ya Watanzania wameajiriwa kwenye sekta ya kilimo. Hata hivyo, kiwango kidogo cha tija katika sekta hiyo kinamaanisha kuna changamoto kubwa, kwakuwa sekta ya kilimo inachangia 29% pekee kwenye pato la taifa (URT 2017, uk. 1). Kilimo ni sekta msingi inayoweza kuleta mageuzi makubwa katika maendeleo ya uchumi nchini (Tanzania Invest 2018a). Kwahiyo, mikakati ifuatayo itasaidia:

- **Kupunguza utegemezi kwenye mvua**
  Kama ilivyoonekana, mabadiliko ya tabia nchi tayari yanaiathiri Tanzania kwa sehemu kubwa. Kwahiyo, kutegemea maji ya mvua kunaendelea kuwa suala muhimu ambalo linapaswa kushughulikiwa. Tanzania imebarikiwa kuwa na vyanzo vingi vya maji ya asili (mito na maziwa) ambavyo vinaweza kutumika kwa ajili ya umwagiliaji. Hii linamaanisha ujenzi wa miundombinu mipya unatakiwa. Gharama za awali zinaweza kuwa kubwa, ila uwekezaji unaweza kuwa wa faida kutokana na matokeo chanya yatakayotokea kwenye sekta ya kilimo. Gharama hizi zinaweza kuchukuliwa na sekta binafsi kama wawekezaji watapata faida katika mpango wa muda wa kati au muda mrefu. Pili, uwezo wa maji ya mvua haujaweza kutumika vizuri. Kuyavuna na kuyahifadhi maji ya mvua ni rahisi na ni mchakato wenye gharama ndogo, ambao utaboresha sana hali ya wakulima msimu wa kiangazi.

- **Kusaidia maendeleo ya kilimo**
  Sekta ya kilimo Tanzania kwa sasa ni duni kutokana na matumizi madogo ya teknolojia lakini pia imetawaliwa na wakulima wadogo wadogo. Kwahiyo, inasafari ndefu ili iweze kuwa na ushindani katika masoko ya kimataifa. Lakini sekta ya

kilimo pia inatoa fursa ya kuchagua aina gani ya maendeleo yanayotazamiwa kwa ajili ya nchi na kuandaa mikakati ipasavyo. Hatua zitakazochukuliwa, ni lazima zikidhi malengo ya muda mrefu. Tanzania inapaswa kuiendeleza sekta ya kilimo kwa uhifadhi wa mazingira na kutafuta ufumbuzi endelevu wa changamoto za kilimo. Kwa mfano, kilimo cha mazao mseto kinapunguza kasi ya uharibifu wa ardhi na kupunguza matumizi ya maji kwenye udongo. Shughuli zenye kuleta uharibifu zinapaswa kupunguzwa. Kwa kuanzisha njia nzuri za kiikolojia katika uzalishaji, Tanzania inachangia kupungua kwa uharibifu wa mazingira. Mbali na hilo, inaweza kuchukuliwa kama chaguo sahihi kiuchumi kwa sababu uendelevu unahitajika na pia taratibu za kimataifa ni muhimu kuzizingatia.

Kuna uhitaji mkubwa kwa wakulima wa Tanzania kukifanya kilimo chao kiwe cha kisasa. Tafiti za kisayansi na kiteknolojia zinatoa fursa za kuongeza tija na ufanisi kwenye sekta ya kilimo. Hata hivyo wakulima wa Tanzania mara nyingi wanakosa uelewa wa namna ya kutumia mbinu mpya za kuboresha kilimo chao. Changamoto hii inaweza kushughulikiwa kwa kuwezesha upatikanaji wa maafisa ugani na au mabwana/mabibi shamba kila kijiji. Kumekua na uhaba wa wataalamu hawa hata kwenye ngazi ya kata, na baadhi ya wale waliopo hawana uelewa wa kutosha wa teknolojia mpya za kilimo na njia endelevu za kukabiliana na masuala ya sasa. Kwahiyo, idadi ya maafisa ugani/mabwana au mabibi shamba inapaswa kuongezwa na kujengewa uwezo ili ujuzi wao uongezeke (The Citizen 2017).

Kwa ujumla, sekta ya kilimo itahitaji uwekezaji mkubwa ili ifikie malengo yake. Kama ilivyo kwenye sekta nyingine, Uchumi wa Jamii unahamasisha ushiriki wa wawekezaji binafsi ili watoe fedha kwa ajili ya kuboresha sekta ya kilimo. Kwa sababu serikali haiwezi kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya maendeleo ya kilimo, mtaji kutoka kwenye vyanzo vingine utahitajika.

- **Uhamishaji wa nguvukazi na utoaji wa elimu vijijini**
  Njia zote mbili zinasaidia kuifanya sekta ya kilimo Tanzania kuendelea na kuwa na tija. Kutokana na hilo, uzalishaji

utaongezeka, ikiwa na maana kwamba gharama za uzalishaji zitapungua – zaidi ya yote, nguvukazi kidogo – itahitajika kuzalisha kiasi kile kile au nguvu kazi ileile itaweza kuzalisha kiasi kikubwa cha mazao. Hili litapelekea kupungua kwa gharama za uzalishaji na kwahiyo bei ya bidhaa itapungua. Kwa njia hii, kilimo cha Tanzania kitakua chenye ushindani kwenye masoko ya kimataifa na bidhaa za chakula zitapatikana kwa bei nafuu kwa walaji. Kwa sababu ya idadi kubwa ya wanafanyakazi wanaojihusisha na sekta ya kilimo, ili kufaidika, hatua hizo zinapaswa kwenda sambamba na mikakati ya kurahisisha mafunzo ya kitaalamu na kuwezesha kuhama kwa wafanyakazi. **Mafunzo kwa wakulima kwenye eneo la ujasiriamali kwenye kilimo yataweza kuwapa ujuzi wa masoko ambao utawawezesha** wajiamini kwenye masoko na kutafuta majibu ya changamoto wakati huo huo wakiendeleza biashara zao.

## 4.4 Hatua za Utekelezaji

Mfumo wa uchumi wa Tanzania utaweza kufanyiwa mageuzi kwa kuzihusisha taasisi zilizopo kwenye mchakato. Mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii nchini Tanzania, SMET, unaweza kutekelezwa katika ngazi tofauti na kwa kupitia jumuiya na mitandao mbalimbali na kuanzia hapo ufahamu utaweza kusambazwa kwenye ngazi zote za taasisi na jamii ili uwe mfumo wa uchumi unaotokana na watu, kulingana na makubaliano, idhini na michango yao.

### *4.4.1 Utekelezaji wa SMET kupitia Jumuiya za Dini*

Jukumu kuu la msingi la kuongeza ufahamu na kutekeleza SMET linaweza kuhusisha viongozi wa kidini kupitia taasisi kama Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Baraza Kuu la Waislamu wa Tanzania (BAKWATA) na miamvuli mingine ya taasisi za kidini. Kwa hakika, kutokana na umuhimu wa dini ambao upo kwenye maisha ya Watanzania wengi, muundo na kanuni ndani ya jumuiya za kidini vina matokeo yanayokubalika, ambayo yanasambaa mpaka nje ya mipaka ya taasisi husika. Kuuwasilisha mfano wa mfumo huu wa uchumi kwa viongozi wa dini wa kitaifa na kuwafundisha kanuni za SMET

kutapelekea maamuzi ya mabadiliko kwenye dira, muundo na namna ya kuendesha taasisi zao. Hili litaleta matokeo chanya kwenye maeneo ya ngazi za chini na litamfikia muumini mmoja mmoja wa taasisi hizo za dini na hivyo wananchi wengi watakuwa wamefikiwa.

### *4.4.2 Utekelezaji wa SMET kupitia Wawakilishi wa Kisiasa*

Serikali pamoja na bunge wanaweza kuanzisha utaratibu mpya na sheria ambazo zitaboresha utekelezaji wa mfumo wa SMET. Hili litaweza kufanikiwa kupitia njia ya kuusambaza mfumo kwa wafanya maamuzi katika ngazi zote muhimu. Kwahiyo, mafunzo yanapaswa kuandaliwa kwa viongozi wa kitaifa (mfano Mawaziri, Wabunge, Kamati Maalumu za Bunge n.k), ngazi ya wilaya (mfano Madiwani, Maafisa wa Wilaya n.k) na ngazi ya kata (mfano wenyeviti wa mitaa, wanakijiji n.k). Ingawa, ni muhimu pia kuutambulisha mfumo huu wa uchumi kwa wananchi wa ngazi za chini kabisa, kwa kuwa mpiga kura mwenye ufahamu na taarifa anaweza kufanya maamuzi ya kina na sahihi ya kuzifanyia tathmini sera za umma na kuwachagua wawakilishi wake.

### *4.4.3 Utekelezaji wa SMET kupitia Sekta Binafsi na ya Umma*

Mfumo unapaswa kutambulishwa kwa wadau wa sekta binafsi, wa kitaifa na kimataifa, kwani ni miongoni mwa wadau muhimu sana wa mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii. Faida za SMET lazima zisisitizwe ili kuwashawishi wadau wa sekta binafsi kuchukua sehemu ya awali ya utambulisho wa mfumo. Sekta binafsi na jamii kwa ujumla ni wanufaikaji wakuu wa SMET kwani mfumo unaruhusu uhuru na ushindani wa haki, uwepo wa haki ya kumiliki mali na kujitegemea. Wajasiriamali, wamiliki wa biashara wadogo, wakati na wakubwa, na vyama vya biashara vyema hawa wafuatwe na kujulishwa wazo la SMET. Kwa kuongezea, taasisi kwenye sekta ya elimu, ikiwemo shule na taasisi za elimu ya juu, wakiwemo wabia wa jamii, mfano waajiri na vyama vya waajiriwa na wadau kutoka sekta ya umma wanapaswa kufuatwa kuutambulisha mfumo na kuomba kujitoa kwao hasa katika kuutekeleza.

### *4.4.4 Utekelezaji wa SMET kupitia Asasi za Kiraia*

Kwa utekelezaji wenye mafanikio, mfumo wa SMET unapaswa uwasilishwe, ueleweke na uungwe mkono na asasi za kiraia. Utekelezaji unaoanzia ngazi ya juu kwenda chini bila ya kuzingatia mahitaji na vipaumbele vya watu na jamii ya ngazi ya chini unaweza kuleta utata na hata kuathiri thamani na miiko ya mfumo. Ili kuwa na ukuaji jumuishi na endelevu na kwa kuzingatia uhuru wa mtu binafsi, SMET lazima itambulishwe kwa asasi za kiraia na mashirika yake. Zaidi ya hayo, ushiriki mzuri wa mashirika haya utasaidia kueneza elimu/uelewa wa mfumo huu mpya wa uchumi kwa wananchi wengi na hivyo kuufanya upokelewe vizuri, jambo ambalo litarahisisha utekelezaji wake.

## 5. Hitimisho

Mwenendo wa ujumla wa maendeleo ya dunia unaonyesha kwamba, uchumi wa soko jamii unaleta mafanikio ya kiuchumi, ubunifu na ubora wa bidhaa na huduma. Muhimu zaidi, mapungufu ya uchumi huo yanapatiwa ufumbuzi na mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii, kama ilivyoshuhudiwa nchini Ujerumani na nchi nyingine za Ulaya. Mfumo wa SMET unatoa fursa ya kuibadilisha Tanzania kuwa nchi yenye nguvu, imara na jumuishi, ambayo imendelea kiuchumi na kijamii. Aliyekua Rais wa Ghana, John Kufuor alikubali wazo kuwa Afrika itumie mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii, wazo ambalo Mwalimu Julius K. Nyerere aliwahi kulitaja kwa namna tofauti na alipendekeza kwamba maendeleo ya kweli yapo ndani ya nguvu ya watu. Hili linapaswa kuwahimiza Watanzania kwamba sasa ni muda wa mabadiliko katika mfumo wa uchumi.

Mfumo huu unasisitiza kwamba maarifa na ujuzi uliopatikana kwenye ngazi za juu unakwenda kwenye ngazi za chini ili wadau wote washiriki kwenye shughuli za kijamii na kiuchumi. Mfumo huu unaweza pia kutumika nchi nzima endapo Serikali itaona manufaa yake. Mchakato wake unaweza kuanzia kwa viongozi kwenda kwa wananchi wanaoishi maeneo ya vijijini na mijini. Haya yanaweza kuhusisha uwasilishaji wa mfumo huu wa kiuchumi kwa viongozi mbalimbali ngazi ya kitaifa, mikoa, wilaya, kata na vijiji ambapo baadaye uelewa utazifikia kaya na mtu mmoja mmoja.

Uwekezaji katika elimu ni sera za kijamii muhimu ambazo zinawezesha watu wengi kuwa waangalifu na kujihudumia wao wenyewe na familia zao, ambapo wataweza kuzitumia fursa zitazowafikia kupitia mfumo wa Uchumi wa Soko Jamii kwa Tanzania. Watu masikini na fukara hawapaswi kutengwa na jamii au kuachwa nyuma, kwahiyo umakini unahitajika ili kuboresha hali zao za maisha.

Ili kufikia maendeleo yanayokusudiwa, inashauriwa kwamba Tanzania ikubali kupokea na kutekeleza Uchumi wa Soko Jamii kama mfumo mpya wa uchumi unaohimiza ukuaji shirikishi na endelevu kwa taifa na watu wake wote.

# Viambatanisho

## Kiambatanisho Na. 1: Orodha ya Mashirika ya Umma Tanzania

| Majina ya Mashirika ya Umma Tanzania Bara |
|---|
| Bodi ya Biashara ya Nje (BET) |
| Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) |
| Hoteli ya Mikumi Wildlife Lodge |
| Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO) |
| Kampuni ya Bidhaa za Mbao ya Imara |
| Kampuni ya Highland Estate |
| Kampuni ya Huduma ya Cooper Motors (CMSC) |
| Kampuni ya Huduma ya Meli (MSCL) |
| Kampuni ya KILTIMBERS |
| Kampuni ya Kukodisha Mitambo (PEHCOL) |
| Kampuni ya Kusafisha Mafuta ya Tanganyika na Italia (TIPER) |
| Kampuni ya Maendeleo ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO) |
| Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) |
| Kampuni ya Maji Songwe |
| Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) |
| Kampuni ya Meli China – Tanzania |
| Kampuni ya Meli ya Taifa |
| Kampuni ya PUMA Energy Tanzania |
| Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) |
| Kampuni ya Reli Tanzania (TRL) |
| Kampuni ya Setchet |
| Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) |
| Kampuni ya Tanganyika Packers |
| Kampuni ya Uwekezaji wa Mahoteli Tanzania (TAHI) |
| Kampuni ya Vifaa vya Elimu Tanzania |
| Kampuni ya Vifaa vya Ujenzi (BHESCO) |
| Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) |

| |
|---|
| Kituo cha Teknolojia ya Mitambo Inayojiendesha (TATC) – NYUMBU |
| Kiwanda cha Kutengeneza Matairi Afrika Masharika cha General Tyre |
| Kiwanda cha Ngozi Morogoro |
| Kiwanda cha Tembo – Chipboards |
| Kiwanda cha Vifaa vya Mashine Kilimanjaro |
| Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) |
| Mashamba ya Mahindi Mbozi |
| Mashamba ya Mpira Kalunga |
| Mashamba ya Mpira Kihuhwi – Muheza |
| Shamba la Basuto |
| Shamba la Gidagamowd |
| Shamba la Mulbadaw |
| Shamba la Murjanda |
| Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC) |
| Shirika la Bima la Taifa (NIC) |
| Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) |
| Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) |
| Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) |
| Shirika la Mzinga |
| Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) |
| Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) |
| Shirika la Reli ya pamoja ya Zambia na Tanzania (TAZARA) |
| Shirika la Taifa la Kilimo na Chakula (NAFCO) |
| Shirika la Umeme la Tanzania (TANESCO) |
| Shirika la Usagishaji la Taifa (NMC) |
| Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) |
| Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) |
| Soko la Kariakoo |
| Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC) |
| Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TASUBA) |
| Taasisi ya Uhandisi na Usanifu wa Mitambo ya Tanzania (TEMDO) |
| Wakala wa Huduma ya Ununuzi na Ugavi Serikalini (GPSA) |
| Wakala wa Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) |
| Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali |

| |
|---|
| Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) |
| Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) |
| Wakala wa Mbegu za Miti (TTSA) |
| Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) |
| Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA) |
| Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) |
| Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA) |
| Wakala wa Usafiri wa Haraka (DART) |
| Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) |

| **Majina ya Mashirika ya Umma Zanzibar** |
|---|
| Hoteli ya Amani |
| Hoteli ya Bwawani |
| Furaha ya Visiwani Zanzibar |
| Sauti ya Tanzania Zanzibar |
| Shirika la Bandari |
| Shirika la Biashara ya Magari |
| Shirika la Meli |
| Shirika la Utalii |
| Television ya Zanzibar (TVZ) |
| Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) |
| Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) |

Chanzo: Bank of Tanzania (2014), “ANNEX 3: Public Non-Financial Corporations (Parastatals)”, *List of Government Units, Parastatals, other Depository Corporations (Banks) and other Financial Corporations*, p. 6-7

## Kiambatanisho Na. 2: Taasisi na Mashirika ya Umoja wa Mataifa nchini Tanzania




Chanzo: United Nations Tanzania (2015), "Resident Agencies", *UN Agencies in Tanzania*, available at: http://tz.one.un.org/who-we-are/un-agencies-in-tanzania [viewed on 23th February 2018]

# Rejea


**Abiona, O./Koppensteiner, M. F. (2018).** Financial Inclusion, Shocks and Poverty: Evidence From the Expansion of Mobile Money in Tanzania, March 2018, available at: https://www.researchgate.net/publication/323959526_FINANCIAL_INCLUSION_SHOCKS_AND_POVERTY_EVIDENCE_FROM_THE_EXPANSION_OF_MOBILE_MONEY_IN_TANZANIA [viewed on 31 August 2018]

**AfDB (African Development Bank) (2015).** *Renewable Energy in Africa: Tanzania Country Profile,* Cote d'Ivoire, available at: https://www.afdb.org/fileadmin/uploads/afdb/Documents/Generic-Documents/Renewable_Energy_in_Africa_-_Tanzania.pdf [viewed on 27 July 2018]

**AU (African Union) (2003).** *List of Countries which have signed, ratified/acceded to the African Charter on the Rights and Welfare of the Child,* available at: https://au.int/sites/default/files/treaties/7773-slafrican_charter_on_the_rights_and_ welfare_of_the_child_1.pdf [viewed on 31 August 2018]

**AfDB/Organisation for Economic Co-operation and Development(OECD)/United Nations Development Programme (UNDP) (2017).** *African Economic Outlook – Tanzania 2017*, available at: http://www.africaneconomicoutlook.org/ [viewed on 04 May 2018]

**Africa Times (2016).** *Free education in Tanzania.* Africa Times (2016-02), available at: http://africatimes.com/2016/02/09/free-education-in-tanzania/ [viewed on 14 November 2017]

**Afxentiou, P.C. (2000).** *Convergence, the Maastricht Criteria, and Their Benefits*, The Brown Journal of World Affairs, Vol. 7, Issue 1

**Andersen, T. M./Holmström, B./Honkapohja, S./Korkman, S./Söderström, H. T./Vartiainen, J. (2007).** *The Nordic Model – Embracing globalization and sharing risks*, The Research Institute of the Finnish Economy, available at: https://economics.mit.edu/files/5726 [viewed on 20 February 2018]

**ATE (Association of Tanzania Empolyers) (2018).** *About Association of Tanzania Employers (ATE)*, Association of Tanzania Employers, available at: http://www.ate.or.tz/about [viewed on 21 February 2018]

**Baumgartner, A. (2012).** *Solidarität als sozialethisches Prinzip,* in: Gabriel, Ingeborg/Renöckl, Helmut (Ed.): Solidarität in der Krise, Wien - Würzburg, pp. 59-66

**Benecke, D. W. (2008).** *Social and Ecological Market Economy – A General Overview*, in: Kuesel, Corinna/Dr. Maenner, Ulrike/ Meissner, Ricarda (Ed.): *The Social and Ecological Market Economy – A Model for Asian Development?* Deutsche Gesellschaft für Technische Zusammenarbeit (GTZ) GmbH., Eschborn: pp. 23-52

**BoT (n. d.).** *About the Bank – Primary Objective and Function of the Bank,* available at: https://www.bot.go.tz/AboutBOT/BOTFunction.asp [viewed on 31 August 2018]

**BoT (2017).** *Monetary Policy Statement 2017/18,* Governor Bank of Tanzania, available at: https://www.bot.go.tz/Publications/MonetaryPolicyStatements/Monetary%20Policy%20ENG%202017-18.pdf [viewed on 27 June 2018]

**BoT (2018).** *Foreign Exchange Rates*, Bank of Tanzania, available at: https//www.bot.go.tz/en/ [viewed on 29 June 2018]

**Bringinshaw, D. (2017).** *Tanzania launches standard-gauge railway project,* in: International Railway Journal, April 13, 2017, available at: http://m.railjournal.com/index.php/africa/tanzania-launches-standard-gauge-railway-project.html [viewed on 31 August 2018]

**Bureau of International Narcotics and Law Enforcement Affairs (2015).** *International Narcotics Control Strategy Report* (INCSR).

